# UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KIFONOLOJIA NA KIMOFOLOJIA YANAYOJITOKEZA KATIKA KAZI ANDISHI ZA WANAFUNZI WA SHULE ZA UPILI, TIGANIA, JIMBO LA MERU

**SHADRACK KIRIMI NYAGAH**

**Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika masomo ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.**

**2016**

## UNGAMO

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo chochote kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Sahihi……………………………………..…… Tarehe…………………………

**Shadrack Kirimi Nyagah**

(Mtahiniwa)

Nambari ya usajili: C50/76241/2014

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi……………………………………..…… Tarehe…………………………

**PROF. JOHN HABWE**

(Msimamizi)

Sahihi……………………………………..…… Tarehe…………………………

**PROF. IRIBE MWANGI**

(Msimamizi)

## TABARUKU

Kwenu nyinyi wazazi wangu wapendwa: Mamangu Siriberia Wanja na babangu Justus Nyagah. Mlinilea, mkajinyima ili kunisomesha, mkanielekeza na kunipa mizungu ya kukabili changamoto za maisha.

Kwenu nyie ndugu zangu wapendwa, na wote wanaonitazama kama kielelezo bora. Kumbukeni, "Adui  wako mkubwa yuko ndani yako."

## SHUKRANI

Mtu bila Mungu na watu si mtu. Singeikamilisha safari ya kuandaa kazi hii bila hawa wawili. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kunipa nguvu za kukabiliana na vizingiti mbalimbali wakati wa kutafitia mada hii. Hamu na ilhamu aliyonipa Mungu ilinitia mshawasha wa kuisukuma mbele kazi hii.

Pili, nawatolea shukrani za dhati wasimamizi wangu, Profesa John Habwe na Profesa Iribe Mwangi kwa msaada wenu wa kupigiwa mfano. Mliniongoza kutoka mwanzo hadi mwisho. Pale nilielekea kupoteza mwelekeo mlinirekebisha. Mchango wenu nauthamini daima. Siwezi kusahau kujitolea hasa nilipokuwa katika safari ya kimasomo kule Ujerumani. Nilipowaomba msaada kupitia barua meme mlinijibu bila kuchoka. Mlinivumilia na kunihimiza nilitie bidii ili kuikamilisha kazi hii kwa muda. Mmenifunza mengi sio tu katika utafiti huu bali pia katika maisha kwa ujumla. Mungu awape mbawazi njema.

Aidha, nawashukuru sana wahadhiri wote wa Chuo Kikuu cha Nairobi na wale wa Chuo Kikuu cha Humboldt cha Berlin kwa mafunzo, ushauri na maelekezo niliyoyapata kutoka kwao. Mlinitia ukakamavu maishani na kuuathiri mwonoulimwengu wangu wa maisha kwa namna chanya. Wahadhiri hawa ni pamoja na: Profesa Peter Wasamba, Profesa Rayya Timammy, Prof. Kithaka, Prof. Wamitila, Prof. Abdulaziz, Prof. Mbatiah, Dkt. Zaja, Dkt. Buregeya, Dkt. Mukhwana, Dkt. Swaleh, Dkt. Mwaliwa, Dkt. Mbuthia na Bi. Ndung'u. Pia, nawashukuru Prof. Guldemann, Dkt. Christfried, Dkt. Klaus, Dkt.Lutz miongoni mwa wengine. Mchango nilioupata baada ya kuwasilisha baadhi ya vipengele vya kazi hii seminani Berlin ulinisaidia sana kufanikisha utafiti huu. Shukrani jazila.

Mwisho nashukuru Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kufadhili utafiti huu na pia kugharamia safari yangu ya Ujerumani. Namshukuru mwanafunzi mwenzangu, Gladys Kaindi niliyesoma naye. Ulinitia nguvu wakati nilihisi kulemewa. Ijapokuwa tulikuwa wawili darasani, ushauri na ushajihishaji wako naukumba. Pia, namshukuru Sylvanus (Namibia) kwa makala kadha aliyonitumia, Gediel kwa kunisaidia kukusanya data. Nawashukuru wote waliochangia ufanisi huu japo sijawataja kwa majina. Mungu awabariki.

**IKSIRI**

Utafiti huu unalenga kuchanganua na kubainisha makosa ya kifonolojia na kimofolojia yanayojitokeza katika kazi andishi za wanafunzi wa shule za upili za Tigania jimboni Meru. Ili kufanikisha lengo hili, data ilikusanywa kutoka shule mbili za mseto na kuchanganuliwa kwa kuongozwa na nadharia ya Lugha-Kati ya Selinker (1972). Uchunguzi huu ulinuia kujaribisha nadharia tete zifuatazo: a) Kazi zilizoandikwa na wanafunzi wa kidato cha pili huwa na makosa mbalimbali ya kifonolojia na kimofolojia. b) Uhawilishaji wa lugha ya kwanza hadi lugha ya pili ndicho kiini kikuu cha makosa ya kifonolojia na kimofolojia. c) Makosa mengi hujitokeza katika kategoria ya vitenzi kuliko kategoria nyingine na d) Zaidi ya asilimia 50% ya makosa itadhihirika katika kazi za wanafunzi wa kiume ikilinganishwa na wenzao wa kike. Matokeo ya uchunguzi huu yalidhihirisha kwamba aina mbalimbali za makosa hujitokeza kwenye insha za wanafunzi. Baadhi ya makosa haya ni pamoja na yale ya unazalishaji wa fonimu, udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa irabu na utumiaji wa sauti mbadala. Pia kuna makosa yaliyotokana na uambishaji na unyambuaji pamoja na mlandano wa kiumbo. Chanzo kikuu cha makosa haya kilibainishwa kuwa athari ya lugha ya kwanza kwa kujizolea frikwezi ya asilia 60%. Vyanzo vingine yaani: ujumlishaji mno, mikakati ya mawasiliano, mikakati ya kujifunza L2 na uhawilishaji wa ufundishwaji viliandikisha asilimia 40% iliyosalia. Aidha, kategoria ya vitenzi iliandikisha frikwenzi ya juu zaidi ya 309 kwa 613 ya jumla ya makosa ambayo ni sawa na asilimia 50.41%. Vilevile, jinsia ya kiume iliandikisha asilimia 53.67% ya makosa nayo ile ya kike ikaandikisha asilimia 46.33%. Isitoshe, mikakati na mbinu anuai zinazoweza kutumiwa kukabili makosa haya zimependekezwa.

## YALIYOMO

UNGAMO ..... ii
TABARUKU ..... iii
SHUKRANI ..... iv
IKSIRI ..... v
YALIYOMO ..... vi
MAELEZO YA DHANA ZILIZOTUMIWA ..... xi
**SURA YA KWANZA ..... 1**
1.1Utangulizi ..... 1
1.2 Tatizo la Utafiti ..... 3
1.3 Madhumuni ya Utafiti ..... 4
1.4 Nadharia Tete ..... 5
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ..... 5
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ..... 7
1.7 Upeo na Mipaka ..... 13
1.8 Msingi wa Kinadharia ..... 13
1.9 Mbinu za Utafiti ..... 22
1.9.1 Mbinu za Kukusanya Data ..... 22
1.9.2 Mbinu za Kuchangangua Data ..... 23
**SURA YA PILI:FONIMU ZA KISWAHILI SANIFU NA KITIGANIA ..... 24**
2.0 Utangulizi ..... 24
2.1 Fonimu za Kiswahili Sanifu ..... 24
2.1.1 Konsonanti za Kiswahili Sanifu ..... 25
2.1.1.1 Vipasuo/ konsonanti za mtuo/vizuiwa ..... 25
2.1.1.2 Vizuiwa-kwamizwa ..... 26
2.1.1.3 Vikwamizwa ..... 26
2.1.1.4 Nazali ..... 27
2.1.1.5 Kitambaza ..... 28
2.1.1.6 Kimadende ..... 28
2.1.2 Fonimu za nusu irabu za Kiswahili Sanifu ..... 29

2.1.3 Fonimu za irabu za Kiswahili Sanifu....30
2.1.3.1 Sehemu ya ulimi....30
2.1.3.2 Mwinuko wa ulimi....30
2.1.3.3 Mkao wa mdomo....30
2.2 Fonimu za Kitigania....32
2.2.1 Konsonanti za Kitigania....32
2.2.1.1 Vizuiwa sighuna....32
2.2.1.2 Vizuiwa nazalishwa....33
2.2.1.3 Vikwamizwa nazalishwa....33
2.2.1.4 Nazali....34
2.2.1.5 Vikwamizwa....34
2.2.1.6 Likwidi....35
2.2.1.6.1 Kimadende....35
2.2.1.6.2 Kitambaza....35
2.2.1.7 Nusu irabu....35
2.2.2 Irabu za Kitigania....36
2.3 Silabi za Kiswahili Sanifu....38
2.3.1 Aina za silabi....40
2.3.2 Miundo ya silabi....40
2.3.2.1 Muundo wa Konsonanti na irabu (KI)....40
2.3.2.2 Muundo wa Konsonanti Konsonanti na Irabu (KKI)....41
2.3.2.3 Muundo wa Konsonanti pekee (K)....41
2.3.2.4 Muundo wa irabu pekee (I)....42
2.3.2.5 Muundo wa Konsonanti Glaidi na Irabu (KGI)....42
2.3.2.6 Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Glaidi na irabu (KKGI)....42
2.3.2.7 Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Konsonanti na irabu (KKKI)....43
2.3.2.8 Silabi funge....43
2.4 Silabi za Kitigania....43
2.4.1 Muundo wa Konsonanti na Irabu (KI)....43
2.4.2 Muundo wa Konsonanti,Konsonanti na Irabu (KKI)....44
2.4.3 Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Konsonanti na irabu (KKKI)....44

2.4.4 Muundo wa Irabu pekee (I) ..... 44
2.5 Hitimisho ..... 44
**SURA YA TATU:UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KIFONOLOJIA NA KOMOFOLOJIA..... 47**
3.1 Utangulizi..... 47
3.2 Makosa ya Kifonolojia..... 48
3.2.1 Unazalishaji wa vizuiwa na kizuiwa-kwamizwa ghuna ..... 48
3.2.2Uchopekaji na udondoshaji wa fonimu /h/ ..... 50
3.2.2.1 Uchopekaji wa fonimu /h/..... 50
3.2.2.2 Udondoshaji wa fonimu /h/..... 50
3.2.3 Uchopekaji na udondoshaji wa irabu..... 51
3.2.3.1 Uchopekaji wa irabu /u/..... 52
3.2.3.2 Uchopekaji wa irabu /i/..... 52
3.2.4 Utumiaji wa sauti mbadala ..... 53
3.2.4.1 Matumizi ya fonimu /s/badala ya /z/..... 53
3.2.4.2 Matumizi ya /z/ badala /s/ ama /ʃ/..... 53
3.2.4.3 Matumizi ya /s/ badala /ʃ/ ama /tʃ/..... 54
3.2.4.4 Matumizi ya fonimu /g/ badala ya /ɣ/ ..... 55
3.2.4.5 Kuchanganya matumizi ya sauti /ð/ na /ɵ/..... 55
3.2.4.6 Matumizi ya /b/ badala ya /v/ ..... 57
3.2.5 Udondoshaji wa nazali /n/ na /m/ ..... 57
3.2.5.1 Udondoshaji wa nazali /n/..... 57
3.2.5.2 Udondoshaji wa nazali /m/ ..... 58
3.3 Makosa ya Kimofolojia ..... 58
3.4 Hitimisho ..... 64
**SURA YA NNE:UCHANGANUZI WA JINSIA NA KATEGORIA YA MANENO INAYOHUSIKA ..... 65**
4.1Utangulizi..... 65
4.2 Matokeo ya shule ya Kaamu..... 65
4.3 Matokeo ya shule ya Kimachia..... 69
4.4 Hitimisho ..... 71
**SURA YA TANO:MIKAKATI YA KUKABILI MAKOSA ..... 75**

5.1 Utangulizi.......................................................................................................75
5.2 Jinsia na ufundishwaji lugha.......................................................................................75
5.3 Baadhi ya mbinu za kupunguza makosa.......................................................................76
**SURA YA SITA:HITIMISHO .......................................................................................81**
6.1 Utangulizi.......................................................................................................81
6.2 Matokeo ya utafiti.......................................................................................................81
6.3 Mapendekezo.......................................................................................................83
**MAREJELEO.......................................................................................................84**
KIAMBATISHO I.......................................................................................................88
KIAMBATISHO II.......................................................................................................89
KIAMBATISHO III.......................................................................................................90
KIAMBATISHO IV.......................................................................................................91
KIAMBATISHO V.......................................................................................................92

**ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA**

/ / Mabano ya fonimu

{} Mabano ya mofu

+ Mpaka wa mofu

$ Mpaka wa silabi

→ Inabadilika na kuwa

* Tungo isiyo sahihi

E: Kielezi

G: Glaidi

H: Kihusishi

I: Kihisishi

I Irabu

K Konsonanti

Kaa :Shule ya Kaamu

K.C.S.E: Kenya Certificate of Secondary Education

Kim: Shule ya Kimachia

L1 Lugha ya kwanza

L2 Lugha ya pili

LK: Lugha-kati

Msi: Msichana

Mvu: Mvulana

N: Nomino

T: Kitenzi

U: Kiunganishi

V: Kivumishi

W:Kiwakilishi

**MAELEZO YA DHANA ZILIZOTUMIWA**

Chombo cha Kupata Lugha: Chombo kinachomwezesha mtoto mchanga kupata lugha. (LAD: *Language Acquisition Device)*

Isimu Tumikizi: *Applied Linguistics*

Kipindi cha kuhirika : P*uberty stage*

Kipindi maalum: C*ritical period*

Lahaja Nafsi: *Idiosyncratic dialects*

Lugha ya kwanza (L1): Lugha ambayo mtoto hujifunza mara ya kwanza (*First Language/Native/Mother-tongue language)*

Lugha ya pili (L2): Lugha anayojifunza mtu baada ya kujifunza lugha yake ya Kwanza *(Second language/foreign language)*

Lugha Kati: Lugha inayojitokeza wakati mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili. Lugha hii huwa imekiuka kanuni za lugha lengwa hivi kwamba hujitokeza kama lugha kamili yenye mfumo wake wa kiisimu (*Inter-Language)*

Majukumu ya kisemantiki-*Semantic roles*

Miundo Kadirifu*: Approximative Systems*

Miundo Tuli ya Kisaikolojia: *LPS: Latent Psychological Structures*

Miundo ya Lugha ya anayejifunza lugha: L*earner Language Systems*

Mwendelezo Lugha: *Language Continuum*

Michakato/mifanyiko ya kiisimunafsia : *Psycholinguistic processes*

Mikakati ya kujifunza L2: *Strategies of L2 learning*

Mikakati ya mawasiliano: *Strategies of L2 communication*

Nadharia Mpya ya Lugha-Kati iliyodurusiwa: *Revised Interlanguage Hypothesis*

Uchanganuzi Linganuzi: *Contrastive analysis*

Uchanganuzi Makosa: *Error Analysis*

Uchanganuzi wa makosa: Mbinu ya kupambanua, kuainisha na kufafanua makosa yanayofanywa na mjifunzaji lugha ya pili

Uhawilishaji lugha**:** *Language transfer*

Uhawilishaji wa ufundishwaji: *Transfer-of-training*

Ujaribishaji-haipothesia :*Hypothesis-testing*

Usimbaji lugha-*Language encoding*

Ujumlishaji mno: *Overgeneralisation*

Uundaji sheria: *Rule formation*

Uyabisi: *Fossilisation*

Vichocheo vya kisensa-*Sensory reinforcements*

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu unalenga kuchanganua na kubainisha makosa yanayojitokeza katika kazi andishi za wanafunzi wa shule za upili za Tigania katika kaunti ya Meru. Wanafunzi hawa ni wale wanaojifunza Kiswahili huku lugha yao ya kwanza ikiwa Gitigania/Kitigania, lahaja ya Kimeru. Tangu miaka ya hamsini hasa baada ya vita vya pili vya dunia, tafiti nyingi kuhusiana na namna binadamu anavyojifunza lugha ya pili zimekwisha kufanywa kwa kujikita kwenye lugha za kigeni (Weinreich 1953, Haugen 1956, Charles Carpenter Fries 1945, na Lado 1957). Maoni tofauti kuhusiana na kujifunza huku kumepelekea kubuniwa kwa nadharia tofauti tofauti za kujifunza lugha kutoka ile ya Uchanganuzi Linganuzi hadi ya Uchanganuzi Makosa mpaka Lugha-Kati. Tafiti hizo zimeonyesha mchango wa makosa katika kujifunza kwa lugha ya pili na hata chanzo cha makosa hayo. Lengo la tafiti hizo limekuwa kutambua na kubainisha makosa haya kwa minajili ya kupendekeza mikakati mwafaka ya kuwasaidia wajifunzaji lugha lengwa kuipata ipasavyo kando na kuuelewa utaratibu wa kujifunza na kuipata L2. Hata hivyo ni tafiti chache ambazo zimechunguza hali hii kwa kujifunga na wajifunzaji wa L2 (Kiswahil) ambao lugha yao ya kwanza ni Kimeru.

Kuanzia miaka ya 1993-2015, watafiti wengi wamekuwa wakichunguza makosa wakijikita kwenye lugha za kwanza (lugha za kiasili/kienyeji) ambazo sio Kimeru katika ujifunzaji wa lugha ya pili (Kiswahili). Haja ya kutafitia lugha ya Kiswahili inatokana na ukweli kuwa ni muhali kupuuza umuhimu wa lugha hii sio tu nchini Kenya bali pia katika jamii ya kimataifa. Lugha ya Kiswahili imekua, ikaenea na ikapanua mawanda yake ya kimatumizi tangu ipangwe na kusanifishwa. Kwa sasa, kwa mujibu wa katiba ya Kenya (2010), lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi ya kwanza ikifuatwa na Kiingereza kama lugha rasmi ya pili bila kusahau kuwa katika katiba hii hii, Kiswahili ni lugha ya taifa. Hii ina maana kwamba, lugha ya Kiswahili imepanda kihali, kihadhi na kuwa na majukumu mengi zaidi. Kama lugha rasmi, lugha ya Kiswahili inatumika kufanikisha shughuli katika mawanda rasmi kama vile ofisi za serikali, bungeni, mahakamani, kutolea elimu katika taasisi za elimu, sayansi na teknolojia, kongamano na warsha, na vikao vingine rasmi. Kama lugha ya taifa, lugha ya Kiswahili imepewa jukumu la

kuwaunganisha watu wa tamaduni tofauti, kuwa chombo cha mawasiliano baina ya Wakenya wenye lugha mbalimbali kando na kutumika kama njia ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Wakenya. Kwa hakika, lugha hii haijapandishwa ngazi tu nchini Kenya, Kiswahili kinatumika kama Lingua Franka katika ukanda wa Afrika Mashariki na Afrika ya Kati kama lugha ya biashara na lugha ya kimawasiliano baina ya wenyeji wa mataifa haya yenye lugha tofauti. Kwa mujibu wa Habwe (2009), biashara ya jinsi hii ambayo inaendeshwa kwa lugha ya Kiswahili ndiyo imeimarisha umoja wa mataifa ya Afrika Mashariki na Kati licha ya kuwa na makabila tofauti tofauti. Kwa mfano, Kiswahili kimeweza kuwafungamanisha Wakenya, Waganda, Watanzania na majirani wao kama watu wa kanda moja na hili limepunguza mizozo baina ya mataifa haya kwani utumiaji wa lugha hii moja ya Kiswahili huwatambulisha kama jamii moja. Nchini Burundi, Kiswahili ni lugha rasmi ya nne. Hadhi kubwa nyingine iliyopewa Kiswahili ni ile ya kutambulikana kama mojawapo ya lugha za Muungano wa Afrika (AU). Hali kadhalika lugha ya Kiswahili imepewa nafasi kubwa katika asasi na taasisi mbalimbali za kimataifa kama vile kufunzwa katika vyuo vikuu mashuhuri ulimwenguni hususan Marekani na Ujerumani kando na kutumika katika vyombo mbalimbali vya habari kote ulimwenguni. Kulingana na Wa 'Njogu (2008) zaidi ya vyuo hamsini Marekani vinafunza Kiswahili. Aidha kulingana na Irele (2010) na wenzake Kiswahili kina takriban wazungumzaji milioni150 kote duniani.

Hoja hizi zinathibithisha ukweli kuwa, lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya lugha zinazokua kwa kasi sio tu katika bara la Afrika bali ulimwenguni kote kwa hivyo kuna haja ya kuitafitia lugha hii zaidi ili iweze kufikia viwango vya kimataifa vinavyotarajiwa ili iweze kushindana na lugha nyingine za kimataifa kama Kingereza. Utafiti huu unaweza kufanywa katika ngazi tofauti tofauti mathalani: kiwango cha shule, kata, taarafa, wilaya, kaunti na hata kiwango cha taifa. Matokeo ya utafiti kutoka kwa sampuli ndogo yanaweza kujumlishwa kwa sampuli kubwa mathalani, jamii pana ama matokeo yake yakatumika kulinganisha matokeo ya tafiti za awali au za baadaye.

Ingawa Kiswahili kimepewa hadhi kubwa kama vile ambavyo tumeshaona (Taz. Uk. 1), ushahidi ni kwamba watumiaji wake hasa wale ambao wanaojifunza lugha hii kama lugha ya pili hukabiliwa na matatizo anuwai wanapoitumia iwe ni katika mazungumzo au kwenye maandishi. Matatizo haya yanadhihirika baina ya watu wa makabila na ngazi mbalimbali mathalani:

wanafunzi, wanasiasa, maafisa wa serikali, mawakili, viongozi wa kidini miongoni mwa wengine. Jambo hili linakuwa kikwazo katika ukuaji, uendeleaji na utekelezaji wa majukumu muhimu ambayo yametajwa hapo juu. Utafiti huu utaendeleza mchango huu wa kukikuza na kukiendeleza Kiswahili pamoja na kuendeleza tafiti zilizofanywa kwa kuangazia masuala mapya na yanayohitaji kuangaziwa hasa katika jamii yetu.

Kwa kuwa utafiti huu utashughulikia lugha sanifu ya Kiswahili na lugha ya Kimeru hususan lahaja ya Kitigania ni vizuri kusema machache kuhusu lugha hii. Kimeru ni lugha inayozungumzwa Kaskazini mwa Kenya na watu wanaoitwa Wameru (Amĩrũ, /amero/).Wameru wanapatikana katika mkoa wa Kaskazini ambapo wanakaa katika kaunti ya Meru. Guthrie (1971) aliweza kuainisha lugha za kibantu katika makundi mbalimbali ambapo lugha ya Kimeru iliwekwa katika ukanda wa E kundi la 50, nambari ya E53. Wanaisimu wengi na wanahistoria wana maoni tofauti tofauti kuhusu idadi kamili ya lahaja za Kimeru. Marete (1981) anasema kuwa Kimeru kina jumla ya lahaja tano ambazo ni Kiimenti, Gitigania, Gichuka, Kimwimbi na Kitharaka. Nkubitu (1993) anatambua lahaja nne (Kiigembe, Gitigania, Kiimenti, na Kimwimbi. Gakii (2006) akimnukuu Gacunku (2005) anatambua lahaja nane: Kiimenti, Gitigania, Gichuka, Kimuthambi, Kimwimbi, Kiigoji, Kiigembe na Kimiutine. Mberia (1981:5) anapinga kwamba Kitharaka sio lahaja ya Kimeru bali lugha tofauti. Sinuii kuingia kwenye mjadala huu kwa sasa. Jambo muhimu hapa ni kwamba lahaja ya Gitigania/Kitigania (ambayo ndiyo inayochunguzwa na utafiti huu) imetambuliwa na watafiti wote hawa.

Tafiti zilizofanywa awali zimebainisha kuwa Kimeru ni lugha ya kibantu (Möhlig 1980:14). Lugha hii kama lugha za kibantu ni lugha ambishi bainishi kwa maana kuwa mizizi ya maneno yake huambishwa viambishi mbalimbali ili kutoa maana inayokusudiwa. Hivyo basi, mfanano mkubwa baina ya lugha hizi mbili unatarajiwa kuwapo. Mfanano wa kisauti utajadiliwa nitakaposhughulikia mfumo wa kifonolojia baadaye.

**1.2 Tatizo la Utafiti**

Tafiti zilizofanywa awali zimedhihirisha kuwa wanafunzi wanaozungungumza lugha ya Kitigania kama lugha yao ya kwanza hukabiliwa na changamoto nyingi wanapojifunza lugha ya pili. Kwa mfano, Josphat Maore (2013) alifanya uchunguzi kuhusu makosa ya tahajia

yanayofanywa na wanafunzi Wameru wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya pili. Maore, aligundua kwamba, makosa mengi ya hijai yalitokana na athari ya lugha ya kwanza; Kimeru. Alihitimisha kwamba, wanafunzi Wameru walitegemea mfumo wa fonolojia ya Kimeru kuandika insha zao. Makosa haya yalitokana na hali kwamba, maneno mengi katika Kimeru huandikwa namna yanavyotamkwa jambo ambalo ni tofauti katika lugha ya Kingereza.

Kutokana na utafiti wa Maore, kuna pengo la utafiti linalofaa kuzibwa. Maore aliangazia lugha ya Kiingereza pamoja na Kimeru kwa ujumla ilhali utafiti huu utashughulikia lahaja ya Kitigania na lugha ya Kiswahili. Aidha, Maore alichunguza makosa ya kifonolojia, utafiti huu utashughulikia makosa ya kifonolojia na kimofolojia. Hali kadhalika, kategoria ya maneno na jinsia inayodhihirisha makosa mengi itaangaziwa jambo ambalo utafiti wa Maore haukushughulikia. Hivyo basi, utafiti huu unalenga kujibu maswali yafuatayo: Ni matatizo gani ambayo huwakumba wanafunzi Watigania wanapojifunza lugha ya Kiswahili sanifu kama lugha ya pili? Matatizo haya husababishwa na nini? Ni jinsia gani huathiriwa zaidi na matatizo haya na ni kwa nini? Je, makosa haya hujitokeza kwa kiasi gani? Kuna uwezekano wa kuchanganua masuala haya kwa kutumia nadharia ya Lugha-Kati? Je, ipo mikakati au mbinu zinazoweza kutumiwa kuyakabili matatizo haya?

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu unanuia kutekeleza madhumuni yafuatayo:

1. Kutambua aina ya makosa ya kifonolojia na kimofolojia yanayodhihirika kwenye insha za wanafunzi wa kidato cha pili wanaojifunza Kiswahili Sanifu kama L2.
2. Kueleza chanzo cha makosa ya kifonolojia na kimofolojia yanayofanywa na wanafunzi.
3. Kubainisha kategoria ya maneno ambamo makosa ya kifonolojia na kimofolojia hudhihirika zaidi.
4. Kutambua jinsia inayodhihirisha zaidi makosa ya kifonolojia na kimofolojia
5. Kupendekeza mikakati inayoweza kutumiwa kupunguza makosa haya.

## 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu utaelekezwa kuthibitisha nadharia tete zifuatazo:

1. Kazi zilizoandikwa na wanafunzi wa kidato cha pili wa shule ya Kaamu na Kimachia huwa na makosa mbalimbali ya kifonolojia na kimofolojia.
2. Uhawilishaji wa lugha ya kwanza hadi lugha ya pili ndicho kiini kikuu cha makosa ya kifonolojia na kimofolojia.
3. Makosa mengi hujitokeza katika kategoria ya vitenzi kuliko kategoria nyingine.
4. Zaidi ya asilimia 50% ya makosa itadhihirika katika kazi za wanafunzi wa kiume ikilinganishwa na wenzao wa kike.
5. Makosa ya kifonolojia na kimofolojia yanaweza kukabiliwa kwa kutumia mikakati mbalimbali.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Kimsingi utafiti huu utaweza kujaza pengo la kiakedemia lililoachwa na tafiti za awali pamoja na kuendeleza mijadala katika nyanja za kiusomi. Nyingi za gunduzi ambazo zimewahi kufanywa duniani ni zao la tafiti zilizofanywa na mijadala iliyoambatana nazo. Kando na hayo, uchunguzi katika mada hii utakuwa na umuhimu mkubwa sio tu kwa watu binafsi bali pia kwa jamii pana. Hutawafaidi wanafunzi, walimu, wakuza mitaala, waandishi, watafiti na hata lugha yenyewe. Matokeo ya utafiti huu kwanza yatawafaa walimu. Utawasaidia kufahamu sehemu za lugha ambazo huwatatiza wanafunzi hivyo kuzitilia mkazo zaidi. Pia, watanufaika na mikakati ya kukabili makosa haya ambayo itapendekezwa na utafiti huu. Aidha, kuna mitazamo hasi miongoni mwa wanajamii kuwa mwanafunzi anapofanya makosa katika mazungumzo au katika uandishi wake hiyo ni ishara ya udhaifu na ushinde maishani. Matokeo ya utafiti huu yatachangia katika kurekebisha mitazamo ya jinsi hiyo kwa kuyafungamanisha na maoni ya wataalam mbalimbali kama vile Corder (1967). Mtaalam huyu anashauri kwamba makosa yanayojitokeza mtu anapojifunza L1 na L2 ni jambo la kawaida kutokea kabla ya mtumizi lugha kuzoea matumizi kamili ya kanuni za lugha lengwa. Kulingana naye, kufanya makosa ni jambo la kawaida. Kwa hivyo, mwanafunzi anapofanya makosa asiadhibiwe bali makosa hayo yachukuliwe kama kigezo cha kuthibitisha kwamba bado mwanafunzi husika hajafikia umilisi wa lugha lengwa. Utafiti huu vilevile, utawapa changamoto walimu wenye msimamo wa namna hii kuzua mbinu mbadala za kuwaauni wanafunzi. Aidha, kwa kuwa mojawapo wa madhumuni

ya utafiti huu ni kubainisha kategoria ya neno ambamo makosa haya hujitokeza zaidi, waandishi wa vitabu wanaweza kupata dira kuhusiana na sehemu ambazo wanafaa kusisitiza zaidi hususan katika sehemu za sarufi, kusoma na kuzungumza. Pia, watafaidika na aina ya makosa na chanzo chake.

Kumekuwapo na madai kuwa wanafunzi hawafanyi vizuri kwenye somo la Kiswahili katika mitihani ya kitaifa ya K.C.P.E na K.C.S.E. Kwa mfano, aliyekuwa Waziri wa Elimu, Sam Ongeri alidai kwamba Sheng' ndiyo iliyochangia kudorora kwa matokeo ya Kiswahili ya K.C.P.E (makala katika gazeti la Standard, Desemba 29, 2011). Naye Kimaro H, (makala katika gazeti la Nation, Machi 21, 2013) Alilalama kuwa matokeo ya Kiswahili yalikuwa ya chini mno. Sababu alizotoa zilikuwa pamoja na: utopa katika silabasi ya Kiswahili, upungufu wa walimu, Kiswahili kutengewa muda mchache ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza miongoni mwa sababu nyigine. Tunahisi kwamba kuna sababu nyingine za kiisimu na zisizo za kiisimu kando na hizo ambazo zinachangia hali hii. Matokeo ya utafiti huu yatatoa mwanga hasa kuhusiana na suala hili. Ingawa sampuli inatoka katika eneo ndogo la Meru (eneo bunge la Tigania Magharibi), matokeo yake yanaweza kujumlishwa katika jamii nzima. Pia, hoja hii inaonyesha kuwa, utafiti huu unaweza kuchochea watafiti mbalimbali kufanya tafiti anuwai katika maeneo mbalimbali ili kuthibitisha na kulinganisha matokeo ya uchunguzi huu. Kando na hayo, kwa kuwa utafiti huu utakuwa kama mwongozo kwa walimu kuwaelekeza wanafunzi, matokeo ya wanafunzi yataimarika maadam somo la Kiswahili huchangia gredi anayotuzwa mwanafunzi katika mtihani wa K.C.S.E.

Isitoshe, lugha ya Kiswahili imepewa hadhi kubwa nchini na hata nje ya nchi. Kama tulivyoonyesha hapo juu, Kiswahili kinatarajiwa kutekeleza majukumu ya lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya, Tanzania na Burundi pia. Aidha, ni lugha inayochangamkiwa na jamii ya kimataifa kutokana na umuhimu wake. Kwa mantiki hii basi, lugha hii inatarajiwa kufikia viwango vya juu ili kudumisha hali na hadhi yake. Ni Sharti lugha hii itumiwe kwa mujibu wa kanuni zake kuanzia viwango vya chini vya elimu hadi viwango vya juu. Lugha haiwezi kukua ikiwa haifanyiwi utafiti kabambe kubaini vikwazo vinavyotatiza ukuaji na uendeleaji wake. Vilevile, ni lazima itumiwe kwa ufasaha na wenyeji wake kwanza ili wageni wanaojifunza na kuitafitia kwa kiwango kikubwa ulimwenguni wapate kuwaiga. Matokeo ya utafiti huu yataweka

wazi sehemu zinazowawia ugumu wazungumzaji na zinazofaa kupigwa msasa kwa manufaa ya kuhifadhi na kudumisha nafasi adhimu ya Kiswahili.

Pia, kwa kuwa utafiti huu unajaribu kuchunguza jinsia inayodhihirisha makosa kwa kiwango kikubwa kuliko jinsia yenzake, ni matumaini yetu kuwa matokeo yake yatachangia mjadala na tafiti ambazo zimeweza kufanywa kuhusiana na jinsia na ujifunzaji lugha. Utafiti huu utatoa mapendekezo ya namna suala hili la jinsia linavyofaa kushughulikiwa ili kutimiza malengo na shabaha ya Maazimio ya Milenia ya Septemba 2000 ya Umoja wa Mataifa yakiwa ni pamoja na kuondoa utousawa wa kijinsia katika elimu ya msingi na sekondari katika mwaka wa 2005 na katika viwango vyote vya kielimu katika mwaka wa 2015.

**1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Tafiti nyingi zimefanywa kuonyesha namna ambavyo binadamu hujifunza L2. Baadhi ya tafiti hizi zimefanywa kulinganisha L1 na L2 ili kudhihirisha athari ya L1 kwenye L2. Tafiti hizi zinahusisha L2 nyingine kando na Kiswahili na Kiingereza. Aidha, kuna kunazo tafiti ambazo zinahusisha lugha za kiasili/makabila mbalimbali nchini Kenya na lugha ya Kiswahili. Tafiti hizi zina mchango mkubwa kwa utafiti huu kwani baadhi ya malengo ya tafiti hizo ndiyo yanayoshughulikwa na utafiti huu walakini kwa namna iliyo tofauti na pia kwa kutumia nadharia tofauti, sampuli, viwago vya kiisimu, eneo la kijiografia, lugha na kiwango cha kielimu ili kuchangia yaliyokwisha kusemwa. Vilevie, kuna mianya ya kiakademia iliyoachwa wazi na tafiti za awali ambayo utafiti huu utajaribu kuziba. Tutaangazia tu yale yaliyoandikwa na ambayo yanahusiana na malengo ya utafiti huu.

Kumekuwa na mjadala mrefu kuhusiana na athari ya L1 katika L2. Kwa kuwa wazo hili ni mojawapo ya malengo ya utafiti huu inafaa kuliangazia. Albert na wenzake (1978), akinukuliwa na Baljit (1999:23) anaeleza kuwa, watu hudhihirisha athari za kileksia zaidi katika faridi zinazofanana. Kwa hivyo, lugha ambazo huwa na miundo inayoshabihiana huweza kudhihirisha viwango vikubwa vya mwathiriano kuliko lugha ambazo zina miundo tofauti. Wazo hili linakinzana na lile la washikilishi wa Uchanganuzi Linganuzi kama vile, Lado 1957, Brown (1980), Fries (1945), Powell 1998, Cook (1969, 1971) na Ervin-Trip (1974). Waandishi hawa

hawa wanaona kuwa miundo na mifumo inayofanana baina ya L1 na L2 huwa rahisi kujifunza ilhali miundo iliyo tofauti huwa muhali kujifunza. Hii ndiyo sababu lengo lao lilikuwa kulinganisha miundo ya lugha L1 na L2 kwani walishikilia kwamba, kwa kuifahamu miundo hiyo ingekuwa rahisi kubashiri sehemu fulani ambazo zingemtatiza mjifunzaji lugha. Kwao L1 ndiyo iliyokuwa chanzo pekee cha makosa yaliyodhihirika katika L2. Wazo la athari za L1 kwa L2 halielekei kupingwa na watafiti. Kwa mfano, Corder (1967,1981), anaeleza kwamba watu wanapojifunza lugha ya pili (L2) huwa wanayo lugha ya kwanza (L1), nao hutumia kanuni wanazozielewa katika L1 katika upataji au ujifunzaji wa L2, kisha huhamisha muundo wa L1 kwa L2. Kwa hivyo, mazoea ya wanafunzi kutumia kanuni za L1 katika L2 hutawaliwa na kaida za L1. Maoni haya ya Corder yanawiana na matokeo ya utafiti wa Halliday (1964). Nadharia hii ingawa iliwekea nadhari zilizo fuata msingi yaani Uchanganuzi Makosa na Lugha-Kati, ilikuja kuonwa ikisheheni udhaifu mkubwa. Matokea ya utafiti wetu utachangia mjadala huu unaoletwa na mkinzano unaoonekana baina ya wasomi hawa kwa kuwa kunayo baadhi miundo ya lugha ya Kimeru inayotofautiana na na ile ya Kiswahili na mingine kufanana ikitiliwa maanani kuwa hizi ni lugha za kibantu.

Utafiti wa Hamdan (1984) unaupa mtazamo unadai kuwa makosa katika L2 hayasababiswhi tu na L1. Hamdan, alichunguza makosa ya kileksia yaliyofanywa na wanafunzi wa Jordan wa Chuo cha umma katika matumizi ya msamiati wa kimsingi wa Kiingereza. Uchanganuzi wake wa data ulionyesha kuwa asilimia 63.85% ya majibu ya sampuli yake yalikuwa na makosa. Aina kuu ya kosa lililodhihirika lilikuwa lile la kutumia leksia mbadala. Aidha, Asilimia 48.2% ya jumla ya makosa yote yalisababishwa na L1.

Utafiti ambao uko mbali kiasi na lugha ambazo tutashughulikia ni ule uliofanywa na He Dan (2010), mtafiti huyu alichanganua makosa yanayofanywa na wanafunzi wa Kichina katika chuo kikuu cha Huizho, wakiwa lugha yao ya kwanza ni Kichina na Kiingereza kama L2. He Dan alitumia Nadharia ya Mwingiliano Lugha ambapo alizingatia makosa yanayotokana na uhamishaji wa Kichina kwa Kiingereza. Kama utafiti wetu, He Dan alikusanya data kupitia insha za wanafunzi ingawa sampuli yetu ni wanafunzi wa shule ya upili. Utafiti wake, ulikitwa China ilhali wetu utakitwa Kenya. L1 na L2 yake ni tofauti na lugha zinazotafitiwa katika utafiti huu. Hata nadharia zinatofautia; yake ni Nadharia ya Mwingiliano Lugha; yetu ni Nadharia ya Lugha-

Kati. Matokeo ya utafiti wake yanaweza kulinganishwa na yetu kwani tafiti zote zinahusu kutafiti makosa katika L2. Wazo la L1 kuathiri L2 pia litatiwa kwenye mizani ingawa hii sio mojawapo ya nadharia tete za utafiti huu.

Hali hii ya L1 kuathiri L2 imethibitishwa na tafiti zilizofanywa kwa kuangazia lugha za kiasili mbalimbali nchini Kenya kama L1 nayo L2 ikiwa Kiswahili na hata kwigineko ikiwa Kiingereza. Mathalani, Chepkwony (1993) alichunguza makosa yanayofanywa na baadhi Wanandi katika matumizi ya Kiswahili. Chepkwony, alitumia sampuli ya Wanandi ambao hawakusoma Kiswahili shuleni. Aliangazia viwango vya kifonolojia, kimofolojia na sintaksia kwa kuongozwa na nadharia ya umuundo. Matokeo ya uchunguzi wake yalidhihirisha kwamba, makosa mengi yalitokana na tofauti za kimuundo baina ya Kinandi na Kiswahili. Maoni haya yanaakisi yale ya wataalam kama Lado (1957). Utafiti huu utatufaa kwa jinsi ya kudhibiti data hasa katika viwango vya kifonolojia na kimofolojia ijapo ametumia L1, nadharia na sampuli tofauti. Vilevile, utafiti wetu unatofautiana na wake maadam Chepkwony, hakuhusisha jinsia wala kategoria ya neno inayodhihisha viwango zaidi vya makosa katika utafiti wake.

Macharia (2013), alifanya utafiti kuchunguza athari za fonolojia ya lugha ya Kikikuyu (L1) katika uandikaji/othografia ya Kiingereza (L2). Sampuli yake ilikuwa wanafunzi wa shule nne za upili (Kikuyu Township, Stonebic, shule ya wasichana ya Riara Springs na Elizabeth Academy). Akiongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa, alisahihisha insha 285 na kubainisha kuwa maneno 424 hayakuendelezwa ipasavyo. Makosa hayo aliyahusisha na athari ya fonolojia ya L1. Utafiti wa Macharia unakurubiana na ule wa Ng'ang'a (2002), aliyetafiti juu ya makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa darasa la saba na jinsi yanavyoshughulikiwa na walimu katika tarafa ya Ndaragwa. Alichunguza makosa ya kisintaksia, kisemantiki, kimofolojia na makosa ya hijai. Lugha za kutafitiwa zilikuwa Kikuyu kama (L1) na Kiingereza kama L2. Kama Macharia, Ng'ang'a aligundua kwamba , lugha ya Kiingereza (L2), iliathiriwa na lugha ya Kikikuyu kwani makosa mengi yaliyobainishwa yalisababishwa na L1. Tafiti za Macharia na Ng'anga zitanufaisha utafiti huu kwa kuwa zimeshughulikia kiwango cha fonolojia ambacho pia kinaangaziwa na utafiti huu pamoja na matumizi ya kazi zilizoandikwa (insha) kama nyenzo ya kukusanya data huku utafiti wa Ng'anga ukiangazia kipenge cha kimofolojia ambacho pia tunakishughulikia. Hata hivyo, tafiti zao zinatofautiana na huu kwani sampuli zao ni

wazungumzaji wa lugha ya Kikuyu wanaojifunza Kiingereza kama L2, ilhali utafiti huu unachunguza makosa yanayotatiza Lugha-Kati ya wanafunzi Wameru kufikia umilisi wa Kiswahili sanifu. Isitoshe, sampuli ya Ng’ang’a ilikuwa ya wanafunzi wa darasa la saba ilhali sampuli yetu ni ya wale wa kidato cha pili. Hata misingi ya nadharia ni tofauti.

Utafiti wa Mudhune (1994) ulidhihirisha kuwa lugha ya Kijaluo ambayo sio lugha ya kibantu iliathiri lugha ya Kiswahili. Mudhune, alichunguza matatizo ya kimofosintaksia yaliyowakumba wanafunzi wa jamii ya Wajaluo katika kujifunza lugha ya Kiswahili (L2). Matatizo yalibainishwa kutokana na insha za lugha ya Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa darasa la nane. Mudhune alichanganua data kwa kutumia Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi. Katika utafiti wake, Mudhune aligundua ya kwamba,lugha ya Kiswahili katika insha za wanafunzi iliathiriwa sana na lugha ya kwanza ya wanafunzi (Kijaluo). Utafiti wake Mudhune utanufaisha huu hasa kwa kuwa amezingatia tanzu za kimofolojia na sintaksia ambazo pia zinagusiwa na utafiti huu. Aidha, utaratibu wa kusasahihisha insha ni wa msaada kwetu. Utafiti wa Mudhune unatofautiana na utafiti huu katika L1, nadharia na hata kwenye nadharia tete kwani hakushughulikia kategoria ya neno inayosheheni makosa mengi.

Tafiti ambazo tumezitaja, zilitumia insha kukusanya data. Kwa upande wake, Musa (2008), alitumia mazungumzo ya wanafunzi wa sekondari katika mijadala kwa kuyarekodi. Kama watafiti wa awali, Musa anawaunga mkono kuwa L1 huathiri ujifunzaji wa L2. L1 aliyoitafitia ilikuwa Kigweno nayo lugha L2 ikikiwa Kiswahili. Musa alitumia Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi ikisaidiwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa kushughulikia vipengele vya kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia. Utafiti wa Musa unatofautiana na wetu sio tu katika L1 bali pia katika, mbinu za kukusanya data, nadharia na hata katika nadharia tete kwani utafiti wetu utaonyesha jinsia inayoathiriwa zaidi na makosa. Utafiti wake Musa utakuwa wa msaada kwa utafiti huu kwani utampa mtafiti dira katika kutoa mapendekezo kwa wanafunzi na walimu kuhusiana na mizungu ya kuyapunguza makosa haya. Pia, utafiti wake umeshughulikia kipengele cha mofolojia kama utafiti huu.

Mtafiti ambaye hakushughulikia kundi mahusasi lenye L1 moja ni Rapando (2005). Yeye, alichunguza makosa ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika

uandishi wa insha jijini Nairobi.Wanafunzi walihitajika kuandika insha. Rapando, alitumia nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Katika utafiti wake, aligundua kwamba baadhi ya makosa yalisababishwa na lugha ya kwanza, Kiingereza na Sheng. Aidha, ujumlishaji mno ulidhihirika kama kisababishi kingine cha makosa ya kimofosintaksia. Makosa mengi yalidhihirika katika kirai kitenzi. Utafiti wa Rapando ni wa umuhimu kwetu kwa kuwa utatupa mwanga katika namna ya kuchanganua data yetu na hata namna alivyoafikia hitimisho kuwa L1 na ujumlishaji mno huchangia makosa kwa L2. Hata hivyo utafiti wake na wetu una tofauti kubwa kwani utafiti wetu umelenga kundi mahususi: Wameru. Isitoshe, nadharia yake na yetu ni tofauti. Pia, Kama alivyofanya Chepkwony na Obara (2014), Rapando, hakuhusisha jinsia katika utafiti wake.

Otiende (2013) alilenga kujadili athari za mofofonolojia za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili kama lugha ya pili. Aligundua kuwa kulikuwa na tofauti kubwa baina ya mifumo ya fonimu za Kiswahili na Kiolusuba ambayo huathiri matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba. Kama Macharia (2013), alithibitisha kuwa kuna baadhi ya fonimu ambazo hutofautiana katika lugha hizo mbili na hivyo kusababisha athari fulani katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Otiende, alitumia mbinu mseto za kukusanya data yaani, insha, imla na kunasa mazungumzo kuku. Kazi ya mtafiti huyu itafaidi utafiti huu japo sampuli yake na yetu ni tofauti kwa kuwa aliangalia wanafunzi ambao L1 ya ni Kiolusuba huku yetu ikiwa ni Kimeru. Aidha, aliongozwa na nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia hasa katika kuchunguza miundo ndani na miundo nje ya maneno na jinsi sauti zinavyobadilika katika harakati za kutamka maneno katika lugha hizo mbili ilhali nadharia yetu ni ile ya LK. Aidha, alitumia sampuli ya wanafunzi thelathini wa shule mbili za msingi ilhali sisi tutatumia wanafunzi sitini wa shule za upili. Kama watafiti tuliooangazia hapo juu, Otiende hakuonyesha kategoria ya neno inayodhihirisha makosa haya ambayo ndiyo mojawapo ya malengo ya utafiti huu.

Tofauti na watafiti waliotajwa hapo juu, Kisakwah (2014) alifanya uchanganuzi wa makosa na muundo sentensi kwa kulinganisha muundo wa sentensi sahili za Kiswahili Sanifu na za Kisuba. Aliainisha makosa ya kisintakisia katika kazi za wanafunzi kutoka Kisiwani Mfangano akahakiki makosa yanayojitokeza katika tungo zao na pia kubaini kiwango cha makosa yanayosababishwa na athari ya L1. Alibaini kuwa makosa mengi hujitokeza katika tungo za wanafunzi na pia makosa hujidhihirisha katika vipashio vyote vya lugha, ijapokuwa kwa asilimia tofauti. Nadharia aliyotumiwa ni ile ya Uchanganuzi Linganuzi. Sampuli yake ilikuwa wanafunzi wa darasa la

saba. Utafiti wa Kisakwah utatufaa hususan katika utaratibu wa kukusanya data na kuainisha ingawa ametumia nadharia na L1 tofauti.

Naye Mangwa (2005), alishughulikia athari za Ekegusii katika lugha ya Kiswahili na jinsi athari hizo zinavyochangia matokeo mabaya katika mtihani wa kitaifa wilayani Kisii Kusini katika kiwango cha sekondari. Katika kazi yake, alifanya uchunguzi katika kipengele cha kifonolojia na sarufi. Alitumia Nadharia ya Uchanaganuzi Makosa (N.U.M) na Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi. Mtafiti mwingine aliyefanya utafiti unaokaribiana na huu ni Obara (2014) aliyechanganua makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii. Utafiti wake ulidhihirisha kuwepo kwa athari za L1 kwa matumizi ya Kiswahili kama L2. Baada ya kuainisha fonimu za Kiswahili Sanifu na Ekegusii alionyesha fonimu zinazopatikana katika kila lugha ya utafiti wake na kuonyesha tofauti iliyomo kifonimu ilivyochangia kuwepo kwa makosa mengi ya kifonolojia. Sawa na Mangwa, Obara alitumia Nadharia ya Uchanaganuzi Makosa japo hakuhusisha ile ya Uchanganuzi Linganuzi kama mwenzake. Sampuli ya Obara ilitolewa katika viwango tofauti vya kielimu yaani wanafunzi wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha tatu ambapo utafiti wake ulionyesha kuwepo kwa makosa katika viwango vyote japo makosa hupungua kadiri mwanafunzi anavyoendelea na masomo katika viwango vya juu. Utafiti wa Mangwa na Obara, utafaa utafiti huu hasa kwa kuwa utafiti wetu unashughulikia kipengele cha kifonolojia na sampuli ya sekondari. Hata hivyo, unatofautiana kwa kuwa utafiti wetu tofauti na wa Obare unajikita kwa wanafunzi wa kidato cha pili. Pia, utatumia asilimia kama mbinu ya kuchanganua data kubaini jinsia na kategoria inayobeba kiwango cha makosa. Vilevile, L1 ya utafiti wetu pamoja na nadharia itakayotumika ni tofauti ikilinganishwa na zile za watafiti hawa.

Kutokana na yaliyoandikwa ni dhahiri kuwa lipo pengo la utafiti. Takribani tafiti zote zimeonyesha kuwa L1 huathiri hujifunzaji wa L2. Hili limethibitishwa na makosa yaliyochunguzwa. Pia, baadhi ya watafiti wameonyesha kwamba makosa yanayojitokeza kwenye L2 hayasababishwi tu na L1; kuna visababishi vingine. Katika tafiti hizi, imejitokeza kuwa hamna utafiti uliojaribu kuangazia suala la jinsia. Aidha, hata kategoria inayodhihirisha kiwango kikubwa cha makosa haijabainishwa. Ni Rapando tu aliyejaribu kushughulikia hili japo

aliangazia kipashio cha kisintaksia cha kirai (kirai kitenzi). Hivyo kuna haya ya mapengo haya kujaribu kuzibwa.

## 1.7 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ni aina ya uchunguzi unaoangukia katika uwanja wa Isimu Tumikizi. Kiini chake ni kubainisha makosa ya kifonolojia na kimofolojia katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi wa kidato cha pili katika kaunti ya Meru. Utafiti utajifunga hasa na makosa katika viwango hivi viwili walakini viwango hivyo vingine hasa kile cha semantiki na kisintaksia vitahusishwa pale ambapo ufafanuzi utahitajika kwa kuwa tanzu hizi za isimu huweza kuingiliana, kutegemeana na kukamilishana. Makosa ya uakifishaji hayatashughulikiwa na utafiti huu maadam yako nje ya upeo wa mipaka wa utafiti huu. Makosa yanayotokana na matumizi ya lugha kisajili hayatashughulikiwa kwa kuwa tunachukulia kuwa mwanafunzi aliyafanya makosa haya kimaksudi ili kuwasilisha ujumbe lengwa. Pia, makosa yanayohusu uhawilishaji wa misemo moja kwa moja kutoka L1 hadi L2 yatapuuzwa pamoja na yale yanayotokana na matumizi ya Sheng'. Hali kadhalika, wanafunzi wa vidato vingine hawatahusishwa kwa kuwa hatudhamirii kulinganisha matokeo kiviwango vya elimu. Vilevile, tutajifunga tu na kazi zilizoandikwa wala sio lugha ya mazungumzo. Nadharia itakayotumika ni ile tu ya Lugha-Kati iliyoasisiwa na Selinker (1972) kwa kujikita katika mifanyiko mitano ya kisaikolojia iliyobainishwa.


## 1.8 Msingi wa Kinadharia

Kuna nadharia mbalimbali zinazotumika kuchanganua makosa yanayojitokeza binadamu anapojifunza lugha ya pili. Kuna nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi, Uchanganuzi Makosa na Lugha-Kati. Nadharia ya Lugha-Kati ilibuniwa kutokana na udhaifu uliojitokeza katika nadharia za awali. Utafiti huu utatumia mtazamo wa Lugha-Kati kuchunguza na kubainisha makosa yanayodhihirika katika kazi za wanafunzi kwa kuwa makosa haya ndiyo huwa kikwazo kwa Lugha-Kati kufikia viwango kamili (umilisi) vya lugha lengwa (L2).

Istilahi 'Lugha-Kati' ilibuniwa kwa mara ya kwanza na mwanaisimu wa Kimarekani, Larry Selinker (1972 ) katika makala yake ya semina yaliyochapishwa kwenye jarida la *International Review of Applied Liguistics.* Selinker anaifasiri Lugha-Kati kuwa lugha iliyo na miundo huru na


tofauti ambayo haitegemei lugha ya kwanza wala lugha ya pili/kigeni/lengwa ingawa huunganishwa (linked) na lugha hizo. Ni lugha ambayo anayejifunza lugha hujiundia kama mbinu ya kujifunza lugha lengwa. Istilahi mbalimbali zimebuniwa kutajia Lugha-Kati ingawa kuna tofauti kidogo. Kwa mfano, Nemser (1969) anatumia istilahi, Miundo Kadirifu, Corder (1971) akaiita Lahaja Nafsi nao Richards na Sampson (1973) wakaiita Miundo ya Lugha ya Mjifunzaji lugha. Maelezo haya yote yanadhihirisha jambo moja kuu kwamba, ujifunzaji lugha ya pili hufuata njia inayoelekea katika lugha lengwa, mwanafunzi akijijengea miundo yake ya kifonolojia, kisarufi na matumizi ya sheria za kisemantiki. Kulingana na Richards na wenzake (1996), Lugha-Kati ni aina ya lugha ambayo huweza kutolewa na wanaojifunza lugha ya pili/lugha ya kigeni ambao wamo katika mchakato wa kujifunza lugha mpya. Katika mtazamo ya kiakili, Lugha-Kati huwa muundo wa lugha ulio baina ya lugha asili/lugha ya kwanza na lugha lengwa (Brown, 1994). Lugha hii huakisi juhudi za mjifunzaji za kujenga mfumo wa kiisimu ambao hukua na kubadilika hatua kwa hatua kufikia mfumo wa lugha lengwa (Fauziati, 2011).

Tofauti na Uchanganuzi Linganuzi na Uchanganuzi Makosa, Lugha-Kati haichukuliwi kama mchakato katika ujifunzaji wa L2 inayoathiriwa na lugha ya kwanza au ya pili. Yaani, lugha hii sio mfumo wa lugha ya kwanza ama mfumo wa lugha lengwa bali ni ni mfumo wa kiisimu unaojitegemea. Lugha-Kati hudhihirika pale ambapo wanaojifunza lugha, hueleza maarifa ambayo tayari wanayafahamu kwa lugha mpya ambayo wanajaribu kujifunza. Selinker (1972) anaeleza kuwa Lugha –Kati kama michakato ya katikati (transitional processes) baina ya L1 na L2, hudhihirika kwenye lugha ya mjifunzaji lugha na inaweza kuchunguzwa. Anachukulia Lugha-Kati kama "lahaja ambayo sheria zake huwa na sifa zinazofanana na lahaja mbili za kijamii za lugha hata kama lugha hizi huwa na sifa sawa au la (Selinker, 1972) akinukuliwa katika Corder, (1981:17). Kulingana naye, dhana ya Lugha-Kati inaweza kufafanuliwa kwenye mchoro ufuatao.




Mchoro 1. Dhana ya Lugha-Kati (Kutoka kwa Corder, 1981:17). Katika mchoro huu, Lugha A inawakilisha L1 ya mjifunzaji lugha.


Corder (1981) anasema kuwa lugha ya mjifunzaji lugha inaweza kuchukuliwa kama lahaja kiisimu. Anamaanisha kuwa lugha mbili zinazofanana katika baadhi ya kanuni za sarufi huwa lahaja. Kwa kuzingatia dai hili, anaeleza kuwa kuwa lugha A na lugha B kama zinavyoonyeshwa katika *mchoro 2* ziko katika uhusiano wa kilahaja ambao ndio huelekeza kwenye Lugha-Kati.




**Madai ya nadharia hii**

Kwa mujibu wa Tarone (2001), Nadharia ya Lugha-Kati ilileta mabadiliko makubwa baina ya utazamaji wa ujifunzaji lugha kisaikolojia badala ya kuutazama kitabia.Awali, ujifunzaji lugha ulihusisha mtazamo wa kitabia (*behaviourist approach*) walakini kutokana na nadharia hii mpya masuala ya kisaikolojia au kiakili yalianza kuangaziwa zaidi kupitia mitazamo ya kisaikolojia *(psychological perspectives*) au kiakili *(mentalist approach*) ya kujifunza lugha.

Wakati wa kujifunza lugha ya pili, mjifunzaji lugha huanza kwa kuandaa nadharia tete kuhusiana na sheria za lugha lengwa yake. Sheria hizi zinaweza kuchukuliwa kama sarufi za kiakili (*mental grammars*) ambazo ndizo huunda mfumo wa Lugha-Kati. Sarufi za jinsi hii huweza kuathiriwa (kuvamiwa) na na mambo yaliyo nje ya mjifunzaji lugha au mambo yaliyo ndani yake yaliyozalishwa kutokana na uzalishaji ndani wa mjifunzaji lugha. Kwa sababu hii inaweza kudaiwa kwamba lugha ya mjifunzaji lugha kimatumizi, hubadilikabadilika kiwakati ama kwa kudondosha sheria, au kuongeza sheria na kuunda upya mfumo ulio kamili. Jambo hili linaonyesha nafasi ya Lugha-Kati katika kila awamu ya kujifunza L2. Katika mchakato huu mzima ya kujifunza L2, kunakuwa na hali ya kutathiminitathimini upya nadharia tete kila mara huku mwanafunzi husika akibadilishabadilisha Lugha-Kati yake hadi pale ambapo mfumo wa lugha lengwa unapoafikiwa. Mchakato huu hujulikana kama Mwendelezo wa Lugha-Kati. Mchoro ufuatao unafafanua mchakato huu.




Mchoro 3. Mwendelezo wa Lugha-Kati (Tanvir Shameem, 1992)

Dai kuu la nadharia ya Lugha-Kati ni kuwa wakati ambapo anayejifunza lugha L2/lugha ya kigeni anapojaribu kuwasiliana kwa lugha lengwa, yeye hutumia mfumo mpya wa kiisimu ulio tofauti na lugha ya kwanza na lugha lengwa. Dai hili kama tulivyoonyesha hapo juu linaungwa mkono na Selinker (1974:35) anayeeleza kuwa Lugha-Kati inaweza kuwa "mfumo wa kiisimu unaojitegemea unaotokana na kile ambacho mjifunzaji lugha hulenga kukiwasilisha anapojaribu kulingana na kaida za lugha lengwa". Anaongeza kuwa "Kila wakati mjifunzaji lugha anapojaribu kuunda sentensi, huweza kuichochea/kuiamsha *(activates)* Miundo Tuli ya Kisaikolojia. (Maelezo zaidi kuhusiana na dhana hii yatatolewa katika mwisho wa sehemu hii). Madai mengine yanafafanuliwa na Mitchell na Myles, (1998 na Larsen-Freeman, 2003). Kimuhtasari madai haya ni pamoja na:

1. Ujifunzaji lugha ni mchakato wa kujaribu kufikia kanuni kamili za lugha lengwa (590-591)
2. Ujifunzaji wa L2 ni ukuaji wa kihatua kutoka lugha ya mama (L1) hadi lugha lengwa.
3. Mfumo wa sheria fulani ambao sio ule wa lugha asilia au lugha ya mama ama mfumo wa lugha ya kigeni au lugha lengwa unaweza kuendelezwa na mjifunzaji lugha katika kila awamu ya mchakato wa kujifunza lugha.
4. Mchakato wa kujifunza lugha huhusu ujaribishaji-haipothesia au uundaji sheria
5. Ni jambo la kawaida kwa mjifunzaji lugha kufanya makosa

6. Wajifunzaji lugha wengi hawafikii umilisi wa lugha lengwa.

Katika Miundo Tuli ya Kisaikolojia (LPS) kuna baadhi ya dhana muhimu ambazo ni uyabisi na Michakato/mifanyiko ya kiisimunafsia.

**Uyabisi**

Hali ya uyabisi imevuta hisia mbalimbali miongoni mwa watafiti wa ujifunzaji wa L2 na imeibua maoni anuwai. Uyabisi ni hali ambapo, hufika wakati, Lugha-Kati ikaacha kukua na kuendelea katika mchakato wa kufikia viwango vya lugha lengwa. Uyabisi ni kipengele muhimu cha mchakato wa Lugha-Kati ambacho hujitokeza katika awamu/sehemu fulani katika ukuaji wa Lugha-Kati. Kulingana na Selinker (1974), uyabisi huchukuliwa kuwa mojawapo ya mikakati muhimu zaidi ya Miundo Tuli ya Kisaikolojia. Katika utafiti wa ujifunzaji wa L2 dhana ya uyabisi inahusiana na nadharia ya Lugha-Kati ambayo inaonwa na Selinker (1972) kuwa tukio katika ujifunzaji wa L2. Dhana ya Uyabisi sio tofauti sana na dhana za Tarone (1976), Nemser (1971), na Sridhars' (1980) zote zilihodhi jaribio za kuelezea chanzo cha uyabisi katika Lugha-Kati ya wajifunzaji L2. Maelezo yake yalikuwa, "matukio ya kiisimu yanayoyabishwa ni faridi za kiisimu, sheria na vijifumo ambavyo mjifunzaji lugha fulani ya kwanza ambavyo huweza kubakisha katika Lugha-Kati inayolandana na lugha lengwa, bila kuzingatia umri ama kiwango cha maelekezo atakayopokea mjifunzaji lugha katila lugha lengwa (Selinker, 1972:215). Anaeleza kuwa wazungumzaji wa L2 hawafikii umilisi wa lugha lengwa, kwa kuwa hukwama mahali fulani katikati katika mchakato wa kujifunza lugha yao kwa kuathiriwa na makosa. Anabainisha kuwa uyabisi hutokea katika awamu tofauti katika mchakato wa kujifunza lugha. Kwa mujibu wa (Birdsong, 2004), ni asilimia 5% tu ya wajifunzaji L2 hufikia tamati ya mwendezo wa Lugha-Kati huu kwa ufanisi huku wengine wakishindwa; wanashindwa kukabiliana na uyabisi. Wakati mjifunzaji lugha hushindwa kupiga hatua katika ujifunzaji, lugha-kati yake huyabishwa. Towell and Hawkins (akinukuliwa katika Han 2005:13) anadai kwamba:

> Hata mjifunzaji wa L2 akiendelea kukaa katika mazingira ambamo mjifunzaji lugha atakuwa akitumia L2 kila siku sio jambo lisilo la kawaida kumkuta akiwa na lafudhi ngeni ya kiwango cha juu, akitumia miundo ya kisarufi isiyo ya wazawa lugha hiyo na asiyekuwa na uelewa wa wazawa kuhusiana na ufasiri wa baadhi ya sentensi" uk. 13 (Tafsiri yetu)

**Michakato ya kiisimunafsia**

Kuna mifanyiko ya kisaikolojia kadhaa inayosababisha uyabisi (Selinker 1972:56). Hata hivyo ni muhimu ikumbukwe kuwa mifanyiko hii inakuwa tu njia ya mjifunzaji lugha kuunda mfumo wa Lugha-Kati. Kwa kujikita na kanuni za lugha lengwa, mifanyiko hii itasababisha makosa walakini kwa mujibu wa sarufi za Lugha-Kati mikakati hii haizui makosa yoyote. Mifanyiko hii ni pamoja na:

1. Uhawilishaji lugha-Hapa ni pale ambapo kanuni na mifumo ya Lugha-Kati yaweza kutokana na L1. Wanafunzi hutegemea lugha yao ya kwanza/mama ili kuunda mifumo ya lugha lengwa. Utegemeaji huu hutokea aghalabu katika awamu za mwanzo mwanzo za ujifundishaji L2. Tofauti iliyopo baina ya kujifunza lugha ya kwanza na ya pili ni kuwa ujifunzaji wa lugha ya pili huathirika na lugha ambayo tayari mwanafunzi anaijua. Kuathirika huku ndiko kunaitwa uhamishaji wa lugha. Uhamishaji lugha waweza kutokana na lugha ya kwanza, pili au tatu na hutokea katika viwango tofauti k.v. sarufi, matamshi, msamiati, diskosi, n.k.


2. Uhawilishaji wa ufundishwaji- Hapa, mwanafunzi huhamisha mafundisho yasiyo sahihi kuhusu lugha lengwa kama anavyoyapokea kutoka kwa vitabu vya kianda au mwalimu asiye na uelewa kamili wa kiisimu ambapo huiga anavyozungumza mwalimu wake. Mwanafunzi anaposikia kutoka kwa mwalimu wake matamshi yasiyokubalika au msamiati au akitumia sarufi ya lugha lengwa isivyofaa, naye hufanya makosa yayo hayo bila kujua. Hali hii hutokea aghalabu pale ambapo mwalimu ni mzungumzaji wa lugha ya kwanza na kwa hivyo katika kufundisha yeye pia hufanya makosa. Uhamishaji huu pia unaweza kusababishwa na mbinu mbalimbali za ufundishaji wa L2.

3. Mikakati ya mawasiliano-Hii ni mbinu ambapo baadhi ya elementi za Lugha-Kati hutokana na njia mahususi ambazo watumiaj lugha hujifunza ili kuwasiliana. Mbinu hizi huongozwa na lengo fulani kama vile kukabiliana na upungufu wa LK hivi kwamba mwanafunzi hukosa neno katika Lugha-Kati kuelezea dhana husika. Kwa mfano, mwanafunzi anapokosa neno la kutajia "malaika" (viumbe) huenda akawaita "viumbe wa Mungu wenye mabawa". Au akishindwa kupata neno la kurejelea "jokofu" huenda akaliita "sanduku la baridi". Lengo hapa huwa ni kuwepezesha mawasiliano. Mikakati hii huenda ikawa sehemu ya mfumo wa Lugha-Kati.

4. Mikakati ya kujifunza L2- Hapa wanafunzi husahilisha mifumo ya L2 ili kufikia uamilifu mpana wa kimawasiliano. Mfano wa mkakati huu ni ule wa kutumia dhana zilizozoeleka kukumbuka dhana zisizozoeleka. Dhana zinazofahamika huenda zikachukua nafasi ya dhana ngeni katika LK ijapokuwa hazina uhusiano wa kiisimu. Maadamu mikakati hii ni ya kimaksudi, mjifunzaji lugha huenda akatambua makosa yake na kujaribu kuyarekebisha ikiwa atazingatia mbinu mwafaka za ujifundishaji lugha. Hata hivyo ni wajifunzaji wachache tu ambao huweza kutumia mikakati ya ujifundishaji mwafaka kujiboresha.

5. Ujumlishaji mno- Katika mkakati huu, kanuni za lugha lengwa hujumlishwa.Wanafunzi hutumia kanuni za lugha ya pili namna ambavyo wazawa wa lugha hii hawawezi
kutumia. Ujumlishaji hutokea pale ambapo, mjifunzaji lugha hufahamu vizuri ruwaza fulani katika lugha lengwa kisha akaijumlisha mno ruwaza hiyo katika miktadha mingi ya lugha lengwa. Kwa mfano, mwanafunzi akifahamu kuwa nomino (hasa nomino zalishi) huundwa kutokana na mzizi wa kitenzi kwa kutia irabu {-i} ya unominishaji huenda akajumlisha mbinu hii ya unominishaji kwa mizizi ya vitenzi vile vya mkopo. Kwa mfano, kutokana na kitenzi "roga" tunapata "mrogi". Huenda mwanafunzi akaunda nomino "mdhulumi" kutokana na kitenzi "dhulumu". Watafiti huamini kuwa miundo hii ya lugha hutokana na ujuzi alionao mwanafunzi katika akili yake. Mwanafunzi hujumlisha sifa za lugha pale ambapo sifa za lugha anayoifahamu zinakaribiana na zile za lugha anayojifunza. Hii husababisha ucheleweshaji wa uelewa wa sifa tofauti. Mwanafunzi anaweza kukataa kujifunza kanuni zilizo tofauti na lugha yake ya kwanza (Richards, 1974).

Mifanyiko hii inaelezwa kwenye mchoro 4.




Mchoro 4. Mifanyiko inayosababisha uyabisi (umenukuliwa kutoka kwa Krzeszowski, 1977:77)

Jambo dhahiri ni kuwa mifanyiko hii huleta uyabisi ambao ndicho kikwazo cha kufikia umilisi wa lugha lengwa kwa kuwa wajifunzaji wake aghalabu hukosa Chombo cha Kupata Lugha cha kukabiliana na uyabisi; badala yake huwa na Muundo Tuli wa Kisaikolojia. Dhana hii ya Muundo Tuli wa Kisaikolojia iliibuliwa na Selinker kuchukua nafasi ya Chombo cha Kupata Lugha (*Language Acquisition Device:* LAD). Kuna mwelekeo wa kuihusisha Lugha-Kati na wajifunzaji lugha ambao ni watu ambao wamepita kipindi cha kubaleghe. Hata hivyo, mwelekeo huu umedurusiwa upya kuwahusisha watoto katika nadharia mpya ya Lugha-Kati iliyodurusiwa ingawa kuna mjadala ikiwa watoto hutumia ama LAD au LPS. Kulingana na Chomsky, watoto wanapojifunza lugha huwezeshwa kuipata na Chombo cha Kupata Lugha ambacho kila binadamu huwa nacho. Chombo hiki huacha kufanya kazi binadamu anapokaribia kipindi cha kubaleghe. Chombo hiki vilevile ndicho humsaidia mtoto kujifunza L2 kwa ukamilifu na kufikia umilisi wa wa lugha lengwa kama wazawa wake kwani humwezesha kukabiliana na kikwazo cha uyabisi. Jambo hili la watoto kusaidiwa na Chombo cha Kupata Lugha, ndilo lililopelekea Selinker kudai kuwa mjifunzaji lugha akishahitimu kipindi hiki maalum hutumia Muundo Tuli wa Kisaikolojia kujifunza L2. Sifa kuu na muhimu ya Lugha-Kati inayohusishwa na watu wazima ni kuwa hufika wakati ambapo huacha kukua na kuendelea walakini watoto wanapojifunza lugha yao ya mama hufikia umilisi wake kikamilifu. Hii ina maana kuwa kuna tofauti kuu na muhimu ya kiisimunafsia katika ujifunzaji wa lugha asili ya mtoto na ujifunzaji wa L2. Hivyo lengo kuu katika utafiti wa Lugha-Kati ni kueleza tofauti hii hususan kueleza na

kufafanua kikwazo kikuu cha Lugha-Kati kufikia kiwango cha lugha lengwa. Kwa hivyo, maswali muhimu katika utafititi wa Lugha-Kati ni; ni mifanyiko gani ya kiisimu inayochangia kuendelea na kuvivia kwa Lugha-Kati? Je, tofauti hizi zinawezaje kueleza tukio la uyabisi? Haya ndiyo baadhi ya maswali ambayo utafiti huu utajaribu kujibu kwa kujikita na lugha ambayo itakayotumiwa na wanafunzi wa shule mbili za Tigania, Meru. Tunachukulia kuwa wanafunzi wa kidato cha pili maadam wamehitimu kipindi cha kubaleghe wanatumia LPS badala ya LAD. Pia, lugha ya kwanza/ mama yao ni Kitigania huku Kiswahili Sanifu ikiwa ndio lugha yao lengwa. Hata hivyo kama tulivyoeleza katika sehemu ya Tatizo la Utafiti, Wazungumzaji wengi ambao ni Wameru hutumia Kiswahili ambacho hakiafiki kanuni za Kiswahili Sanifu kumaamisha kuwa wazungumzaji hawa hawajafikia umilisi wa Kiswahili Sanifu au viwango vitatakiwanavyo kutokana na makosa mbalimbali wanayokumbana nayo. Kwa hivyo katika utafiti huu tunachukulia kuwa na lugha tatu. Kwanza, tuna lugha ya kwanza au lugha asili/ lugha ya kuzaliwa au lugha ya mama ambayo ni Kitigania. Pili, tuna lugha lengwa ambayo hapa ni Kiswahili Sanifu kisha tuna Lugha-Kati ambayo hapa ni "Kiswahili kinachoandikwa na wanafunzi Watigania. Mifanyiko ya kisaikolojia iliyotajwa hapo juu inaweza kuchunguzwa kwa kurejelea lugha-kati kwani ni katika lugha hii ambapo uhamishaji wa kanuni za lugha ya kwanza, ujumlishaji mno wa sheria za lugha lengwa, mikakati ya ujifunzaji, mikakati ya mawasiliano na ufunzwaji mbaya udhihirika. Kimsingi, tutajaribu kuchunguza ikiwa mifanyiko hii ndiyo huchangia makosa ya kifonolojia na kimofolojia ambayo ndiyo kiini cha utafiti huu.

### 1.9 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanywa nyanjani na maktabani. Nyanjani, nilitumia insha sitini kutoka shule mbili. Pia, nilisoma kwenye maktaba ili kuangazia yaliyoandikwa kuhusiana na mada ya utafiti huu.

#### 1.9.1 Mbinu za Kukusanya Data

Nilichagua shule mbili za za upili za mseto katika jimbo la Meru, eneo mbunge la Tigania Magharibi. Shule hizi ni Kaamu na Kimachia.Nilichagua shule za mseto maadam utafiti huu unalinganisha jinsia inayodhihirisha viwango vikubwa zaidi vya makosa. Sababu nyingine ya kuchagua shule hizi ni kwamba, ziko katika eneo ambalo wazungumzaji wa lahaja ya Kitigania wamo. Vilevile, sampuli ya wanafunzi wa kidato cha pili ilichaguliwa kwa minajili ya kutathimini wazo la Tanvir S. (1992) la Mwendelezo wa Lugha-Kati, ambalo ni wazo muhimu katika nadharia inayoongoza utafiti huu. Aidha, eneo hili la Tigania ndilo eneo la kuzaliwa la

mtafiti kwa hivyo ujuzi wake wa lahaja hii ni muhimu katika uchanganuzi wa data husika. Pia, nilichagulia shule za kaunti ambazo zimo katika kiwango kimoja ili kuweza kufanya ulinganishaji sawa. Aidha, shule hizi ziliweza kutimiza idadi ya wanafunzi zaidi ya thelathini kwa minajili ya kukidhi matakwa ya uchunguzi huu ya wanafunzi thelathini kutoka kila shule. Ili kupata idadi sawa ya wavulana na wasichana, wanafunzi kutoka kila kidato walitiwa katika makundi mawili kulingana na jinsia yao. Kutoka kila kundi nilichagua wanafunzi kumi na watano kwa kuandika nambari moja hadi kumi na tano kwenye vikaratasi. Vikaratasi vingine havikuandikwa chochote ingawa vilikuwa sehemu ya vile ambavyo wanafunzi waliviookota kisha vikakunjwa na kutiwa kwenye kikapu.Wanafunzi waliookota vijikaratasi vyenye nambari, ndio nilitumia kuandika insha ya kawaida yenye urefu wa maneno yasiyopungua mia nne. Wanafunzi hawa walitakikana kutumia dakika arobaini na tano kama inavyohitajika katika mitihani ya shule na ile ya kitaifa. Isitoshe, wanafunzi walioshiriki katika mchakato huu walifahamishwa kwanza kuhusu lengo la shughuli hii ya uandishi wa insha na pia kuhakikishiwa kwamba majina yao yangebanwa iwapo wangeidhinisha hivyo.

### 1.9.2 Mbinu za Kuchangangua Data

Insha za shule hizi mbili zilisahihishwa huku tukitenga za wavulana na wasichana kutoka kila shule. Kila kosa la kifonolojia na kimofolojia lilipigiwa mstari kulingana na kategoria ya neno husika. Majedwali yalitumika kuanisha makosa haya. Aidha, frikwenzi ya kila kategoria ilibainishwa. Vilevile, jinsia iliyodhihirisha viwango vikubwa vya makosa ilionyeshwa. Hali kadhalika, chanzo cha makosa kilielezwa kulingana na aina ya kosa husika.

## SURA YA PILI

## FONIMU ZA KISWAHILI SANIFU NA KITIGANIA

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, fonimu za Kiswahili Sanifu na za Kitigania zitashughulikiwa. Kwa kufanya hivi tutaweza kuona namna lugha hizi mbili zinavyolandana na kutofautiana katika mifumo yake ya sauti kama lugha za asili moja: Kibantu. Aidha, sehemu hii itawekea sehemu zinazofuata msingi na hata kutoa mwanga kuhusu sababu zinazosababisha kuwepo kwa makosa katika insha za wanafunzi. Vilevile, kwa kuwa silabi ni sehemu inayochunguzwa katika kiwango cha kifonolojia tutaiangazia pia katika sehemu hii hasa ikitiliwa maanani kuwa mojawapo wa makosa yanayolengwa kubainishwa na utafiti huu ni yale ya kifonolojia.

Fonimu ni kipashio cha kimsingi cha lugha kinachoshughulikiwa na tawi la fonolojia. Massamba na wenzake (2004) wanaieleza fonimu kama kipashio kidogo ambacho hudhihirika kama sauti katika lugha mahususi. Wanaongeza ya kwamba uamilifu wa fonimu ni kutofautisha maana ya maneno. Kwa mfano, maneno [ugali] na [ukali] yana fonimu sawa isipokua zile za tatu /g/ na /k/ mtawalia. Fonimu hizo ndizo zinaleta tofauti ya maana. Ikiwa sauti fulani inayopatikana katika neno fulani itaondolewa na badala yake sauti nyingine kutiwa mahali pake, sauti hiyo iliyotiwa ikibadilisha maana ya neno hilo basi sauti husika ni fonimu za lugha hiyo. Kwa mfano sauti /a/ na /i/ katika maneno [chai] na [chui].Tunapoondoa /a/ na kutia sauti /u/ maana inakuwa tofauti. Sauti hizi mbili ni fonimu za Kiswahili.

### 2.1 Fonimu za Kiswahili Sanifu

Wanaisimu mbalimbali wameushughulikia mfumo wa fonimu za Kiswahili. Baadhi yao ni pamoja na: Polome (1967), Mgullu (2001), Habwe na Karanja (2004) na Iribemwangi (2010). Wote wameziainisha fonimu kama:

i. Fonimu za irabu

ii. Fonimu za nusu irabu

iii. Fonimu za konsonanti

### 2.1.1 Konsonanti za Kiswahili Sanifu

Wataalam mbalimbali wanaelekea kukubaliana na vilevile kutofautiana kuhusiana na idadi kamili ya konsonanti za Kiswahili Sanifu. Polome (1967) aliorodhesha konsonanti 24, wameanisha konsonanti 23. Iribemwangi (2010) ameorodhesha konsonanti 25.

Kuna vigezo kadha vinavyotumiwa kuainisha konsonanti za Kiswahili. Hata hivyo vigezo vitatu muhimu vinavyoweza kutumiwa kutofautisha konsonanti hizi ni pamoja na: mahali pa kutamkia, namna/jinsi ya kutamka na hali ya nyuzi za sauti. Konsonanti za Kiswahili Sanifu ziko katika makundi sita makuu kwa kutegemea kigezo cha namna ya kutamka. Makundi hayo ni vipasuo, vizuiwa-kwamizwa, vikwamizwa, nazali, vitambaza na vimadende.

#### 2.1.1.1 Vipasuo/ konsonanti za mtuo/vizuiwa

Sauti hizi zinapotamkwa, ala husika hukutana na kufungia hewa kabisa kisha hewa huachiliwa ghafla baada ya ala hizo kuachana kiasi kwamba sauti hutoka kwa mpasuko au mfyatuko. Kiswahili kina vipasuo sita ambavyo ni: **/p/, /b/,/t/,/d/,/k/** na/**g**/.

Sifa zake bainifu ni kama zifuatavyo:

| /p/ | /b/ | /t/ | /d/ |
|---|---|---|---|
| +kons | +kons | +kons | +kons |
| +kip | +kip | +kip | +kip |
| +midomo | +midomo | +ufizi | +ufizi |
| -nazali | -nazali | -nazali | -nazali |
| -ghuna | +ghuna | -ghuna | +ghuna |

| /k/ | /g/ |
|---|---|
| +kons | +kons |
| +kip | +kip |
| +kaakaa laini | +kaakaa laini |
| -nazali | -nazali |
| -ghuna | +ghuna |

#### 2.1.1.2 Vizuiwa-kwamizwa

Wakati wa kuzitamka sauti hizi, ala sauti husika hukutana na kuzuia hewa kabisa kama ilivyo katika utamkaji wa vizuiwa kisha huachana kidogo na kuacha mwanya mdogo ambapo hewa hupitia huku ikisababisha mkwaruzo kama ilivyo katika utamkaji wa vikwamizwa. Sauti hizi ni mbili katika Kiswahili Sanifu: /**tʃ**/ na /**ɟ**/

| /tʃ/ | / **ɟ** / |
|---|---|
| +kons | +kons |
| +kizuiwa kwamizwa | +kizuiwa kwamizwa |
| +kaakaa gumu | +kaakaa gumu |
| -ghuna | +ghuna |
| -nazali | -nazali |

#### 2.1.1.3 Vikwamizwa

Katika kutamka sauti hizi, ala za matamshi tofauti tofauti hukaribiana sana na kuacha mwanya mdogo ambamo hewa hupitia huku ikitoa sauti ya mkwaruzo. Sauti hizi ndizo nyingi katika lugha ya Kiswahili. Nazo ni /f/,/v/s/,/z/,/ɵ//ð/,/ʃ/,/ɤ/,/h/.

Sifa zake bainifu:

| /f/ | /v/ | /s/ | /h/ |
|---|---|---|---|
| +kons | +kons | +kons | +kons |
| +kikwamizwa | +kikwamizwa | +kikwamizwa | +kikwamizwa |
| +midomo-meno | +midomo-meno | +ufizi | +glota |
| -ghuna | +ghuna | -nazali | -nazali |
| -nazali | | -ghuna | -ghuna |

/z/

+kons
+kikwamizwa
+ufizi
-nazali
+ghuna

/ɵ/

+kons
+kikwamizwa
+menoni
-nazali
-ghuna

/ð /

+kons
+kikwamizwa
+menoni
-nazali
+ghuna

/ɣ/

+kons
+kikwamizwa
+kaakaa laini
+ghuna
-nazali

/ʃ/

+kons
+kaakaa gumu
+ufizi
-nazali
+ghuna

### 2.1.1.4 Nazali

Wakati wa kutamka sauti za nazali au ving'ong'o, hewa hufungiwa mahali mbalimbali katika bomba la sauti kisha huachiliwa kupitia kwenye chemba cha pua na wakati huo huo baadhi ya hewa ikipitia kinywani. Sauzi hizi ni /m/,/n/,/ɲ/na /ŋ/.

Sifa zifuatazo hutumika kuzibainisha.

/m/

+kons
+midomo
+nazali
+ghuna

/n/

+kons
+ufizi
+nazali
+ghuna

/ɲ/

+kons
+kaakaa gumu
+nazali
+ghuna

/ŋ/

+kons
+kaakaa laini
+nazali
+ghuna

### 2.1.1.5 Kitambaza

Wakati wa kutama kitambaza, ncha ya ulimi hugusa ufizi na kutatiza mkondo wa hewa. Hewa huruhusiwa kupita (kutambaa) pembezoni mwa ulimi. Lugha ya Kiswahili Sanifu ina kitambaza kimoja /l/.

$$
/l/ \begin{pmatrix} +\text{kons} \\ +\text{kitambaza} \\ +\text{ufizi} \\ +\text{ghuna} \\ -\text{nazali} \end{pmatrix}
$$

### 2.1.1.6 Kimadende

Kimadende hutamkwa huku ncha ya ulimi ikigotagota kwenye ufizi huku hewa ikiendelea kupita na kusababisha mrindimo wa ulimi. Kiswahili Sanifu kina kimadende kimoja: /r/. Fonimu kitambaza na kimadende hujulikana kwa pamoja kama likwidi.

$$
/r/ \begin{pmatrix} +\text{kons} \\ +\text{kimadende} \\ +\text{ufizi} \\ +\text{ghuna} \\ -\text{nazali} \end{pmatrix}
$$

**Kielelezo 5: Jedwali la Konsonanti zaKiswahili Sanifu**

| **Mahali pa kutolewa** / **Namna ya kutolewa** | Mido moni | Midomo + meno | men oni | ufizi ni | Kaak aa + ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | Koro meo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vipasuo | /p/ /b/ | | | /t//d/ | | | /k//g/ | |
| Vizuiwa vikwamizwa | | | | | | /tʃ//ɉ/ | | |
| Vikwamizwa | | /f//v/ | /ɵ//ð/ | /s//z/ | /ʃ/ | | /ɤ/ | /h/ |
| Nazali | /m/ | | | /n/ | | /ɲ/ | /ŋ/ | |
| Kitambaza | | | | /l/ | | | | |
| Kimadende | | | | /r/ | | | | |
| Nusu irabu | /w/ | | | | | /j/ | /w/ | |

Tanbihi: nusu irabu /w/ imetiwa katika kaakaa laini na mdomoni kwa kuwa sauti hii inapotamkwa sehemu ya nyuma ya ulimi huinuka na kukaribia kaakaa laini jinsi irabu ya nyuma /u/ ifanyavyo na hii ndio sababu irabu /u/ uyeyushwa na kuwa /w/ inapotanguliwa na irabu nyingine isiyo /u/. Vilevile, imetiwa midomoni maadamu midomo huviringwa wakati wa kuitamka.

### 2.1.2 Fonimu za nusu irabu za Kiswahili Sanifu

Lugha ya Kiswahili ina nusu irabu mbili: /j/ na /w/. Nusu irabu pia huitwa viyeyusho au glaidi. Sauti hizi zinapotamkwa ala husika hazikaribiani kiasi cha kutatiza mkondo-hewa kama ilivyo katika konsonanti na vilevile haziachani kiasi cha kutoathiri hewa kama ilivyo katika utamkaji wa irabu. /w/ hutamkwa midomo ikiwa imeviringwa na shina la ulimi likiinuliwa kuelekea

kwenye kaakaa laini. /j/ hutamkwa midomo ikiwa imetandazwa huku bapa la ulimi likiwa limeinuliwa kuelekea kwenye kaakaa gumu. Sauti hizi tutazianisha kama konsonanti kwa sababu ya uamilifu wake kisilabi. Yaani, sauti za nusu irabu haziwezi kuunda silabi peke yake kama irabu bali huandamanishwa na irabu kama baadhi ya konsonanti. Aidha, nusu irabu haiwezi kamwe kuwa kilele cha silabi kama irabu. Nusu irabu huweza tu kuwa kitangulizi au mwanzo wa silabi.

### 2.1.3 Fonimu za irabu za Kiswahili Sanifu

Kiswahili Sanifu kina irabu tano ambazo ni: /a/, /ɛ/, /i/, /ɔ/ na /u/ sauti hizi za irabu ndizo huungana na konsonanti kuunda silabi. Wakati wa kutamka sauti hizi, mkondo-hewa huwa hautatizwi na ala za matashi. Irabu huainishwa kwa kutumia vigezo vitatu ambavyo ni: Sehemu ya ulimi, mwinuko wa ulimi na mkao wa mdomo.

#### 2.1.3.1 Sehemu ya ulimi

Sehemu ya ulimi inayohusika wakati wa kutamka irabu hurejelewa. Sehemu hii inaweza kuwa ya mbele, kati au nyuma. Katika Kiswahili Sanifu irabu za mbele ni /ɛ/ na /i/ ilhali zile za nyuma ni /ɔ/ na /u/. Irabu ya kati ni /a/.

#### 2.1.3.2 Mwinuko wa ulimi


Ulimi una uwezo wa kuinuka juu ukawa sambamba na sehemu ya juu ya kinywa au ukainuka wastani au ukalala kwenye sakafu ya kinywa. Irabu zitamkwazo ulimi ukiwa umeinuliwa juu kabisa huwa na sifa ya [+juu] nazo ni /i/ na /u/. Irabu zinazotamkwa ulimi ukiwa umeinuka wastani ni /ɛ/ na /ɔ /. Irabu ambayo hutamkiwa katika sehemu ya chini mwa kinywa ni /a/.

#### 2.1.3.3 Mkao wa mdomo

Midomo inaweza kuwa katika hali ya mviringo au ikawa imetandazwa wakati wa kutamka irabu. Irabu zinazotamkwa midomo ikiwa imeviringwa ni /ɔ/ na /u/ nazo irabu /a/, /ɛ/ na /i/ hutamkwa midomo midomo ikiwa imetandazwa. Hata hivyo, kiwango cha mviringo au mtandazo huwa tofauti kulingana na irabu inayohusika mathalani mdomo hutanda wakati wa kutamka /a/ zaidi ya

/ɛ/ na /i/ nayo irabu ya /i/ hutamkwa midomo ikiwa imetanda zaidi ya utamkwaji wa /ɛ/. Wakati wa kutamka irabu za nyuma, kiwango cha mviringo pia hutegemea kiwango cha mwinuko. Irabu ya juu /u/ huwa na mviringo mkubwa kuliko irabu /ɔ/. Mchoro ufuatao unaonyesha namna irabu za Kiswahili hutamkwa

**Kielelezo 6: Fonimu za Irabu za Kiswahili Sanifu**




Asili: Otiende (2013)

**Kielelezo 7: Sifa bainifu za irabu za Kiswahili Sanifu**

| | **/a/** | **/ɛ/** | **/i/** | **/ɔ/** | **/u/** |
|---|---|---|---|---|---|
| *Juu* | - | - | + | - | + |
| *Chini* | + | - | - | - | - |
| *Nyuma* | - | - | - | + | + |
| *Mbele* | - | + | + | - | - |
| *Mviringo* | - | - | - | + | + |
| *Kaze* | + | - | + | - | + |
| *Kati* | + | - | - | - | - |

Asili: Otiende (2013)

Katika jedwali hili tunaona ya kwamba irabu ambazo ni [+*juu*] na [+*nyuma*] zina sifa za [+*mviringo*]. Kwa hivyo /u/ ambayo ni sauti ya [+*juu*] na pia [+*nyuma*] ina sifa ya [+*mviringo*]. Vivyo hivyo sauti za [–*nyuma*] na [–*juu*] ni [–*mviringo*]. Sauti hizo ni /a/ na /ɛ/. Vile vile, sauti

za [–*chini*] na [-*nyuma*] ni [+*mbele*] nazo ni /ɛ/ na /i/. Sauti za [-*chini*] na [-*juu*] ni [-*kaze*]. /a/ pekee ndiyo [+*kati*].

### 2.2 Fonimu za Kitigania

Katika sehemu hii istilahi lugha na lahaja zitatumika kwa pamoja kurejelea dhana ile ile moja ya lugha. Hii ni kutokana na mjadala uliopo kuhusiana na mipaka wazi ya kutofautisha dhana hizi mbili. Ross M. (1997; 212) anapendekeza matumizi ya istilahi ya Kiingereza, *lect* kurejelea lugha na lahaja. Kitigania kina makundi matatu ya fonimu kama Kiswahili: Konsonanti, nusu irabu na irabu.

#### 2.2.1 Konsonanti za Kitigania

Kuna maoni mbalimbali kuhusiana na idadi kamili ya konsonanti za Kitigania. Hata wale wanaokubaliana kuhusiana na idadi hiyo hawaelekei kukubaliana kuhusu aina fulani ya kitamkwa kinachofaa kutiwa au kutotiwa katika orodha husika. Kwa mfano, Mberia (1981) na Maore (2011) wanaorodhesha 23. Maore anajumuisha /nð/ ilhali Mberia haiorodheshi. Utafiti huu utaainisha konsonanti 25 (Pamoja na nusu irabu). Hii ni kwa sababu Maore hakujumuisha fonimu /ɉ/. Pia fonimu /l/ itajumuishwa.  Ikumbukwe kuwa fonimu za Kimeru/Kitigania ambazo hupatikana katika Kiswahili Sanifu huwa na sifa bainifu sawa.

##### 2.2.1.1 Vizuiwa sighuna

Kitigania kina vizuiwa sighuna vitatu /p/, /t/ na /k/

Mifano:

| Fonimu | grafimu | Kitigania | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /p/ | p | gapandi  /ɤapandi/ | Kijipanzi/panzi mdogo |
| /t/ | t | toro /tɔrɔ/ | usingizi |
| /k/ | k | kĩratũ /kerato/ | kiatu |

### 2.2.1.2 Vizuiwa nazalishwa

Lahaja ya Kitigania huwa na vizuiwa nazalishwa sita. /mp/, /mb/, /nt/,/nd/, /ŋk/, /ŋg/

Mifano:

| Fonimu | grafimu | Kitigania | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /mp/ | mp | mpara /mpara/ | njaa |
| /mb/ | mb | mbiti /mbiti/ | fisi |
| /nt/ | nt | ntamĩĩ /ntame:/ | mararuraru |
| /nd/ | nd | nduka /nduka/ | nduka |
| /ŋk/ | nk | nkima /ŋkima/ | ugali |
| /ŋg/ | ng | ngatũnyi /ŋgatoɲi/ | simba |

### 2.2.1.3 Vikwamizwa nazalishwa

Kitigania kina vikwamizwa nazalishwa vitatu: /nð/, /ɲc/ɲɟ/

Mifano:

| Fonimu | Grafimu | Kitigania | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /nð/ | nth | nthoni /nðɔni/ | haya |
| /ɲc/ | nc | ncobi /ɲcɔβi/ | pombe |
| /ɲɟ/ | nj | njogu /ɲɟɔɣu/ | ndovu |

#### 2.2.1.4 Nazali

Lugha ya Kitigania kina nazali nne: /m/ /n/, /ɲ/ na /ŋ/

Mifano:

| Fonimu | grafimu | Kitigania | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /m/ | m | mami /mami/ | mama |
| /n/ | n | nene /nɛnɛ/ | nene |
| /ɲ/ | ny | nyanki /ɲanki/ | nyasi |
| /ŋ/ | ng’ | ng’ina /ŋina/ | mama |

#### 2.2.1.5 Vikwamizwa

Kuna vikwamizwa vitano: /β/, /ð/, /c/, /ɟ/ na /ɣ/

Mifano:

| Fonimu | grafimu | Kitigania | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /β/ | b | biimba /βi:mba/ | vimba |
| /ð/ | th | ũthiũ /oðio/ | uso |
| c | c | cukuru /cukuru/ | shule |
| /ɟ/ | j | kajira /kajira/ | kijia |
| /ɣ/ | g | iiga /i:ɣa/ | jiwe |

### 2.2.1.6 Likwidi

#### 2.2.1.6.1 Kimadende

Kitigania kina kimadende kimoja tu ambacho ni /r/

Mfano.

| Fonimu | grafimu | Kitigania | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /r/ | r | rugira /ruɣira/ | pikia |
| | | **r**ukĩĩ**r**i / roke:re/ | asubuhi |

#### 2.2.1.6.2 Kitambaza

Kama Kiswahili, Kitigania kina kitambaza kimoja /l/

| Fonimu | grafimu | Kitigania | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /l/ | l | lambu /**l**ambu/ | maringo |
| | | Ti**l**a | lima kwa uma |

### 2.2.1.7 Nusu irabu

Kama Kiswahili, Kitigania kina glaidi mbili ambazo ni /w/ na /j/

Mfano.

| Fonimu | grafimu | Kitigania | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /w/ | w | waaku /wa:ku/ | wako |
| /j/ | y | yakwa /jakwa/ | yangu |

**Kielelezo 8: Jedwali la Konsonanti za Kitigania**

| **Mahali pa kutolewa** / **Namna ya kutolewa** | Midomoni | menoni | ufizini | Kaakaa gumu | Kaakaa laini |
|---|---|---|---|---|---|
| Vipasuo | /p/ | | /t/ | | /k/ |
| Vikwamizwa | /β/ | /ð/ | **/c/** | /ɟ/ | /ɤ/ |
| Nazali | /m/ | | /n/ | /ɲ/ | /ŋ/ |
| Kimadende | | | /r/ | | |
| Kitambaza | | | /l/ | | |
| Nusu irabu | | | | /j/ | /w/ |
| Vizuiwa-nazalishwa | /mp/,/mb/ | | /nt/,/ nd/ | | / ŋk/, /ŋg/ |
| Vikwamizwa - nazalishwa | | /nð/ | | /ɲc/, /ɲɟ/ | |

### 2.2.2 Irabu za Kitigania


Lahaja ya Kitigania huwa na vokali saba kama zilivyo lugha nyingi za kibantu. Irabu hizi ni: /a/, /ɛ/, /e/,/i/, /ɔ/, /o/ na /u/. Kielelezo kifuatacho kinaonyesha mifano ya irabu hizi katika maneno.

**Kielelezo 9: Mifano ya irabu za Kitigania katika maneno**

| Fonimu | grafimu | Kitigania | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /a/ | a | aka /aka/ | jenga |
| /ɛ/ | e | enda /ɛnda/ | penda |
| /e/ | î | îgamba /eɣamba/ | kesi |
| /i/ | i | irio /iriɔ/ | chakula |
| /ɔ/ | o | roga /rɔɤa/ | roga |
| /o/ | ŭ | ŭkŭrŭ /okoro/ | uzee |
| /u/ | u | umaga /umaɣa/ | kojoa |

Ni ada kwa Wameru kutamka irabu kwa wakaa mrefu yaani kwa kuivuta. Katika baadhi ya maneno, wakaa huu huweza kutofautisha maana. Kwa mfano: arî /are/ (hapana) na aarî /a:re/ (wasichana) au eku /ɛku/ (yako) na eeku /ɛ:ku/ (yuko). Baadhi ya wanaisimu mathalani, Kanana (2011) wanaona lugha ya Kimeru kuwa na irabu kumi na nne yaani kila irabu ikiwa na irabu yenzake; fupi na ndefu. Katika utafiti huu hali hii itachukuliwa kama inayotokana na sifa za kiarudhi zinazodhihirishwa na wazungumzaji wa lugha husika. Jambo hili pia hudhihirika katika Kiswahili ambapo tuna maneno kama vile kaakaa /ka:ka:/, kaa /ka:/na paa /pa:/ ilhali "a:" haichukuliwi kama vokali ndefu ya Kiswahili.

**Kielelezo 10: Mahali na namna ya kutamka irabu**




**Kielelezo 11: Sehemu na mwinuko wa ulimi zinazohusika katika kutamka irabu**


| Mwinuko wa ulimi | Sehemu ya ulimi | | |
|---|---|---|---|
| | Mbele | Katikati | Nyuma |
| Juu | i | | u |
| Kati-juu | e | | o |
| Kati-chini | ɛ | | ɔ |
| Chini | | a | |

## 2.3 Silabi za Kiswahili Sanifu

Silabi ni muhimu katika utafiti huu hususan katika kiwango cha kifonolojia. Goldsmith (1990:153) anaeleza kuwa silabi imo kwenye kiini cha uwakilisho wa kifonoloji. Katamba F. (1989: 153) anaiangalia silabi kama mhimili muhimu katika uwasilishaji wa mifanyiko ya kifonolojia. Anaiona silabi kama tukio la kifonolojia pekee ambalo haliwezi likafungamanishwa na viwango vya kisarufi au kisemantiki. Kimsingi, silabi inaweza kuelezwa kama pigo moja la sauti ambalo linaweza kutamkika kwa mpumuo mmoja wa hewa.

Roach (2000:70) anabainisha umbo la silabi na kutambua kuwa silabi huwa na sehemu tatu ambazo ni: mwanzo/kitangulizi (*onset*) na kilele/kiini (*nucleus/peak*) na kifungio/koda (*coda/margin).* Sehemu hizi anazigawa kuwili yaani: mwanzo/kitangulizi na kina (*rhyme*). Kina kinajumuisha kilele/kiini na koda. Kila silabi lazima iwe na kilele ambacho katika lugha nyingi huwa irabu au nazali inayojisimamia kama silabi. Sehemu ya mwanzo, hukaliwa na konsonanti inayotangulia kilele nayo koda/kifungio huwa konsonanti inayofuata kilele. Mawazo haya ya Roach yanajikita katika mawazo ya wanamiundo mapokeo ambao waliangazia umbo ndani la silabi kwa kutumia mchoro wa kimatawi na kuweka wazi vipengele vyake.Wataalamu hawa wakiwemo, Pike (1967) na Pulgram (1970) walidhihirisha umbo ndani la silabi kwa kutumia mchoro ufuatao: Katika mchoro unaofuata, tutatumia silabi funge **muh-** kutoka katika neno [**muh**$ta$sari]” kufafanua umbo hili.

**Michoro12: Umbo ndani la silabi.**



### 2.3.1 Aina za silabi

Kiswahili kina aina mbili za silabi yaani silabi wazi na silabi funge. Silabi wazi ni silabi mbayo haina koda. Hii ina maana kuwa silabi hii huishia kwa irabu. Kwa mfano, /**ta**$ti$za/. Silabi funge ni silabi ambazo huishia kwa konsonanti yaani huwa na kifungio. Mfano: /**nuk**$ta/ Maneno yenye silabi funge aghalabu huwa ni maneno ya mkopo.

### 2.3.2 Miundo ya silabi

Lugha ya Kiswahili Sanifu huwa na miundo ifuatayo ya silabi:

#### 2.3.2.1 Muundo wa Konsonanti na irabu (KI)

Huu ndio muundo wa silabi unaopendelewa zaidi na takribani lugha zote ulimwenguni na hakuna lugha ambayo imeripotiwa kukosa muundo huu hadi sasa (Gatamba 1989:160). Ni kutokana na muundo huu ambapo miundo mingine ya silabi huzalizika ama kwa kuogezea konsonanti na kuzidondosha. Muundo huu aidha ndio mtoto hujifunza kwanza katika mchakato wa upataji lugha kabla ya kuipata miundo mingine. Katika lugha ya Kiswahili, mifanyiko mingi ya kifonolojia huwa na msukumo wa ama kushabihiana ama kuukaribia. Kwa mfano, nomino zote zinazozalishwa kutokana na vitenzi ambavyo mizizi yake inaishia kwa vokali huchopekwa fonimu /z/ ili kuvunja mkururo wa irabu na kupata muundo pendwa (KI) wa silabi. Mifano:

| **Kitenzi** | **Nomino zalishwa** |
|---|---|
| /za.a/ | /m$za$i/→/m$za$**z**i/ |
| /lɛ.a/ | /m$lɛ$i/→/m$lɛ$**z**i/ |
| /ka.a/ | /m$ka$i/→ /m$ka$**z**i/ |
| /tɛmbɛ.a/ | /m$tɛ$mbɛ$i/→/m$te$mbɛ$**z**i/ |

Hata vitenzi ambavyo mizizi yake huishia kwa vokali vinaponyambuliwa katika kauli ya kutendea, fonimu /l/ huchopekwa. Kwa mfano:

| **Kitenzi** | | **kauli ya kutendea** |
|---|---|---|
| /tɔ.a/ | → | /tɔ$e$a/→/tɔ$**l**ɛ$a/ |
| /ti.a/ | → | /ti$i$a/→/ti$**l**i$a/ |
| /u.a/ | → | /u$i$a/→/u$**l**i$a/ |

Vilevile, udondoshaji wa irabu kutoka umbo la ndani hadi umbo nje, hunuia kupata muundo huu. Kwa mfano:

/pa+ɔte/ → /pɔ$tɛ/

/mi+iɲginɛ/→ /mi$ngi$nɛ/

Uyeyushaji vilevile hupata motisha kutokana na hali hii. Mfano:

/u+ibi/→/wi$zi/

Hata uwiano wa irabu husababishwa na hali hiyo hiyo. Kwa mfano:

/wa+iɲgine/→/wɛ$ɲgi$nɛ/

Mifano zaidi.

/ʃ**a**$ba/

/**si**$mu/

/**ða**$mbi/

**2.3.2.2 Muundo wa Konsonanti Konsonanti na Irabu (KKI)**

Katika muundo huu sehemu ya mwanzo hukaliwa na konsonanti mbili ambapo konsonanti inayotangulia yenzake huwa nazali.

Mifano:

**/mbu**$zi/

/**ŋga**$mi$a/

/tu$**nda**/

**2.3.2.3 Muundo wa Konsonanti pekee (K)**

Muundo huu huhusisha sauti nazali / n/ na /m/ pekee. Nazali hizi hazihitaji msaada wa irabu. Kwa mujibu wa **Massamba** (2001), nazali hizi zina usonoranti mkubwa kiasi cha kuziwezesha kutamkika.

Mifano:

/**m**$tɔ$tɔ/

/**n**$nɛ/

/na$**m**$na/

### 2.3.2.4 Muundo wa irabu pekee (I)

Muundo huu huwa na irabu pekee inayojisimamia kama silabi. Irabu kama zilivyo nazali /m/ na /n/, huwa na usonoranti mkubwa. Hawkins (1984) anaziweka irabu katika nafasi ya kwanza katika ngazi za usonoranti (*sonorarity hierarchy)* zikifuatwa na viyeyusho, likwidi, nazali, vifulizwa ghuna na vifulizwa visoghuna. Mifano ya maneno yenye muundo huu:

/**u**$a/

/**ɔ**$na/

/zɔ$**ɛ**$**a**/

### 2.3.2.5 Muundo wa Konsonanti Glaidi na Irabu (KGI)

Muundo huu huhusisha konsonanti moja ambayo hufuatwa na nusu irabu kisha irabu. Kwa mfano:

/**twi**$ga/

/m$**pwi**$tɔ/

/ki$**tʃwa**/

### 2.3.2.6 Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Glaidi na irabu (KKGI)

Muundo huu huwa na konsonanti ya nazali kisha ikafuatwa na konsonanti kisha glaidi ambayo hufuatwa na irabu. Mifano ya baadhi ya maneno ni:

/**ndwɛ**lɛ$ /

/tʃi$**ɲɟwa**/

/fu$**nzwa**/

#### 2.3.2.7 Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Konsonanti na irabu (KKKI)

Muundo huu hupatikana katika maneno yaliyokopwa. Mifano:

/skru$bu/

/spri$ŋgi/

#### 2.3.2.8 Silabi funge

Silabi hizi huishia kwa konsonanti. Muundo huu pia hujitokeza katika maneno yaliyokopwa. Mifano:

/haf$la/

/Bais$k**ɛ**li/

/mak$taba/

## 2.4 Silabi za Kitigania

Lahaja ya Kitigania huwa na miundo mbalimbali ya silabi ingawa sio mingi kama ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Miundo hii ni kama ifuatavyo. Muundo wa Konsonanti na Irabu (KI), Irabu pekee (I), Konsonanti mbili na Irabu (KKI) na Konsonanti tatu na Irabu (KKKI).

### 2.4.1 Muundo wa Konsonanti na Irabu (KI)

Huu ndio muundo maarufu katika maneno mengi ya Kitigania. Mifano:

/**ri**$ɲga/ (piga)

/**mo**$te/ (mti)

Maneno yanapokopwa kutoka lugha nyingine, hufanyiwa marekebisho ya kimaksudi ili yashabihiane na mu

undo huu pendwa. Mifano:

/βɛ$**tɛ**$**ro**$ri/ (petroli)

/**mo**ɣatɛ**/** (mkate)

**2.4.2 Muundo wa Konsonanti,Konsonanti na Irabu (KKI)**
Muundo huhusisha konsonanti mbili na irabu ambapo konsonanti inayotangulia yenzake huwa nazali. Aidha, muundo huu hujengwa na konsonanti huku ikifuatwa na nusu irabu na irabu. Mifano.

**/mpi**$**ɔ/** (baridi)

/**kjɔ**$**ŋgɔ**/ (kichwa)

/**nku**$ma/ (sifa)

**2.4.3 Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Konsonanti na irabu (KKKI)**
Silabi hizi huundwa kwa konsonanti mbili pamoja na kiyeyusho. Konsonanti ya kwanza huwa nazali. Mifano:

/**ŋgwa**$ta/ (nishike)

/**mbwɛ**/ (mbweha)

/**ndwa**$m**ɛ/** (nisimame)

**2.4.4 Muundo wa Irabu pekee (I)**
Muundo huu huwa sawa na ulivyo muundo ule wa Kiswahili.

Mifano:

/**a**$re$mi/ (wakulima)

/a$ra$**u**$ɤa/ (akasema)

**2.5 Hitimisho**
Sehemu hii imeangazia fonimu na muundo wa silabi wa lugha ya Kiswahili na ile ya Kitigania. Mfanano mkubwa umedhihirika baina ya lugha hizi mbili kwa kuwa ni lugha za kibantu. Hata hivyo, kwa kuwa lugha mbili haziwezi kuwa sawa kikamilifu, tofauti kadha zimejitokeza. Kwa mfano, tumeonyesha kwamba lugha ya Kiswahili Sanifu na Kitigania zina jumla ya konsonanti

sawa; 25 na 25 (nusu irabu zikijumuishwa) mtawalia. Konsonanti zifuatazo zimejitokeza katika lugha hizi mbili: /p/,/t//k/,/ð,/ɣ/,/m/,/n/,/ɲ/,/ŋ/,/r/,/l/,/y/na /w/. Aidha, Kiswahili kimeonyesha kuwa na konsonanti ambazo hazijitokezi katika lahaja ya Kitigania. Konsonanti hizi ni pamoja na (i) Vizuiwa ghuna: /b/,/d/,/g/ (ii) Kizuiwa kwamizwa /tʃ/ (iii) Vikwamizwa /f//v//ɵ//s//z/ /ʃ/na /h/. Vivyo hivyo kuna konsonanti ambazo zimepatikana katika lugha ya Kitigania ambazo hazikupatikana katika mfumo wa lugha ya Kiswahili Sanifu. Konsonanti hizi ni kama zifuatazo: /β/,/c/, /mp/,/mb//nt/,/nd/,/ɲk/, /ɲg//nð//ɲc/ na/ɲɟ/. Ikumbukwe kwamba kikwamizwa ghuna /ð/ katika Kitigania hujitokeza kiothografia kama fonimu /ɵ/ ya Kiswahili. Yawezekana tofauti hii ilitokana na kosa lililofanywa na wale waliotayarisha mfumo wa othografia ya Kimeru kwa ujumla.

Katika upande wa irabu, mfanano na msigano ulioshuhudiwa kwenye konsonanti unajidhihirisha pia. Kiswahili Sanifu kina irabu tano nacho Kitigania kina saba kama alivyoona Mathews (1997:384) anaposema kuwa lugha nyingi za kibantu zina irabu baina ya tano na saba. Lugha ya Kiswahili na ile ya Kitigania zimeonyesha kuwa na irabu /a/, /ɛ/,/i/, /ɔ/ na /u/. Kitigania kina irabu mbili zaidi ambazo ni /e/na /o/. Jambo jingine ambalo limejitokeza hapa ni kwamba lugha ya Kitigania huwa na wakaa mrefu katika utamkaji wa irabu jambo ambalo hujitokeza kwa kiwango kidogo katika Kiswahili Sanifu.

Kando na fonimu, lugha hizi mbili zimedhihirisha miundo sawa na vilevile miundo tofauti ya silabi. Miundo ya konsonanti na irabu (KI), Irabu pekee (I), konsonanti mbili na irabu (KKI) na konsonanti tatu na irabu (KKKI) imo kwenye lugha zote. Hata hivyo, lugha ya Kiswahili ina miundo ambayo haipatikani kwenye lahaja ya Kitigania. Miundo hii ni pamoja na muundo wa konsonanti pekee (K), muundo wa silabi funge na miundo mingine ya kigeni kama vile mfuatano wa konsonanti tatu zisizo viyeyusho pamoja na irabu (KKKI). Hii ina maana kwamba, silabi zote za lugha ya Kitigania huwa silabi huru; lazima ziishie kwa irabu. Ingawa nazali huweza kujisimamia kama silabi katika Kiswahili, hali hii hairuhusiwi katika Kitigania. Hii ndiyo sababu tumepata mifano kama vile, /mote/ (mti) na /moɣatɛ/ (mkate).

Kimsingi sehemu hii itakuwa ya umuhimu mkubwa katika uchanganuzi wa makosa yatakayojitokeza kwenye kazi za wanafunzi. Tunatarajia sehemu hii kutoa ushahidi kuhusiana na

visababishi vya baadhi ya makosa hayo. Isitoshe, kutokana na mifano michache ambayo imeshatolewa inaweza kudhihirika kuwa maumbo ya maneno ya Kiswahili na yale ya Kitigania yanakaribiana. Kwa mfano, maneno yafutayo katika lugha ya Kiswahili na Kitigania /rɔga/ na /rɔɤa/, /ɛnda/ (nenda) na /ɛnda/ (penda) yanafanana kimuundo mtawalia. Pia, imedhihirika kwamba lugha hizi mbili zinanyambuliwa na kuambishwa. Kwa mfano, /pikia/ na /ruɤira/, /ɔmbɛa/ na /rɔmbɛra/. Hali hizi zitasaidia kuonyesha namna lugha kati inavyokiuka kanuni (za kifonolojia na kimofolojia) za lugha lengwa ambayo ni Kiswahili Sanifu hasa kwa mujibu wa mifanyiko ya kisaikolojia ya nadharia tumikizi ya Lugha-Kati ya Selinker (1972).

# SURA YA TATU

# UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KIFONOLOJIA NA KOMOFOLOJIA

## 3.1 Utangulizi

Katika sehemu hii tutachanganua makosa ya kifonolojia na kimofolojia kama yalivyojitokeza kwenye insha za wanafunzi. Aidha tutatoa sababu za kujitokeza kwa makosa haya tukiongozwa na mifanyiko ya kisaikolojia kama inavyoelezwa katika nadharia yetu tumikizi ya Lugha-Kati. Tutaeleza kwa mfano ikiwa kosa au makosa fulani yanatokana na hali ya mwanafunzi kuhawilisha mfumo au elementi za mfumo wa lugha yake ya kwanza hadi lugha L2, au makosa yanayodhihirika ni tokeo la ujumlishaji mno wa sheria za lugha lengwa (Lugha ya Kiswahili Sanifu kwa muktadha huu) hadi lugha kati au makosa haya yanatokana na mikakati anayobuni mwanafunzi ya kuwasiliana ama iwe ni zao la ufundishwaji usiofaa hususan ikitiliwa maanani kuwa wanafunzi hutarajiwa kuiga na kuzingatia kile ambacho mwalimu wake husema. Vilevile, tutaona ikiwa makosa haya ni tokeo la juhudi za mwanafunzi kubuni mikakati ya kujifunza kufikia umilisi wa Kiswahili Sanifu kwa kujaribu kusahilisha miundo ya lugha lengwa kama anavyofafanua Selinker (1972).

Fonolojia kama tulivyoeleza katika sura ya pili ni tawi la kiisimu linalojihusisha na uchunguzi wa sauti (fonimu) za lugha mahususi. Taaluma hii ya isimu inajihusisha na sifa za lugha mahususi na kuchunguza jinsi sauti hizo zinavyoungana katika kuunda vipashio vingine vikubwa vya lugha husika. Fasili hii inatupelea kudai kuwa kila lugha huwa na mfumo wake wa fonolojia ulio tofauti na wa lugha nyingine. Ikiwa mtumiaji lugha yeyote atauvuruga mfumo huu wa sauti basi utata wa maana iliyokusudiwa utaibuka. Hata hivyo ni muhimu kukumbuka kuwa wanajamii lugha moja au sehemu ya wanajamii lugha hiyo inapokuwa imeathirika na makosa fulani huenda isiyatambue kwa hivyo mawasiliano hayatakwamizwa. Hii ndiyo sababu utaona kuwa watumiaji lugha fulani wataendelea kutamka maneno fulani kwa namna ambayo isiyofaa ilhali hamna kati yao anaona hili kuwa dosari hadi pale ambapo mtu aliye na uelewa wa lugha hiyo atapoingilia kati. Mtumiaji lugha anaposahihishwa kosa lake, mambo matatu yanatarajiwa kufanyika. Kwanza, kuna uezekano wa kulisahihisha mwenyewe hivyo kutolirudia. Pili, anaweza kulisahihisha kosa hilo wakati tu wa kusahihishwa na kulirudia labda kutokana na kughafilika. Tatu, huenda akashindwa kabisa kulisahihisha labda kutokana na uyabisi.

Baada ya kusahihisha insha za wanafunzi makosa kadha yamejitokeza walakini tumejifunga tu na yale yanayohusu uchunguzi wetu kama ilivyobainishwa katika sehemu ya upeo na mipaka. Makosa haya yalidhihirika takriban kwa kila mwanafunzi. Hata hivyo kama nitakavyokuja kuonyesha hatimaye, kuna baadhi ya wanafunzi walioathiriwa zaidi ikilinganishwa na wengine. Pia, kuna aina fulani ya makosa ambayo yana frikwenzi kubwa sana ikilinganishwa na aina zingine. Katika sehemu hii, nitadondoa aina za makosa kisha chini yake nitatoa sababu inayochangia au sababu zinazosababisha kufanywa kwake. Makosa yakifonolojia yaliyojitokeza ni pamoja na:

## 3.2 Makosa ya Kifonolojia

### 3.2.1 Unazalishaji wa vizuiwa na kizuiwa-kwamizwa ghuna

**Mifano:**

| **Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi** | **Uwakilisho wa kifonetiki** | **Kategoria** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|---|
| **n**damu | /ndamu/ | nomino | damu |
| Kusai**n**dia | /kusaindia/ | kitenzi | kusaidia |
| ***m****basi* | /*mbasi/* | *nomino* | *basi* |
| ***m****baraka* | */mbaraka/* | *nomino* | *baraka* |
| **n**gari | /ŋgari/ | nomino | gari |
| **n**gafla | /ŋgafla/ | kielezi | ghafla |
| Ru**n**di | /rundi/ | kitenzi | rudi |

Kutokana na mifano iliyotolewa inadhihirika kwamba wanafunzi wanatia nazali kabla ya konsonanti za vipasuo ghuna /d/, /g/ na /b/. Nazali inayochopekwa inategemea aina ya

konsonanti inayoitangulia. Kwa mfano, kwa kuwa sauti /d/ ni ya ufizini kama tulioonyesha katika sura ya pili tulipoangazia sifa bainifu za konsonanti za Kiswahili sanifu /n/ inasalia. Vilevile kwa kuwa nazali /n/ ni sauti ya ufizini sauti hiyo haibadiliki katika sifa zake za kifonetiki. Walakini nazali /n/ inapotanguliwa na fonimu /g/, /ɟ/ na /b/ umbo na sifa zake za kifonetiki zinabadilika na kuwa /ŋ/,/ɲ/ na /m/ mtawalia. Nazali hiyo inasilimishwa na fonimu inayoitangulia ili kuweza kuchukua sifa za fonimu jirani. Kwa mfano, nazali /n/ hutamkiwa ufizini, inapopakana na sauti /ɟ/ ya kakaa gumu inakaakaaishwa na kuwa nazali /ɲ/ ya kaakaa gumu. Vivyo hivyo /n/ inapopakana na kizuiwa cha mdomoni inabadilika na kuwa nazali /m/ ya mdomoni.

**Sababu**

Sababu kuu ya hali hii ambayo ilijitokeza katika takriban insha zote inatokana na mfumo tofauti wa kifonolojia wa lugha ya Kiswahili na Kimeru. Kama tulivyoona katika sehemu ya pili tulipoainisha fonimu za Kiswahili na Kimeru ilidhihirika kwamba lugha ya Kimeru tofauti na Kiswahili haina vizuiwa ghuna /b/,/d/, na /g/. Badala ya sauti hizi Kitigania kina vinazalishwa /mb/, /nd/,na /ŋg/. Kwa hivyo, kama anavyosema Selinker, ni wazi kwamba wanafunzi wanapokumbana na maneno yenye sauti geni hutegemea mfumo wa sauti wa lugha yao ya kwanza ili kupata sauti inayokaribiana na fonimu hiyo tatizi. Maelezo haya ya Selinker yanathibitika hasa tukiangalia kuwa wanafunzi wanapokosa kizuiwa ghuna /b/ cha mdomoni wanaendea kizuiwa nazalishwa cha mdomoni /mb/ ambacho kinapatikana katika lugha yake bali hawatumii kikwamizwa /β/ cha mdomoni kwani hali hii ingesababisha kuwapo kwa kutengana kwa vitamkwa (*maximum differenciation*). Kwa hivyo tunaweza kudai kuwa kosa hili linadhihirisha juhudi za mwanafunzi za kuunda mfumo wa kifonolojia unaokubalika kwa kujikita kwa mfumo wa Kimeru. Mifano hii ya uchopekaji wa nazali inaonyesha kuwa fonolojia ya Kimeru huathiri othografia ya Kiswahili.

### 3.2.2Uchopekaji na udondoshaji wa fonimu /h/

#### 3.2.2.1 Uchopekaji wa fonimu /h/

| Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi | Uwakilisho wa kifonetiki | Kategoria | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| **h**abiria | /habiria/ | nomino | abiria |
| ra**h**ia | /rahia/ | nomino | raia |
| sita**h**isahau | /sitahisahau/ | kitenzi | sitaisahau |
| **h**ilikuwa | /hilikuwa/ | kitenzi | ilikuwa |
| **h**awali | /hawali/ | kielezi | awali |
| **h**ile | /hilɛ/ | kivumishi | ile |

#### 3.2.2.2 Udondoshaji wa fonimu /h/

| Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi | Uwakilisho wa kifonetiki | Kategoria | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| akuna | /akuna/ | kitenzi | hakuna |
| ana | /ana/ | kitenzi | hana |
| emaema | /ɛmaɛma/ | Kitenzi | hemahema |
| uonekana | /uɔnɛkana/ | Kitenzi | huonekana |
| asubui | /asubui/ | nomino | asubuhi |
| usuni | /usuni/ | nomino | huzuni |
| uko | /ukɔ / | kiwakilishi | huko |

Kutokana na mifano iliyotolewa hapo juu inaonekana kuwa wanafunzi walichopeka fonimu /h/ mwanzoni mwa neno kama katika 'hilikuwa' au katikati kama ilivyo katika neno 'sitahisahau'. Vilevile, fonimu hii hii, inadondoshwa katika hali zilezile. Kwa mfano, mwanzoni 'akuna', katikatika ya neno 'emaema' au katika silabi ya mwisho ya neno. Kwa mfano, 'asubuhi'.

Ruwaza wazi inayodhihirika ni kwamba uchopekaji au udondoshaji wa fonimu hii hutokea kabla ya irabu. Udondoshaji wa fonimu ulipofanywa hususan pale ambapo mwanafunzi alilenga kukana, maana kusudiwa ilipotea. Kwa mfano, mwanafunzi alilenga kusema, "Dereva huyo ana usingizi" akaishia kusema, "Dereva huyo hana usingizi".

**Sababu**

Tabia hii ya wanafunzi kuchopeka na kudondosha fonimu /h/ inaweza kuhusishwa na sababu tatu. Kwanza, konsonanti /h/ haimo katika mfumo wa sauti wa Kitigania. Kwa hivyo wanafunzi walichanganyikiwa ni wakati upi fonimu hii inafaa kutumiwa na ni lini haifai. Pili, hali hii inatokana na kile ambacho Selinker anakiita ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa katika lugha kati. Kwa hivyo, kwa kuwa lugha ya Kiswahili huwa na fonimu /h/ wanafunzi huishia kuitumia kiholela inapotanguliwa na irabu. Tatu, hali hii inatokana na juhudi za wanafunzi kurahisisha miundo ya lugha lengwa kama mkakati wa mawasiliano. Hata hivyo usahilishaji huu ujitokeza tu katika udondoshaji wa /h/ kwani utamkaji wa irabu pekee kama silabi huwa rahisi ikilinganishwa na utamkaji wa silabi ya konsonanti /h/ na irabu.

### 3.2.3 Uchopekaji na udondoshaji wa irabu

Katika mifano niliyokusanya, ni irabu mbili tu /i/ na /u/ ama zilizochopekwa au kudondoshwa zaidi.Irabu /ɛ/ ilijitokeza katika mfano mmoja tu. Majedwali yafuatayo yanadhihirisha hili:

#### 3.2.3.1 Uchopekaji wa irabu /u/

| Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi | Uwakilisho wa kifonetiki | Kategoria | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| m**u**tu | /m**u**tu/ | nomino | Mtu |
| m**u**nene | /m**u**nɛnɛ/ | kivumishi | mnene |
| m**u**lima | /m**u**lima/ | nomino | mlima |
| b**u**reki | /b**u**rɛki/ | nomino | breki |
| niliam**u**ka | /niliam**u**ka/ | kitenzi | /niliamka/ |
| wakam**u**chukua | /wakam**u**chukua/ | kitenzi | wakamchukua |

#### 3.2.3.2 Uchopekaji wa irabu /i/

| Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi | Uwakilisho wa kifonetiki | Kategoria | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| as**i**kari | /as**i**kari/ | nomino | askari |
| alis**i**tuka | /alis**i**tuka/ | kitenzi | alishtuka |
| har**i**dhi | /har**i**dhi/ | nomino | ardhi |
| mwaf**i**rika | /mwaf**i**rika/ | nomino | mwafrika |

**Sababu**

Kutokana na mifano iliyotolewa hapo juu, inadhihirisha mambo mawili. Kwanza, irabu hasa /i/ na /u/ zinatiwa katika maneno yenye silabi mwambatano kwa mfano. **-fri-** kwenye neno, mwa-**fri-**ka ili kuvunja mkururo wa konsonanti kwa lengo la kupata muundo wa silabi pendwa wa KI kurahisisha matamshi. Aghalabu hali hii hujitokeza zaidi kwa maneno yaliyokopwa, Kama vile katika maneno, *askari* na *mwafrika.* Pili, inaonekana kuwa, kinyume na Kiswahili ambacho

huruhusu fonimu za nazali kusimama pekee kama silabi, Kitigania hakiruhusu hali hii kwa kuwa silabi zake zote huwa wazi. Kwa mfano, ‘m**u**lima’ badala ya ‘mlima’. Kwa hivyo, kosa ili bila ya shaka linatokana na athari ya L1 iliyo na muundo tofauti wa silabi na L2. Vilevile, inawezekana kosa hili likatokana na mkakati wa kujifunza L2 hasa wanafunzi wanapojaribu kusahilisha miundo ya L2. Mfano wa uchopekaji wa irabu /ɛ/ nilioupata ni ule wa kutoka kwa neno la mkopo, pet**e**roli /pɛt**ɛ**rɔli/badala ya petroli, msukumo ukiwa ni kupata muundo unaopendelewa katika lugha ya Kimeru.

### 3.2.4 Utumiaji wa sauti mbadala

#### 3.2.4.1 Matumizi ya fonimu /s/badala ya /z/

| **Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi** | **Uwakilisho wa kifonetiki** | **Kategoria** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|---|
| kupote**s**a | /kupote**s**a / | Kitenzi | kupoteza |
| ku**s**ima | /ku**s**ima/ | Kitenzi | kuzima |
| uli**s**a | /uli**s**a/ | Kitenzi | uliza |
| nyama**s**a | /nyama**s**a/ | Kitenzi | nyamaza |
| Wa**s**azi | /wa**s**azi/ | Nomino | wazazi |

#### 3.2.4.2 Matumizi ya /z/ badala /s/ ama /ʃ/

| **Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi** | **Uwakilisho wa kifonetiki** | **Kategoria** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|---|
| Kazi | / kazi/ | *kielezi | kasi |
| Wazasi | /wazasi / | Nomino | wazazi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| kiam**z**akinywa | /kiam**z**akinywa/ | Nomino | kiamshakinywa |

**3.2.4.3 Matumizi ya /s/ badala /ʃ/ ama /tʃ/**

| **Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi** | **Uwakilisho wa kifonetiki** | **Kategoria** | **Kiswahili Sanifu** | **Uwakilisho wa kifonetiki** |
|---|---|---|---|---|
| sida | /sida/ | nomino | shida | /ʃida/ |
| masitaka | /masitaka/ | nomino | mashtaka | /maʃtaka/ |
| suka | /suka/ | kitenzi | shuka | /ʃuka/ |
| kisaka | /kisaka/ | nomino | kichaka | /kitʃaka/ |
| sai | /sai/ | nomino | chai | /tʃai/ |

**Sababu**

Kutokana na mifano kwenye majedwali hayo matatu, ni wazi kuwa wanafunzi huchanganya sauti /z/, /s/,/tʃ/, na /ʃ/ kutokana na sababu tatu. Kwanza, fonimu hizi hazipatikani katika mfumo wa fonimu wa Kimeru. Kwa hivyo, wanafunzi wanaishia kutumia sauti hizi kiholela jambo ambalo huenda likazua utata wa kimaana. Kwa mfano, pale ambapo mwanafunzi anapoandika *suka* badala ya *shuka*. Aidha, maneno mengine, hukosa maana kusudiwa kabisa. Kwa mfano, *sai* badala ya *chai*. Vilevile, tunaweza kudai kuwa kosa hili la kuchanganya sauti ni mkakati wa kuwasiliana. Hoja hii inatiliwa nguvu na ukweli kwamba, watumiaji hawa wa lugha hii wanapowasiliana, mawasiliano yao hayakwamizwi kamwe. Huenda, hata asilimia kubwa yao, (isipokuwa wachache waliofikia umilisi wa L2) wasitambue kuwa mwenzao amekosea). Chanzo kingine, ni kile cha kujumlisha mno kaida za L2 kwenye lugha-kati. Hapa, mwanafunzi hubaini kuwa L2 ina fonimu/z/, /s/,/tʃ/, na /ʃ/ walakini akazitumia kivoloya bila kufahamu fika mahali zinapofaa kutumika sahihi. Kama anavyoeleza Selinker, hali kama hizi ndizo zinazopelekea kuwepo na lugha-kati iliyo na miundo tofauti na L1 na L2.

### 3.2.4.4 Matumizi ya fonimu /g/ badala ya /ɣ/

| Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi | Uwakilisho wa kifonetiki | Kategoria | Kiswahili Sanifu | Uwakilisho wa kifonetiki |
|---|---|---|---|---|
| gala | /gala / | nomino | ghala | /ɣala/ |
| garimu | /garimu/ | kitenzi | gharimu | /ɣarimu/ |
| /ngafla/ | /ŋgafla/ | kielezi | ghafla | /ɣafla/ |

**Sababu**

Kipasuo ghuna /g/ hakipatikani katika mfumo wa sauti wa lahaja ya Kitigania badala yake kikwamizwa cha kaakaa laini /ɣ/ kipo. Jambo linalozua utata hata zaidi ni uwakilishaji wa sauti /ɣ/ kama /g/ kimaandishi katika lugha ya Kimeru kama nilivyoonyesha katika suraya pili. Hali hii inachangia kuwepo kwa kosa hili ingawa linahusisha sauti ambayo imo katika mfumo wao wa kifonolojia.

### 3.2.4.5 Kuchanganya matumizi ya sauti /ð/ na /ɵ/

| Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi | Uwakilisho wa kifonetiki | Kategoria | Kiswahili Sanifu | Uwakilisho wa kifonetiki |
|---|---|---|---|---|
| walithoofika | /wali**ɵ**ɔɔfika/ | kitenzi | walidhoofika | /wali**ð**ɔɔfika/ |
| thambi | /**ɵ**ambi/ | nomino | dhambi | /**ð**ambi/ |
| dhamini | /**ð**amini/ | kitenzi | thamini | /**ɵ**amini/ |
| adhari | /a**ð**ari/ | nomino | athari | /a**ɵ**ari/ |
| thibiti | /**ɵ**ibiti/ | kitenzi | dhibiti | /**ð**ibiti/ |

**Sababu**

Makosa haya yanatokana na athari ya lugha ya kwanza kwa namna mbili. Kwanza, sauti /ɵ/ haimo katika mfumo wa kifonolojia wa Kitigania. Pili, sauti ii hii ambayo haimo katika mfumo wa sauti ndiyo inayotumika kimaandishi kuwakilisha sauti /ð/. Hapa kuna hitilifu inayotokana na waliotayarisha mfumo wa fonolojia ya Kimeru kwa ujumla. Vilevile, kosa hili linaweza kuwa linatokana na ufundishwaji usiofaa, hivi kwamba wanafunzi wamerithishwa makosa jambo ambalo linakuwa gumu kwao kulifahamu. Hali inapokuwa hivi wanafunzi huchanganyikiwa ni sauti ipi kati ya hizo mbili wanafaa kutumia jambo ambalo huchangia uchanganyaji huu. Hata hivyo ni muhimu kusisitiza kwamba, fonimu hizi zinakurubiana katika sifa zake za kifonetiki maadam hutamkiwa mahali pamoja (menoni) na katika jinsi ya kutamka (vikwamizwa) isipokuwa tu kwamba /ð/ ni ghuna na /ɵ/sighuna. Kwa mantiki hii basi, mwanafunzi anapotumia sauti mojawapo ya hizi badala ya yenzake, ule mtengano mkubwa wa sifa za kifonetiki hautokei. Hali hii inakuwa tofauti katika lugha za Kiolusuba kama anavyodai Otiende 2013:81 anapotoa sababu kuhusu tabia ya wazungumzaji hawa kutumia sauti /z/ badala ya /ð/, kwa mfano, kusema /zambi/ badala ya /dhambi/. Anafafanua:

> "Fonimu /ð/ hutamkwa kwa ulimi na meno. Kiolusuba hakina sauti ya meno na ulimi kama /ð/ kwa hivyo sauti /z/ ambayo ni ghuna kama ilivyo / ð/ ndiyo hutamkwa badala yake. Sauti /z/ hutamkwa wakati bapa la ulimi hukaribiana sana na kaakaa gumu [sic] na huku hewa ikipitishwa kwa mkwamzo kandokando mwa ulimi na kusababisha mkwaruzo. Ala hizo husika ndizo zinakaribiana na za kutamka sauti /ð/. Kwa hivyo, mzungumzaji wa Kiolusuba hutumia /z/ ambayo hukaribiana na /ð/ kwa kiasi fulani."

Kwa muhtasari ni kuwa Walosuba hawana ama sauti /ð/ au /ɵ/ na hii ndio sababu wanaendea sauti /z/ ambayo imo kwenye mfumo wao wa kifonolojia. Sababu kuu ya kuichagua sauti hii badala ya /s/ ambayo pia imo kwenye orodha ya fonimu za lugha hiyo ni kwamba inakaribiana zaidi na /ð/ kwamba zote ni vikwamizwa ghuna. Kwa upande wa Watigania, wana mojawapo ya fonimu hizi na ii ndio sababu wanazichanganya badala ya kuendea fonimu zinazotamkiwa kwingine kama vile /s/ ama /z/ ambazo ni fonimu za ufizini.

#### 3.2.4.6 Matumizi ya /b/ badala ya /v/

| Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi | Uwakilisho wa kifonetiki | Kategoria | Kiswahili Sanifu | Uwakilisho wa kifonetiki |
|---|---|---|---|---|
| **biongozi** | /b**iɔngɔzi/** | nomino | viongozi | /viɔngɔzi/ |
| bitanda | /bitanda/ | nomino | vitanda | /vitanda/ |

**Sababu**

Makosa ya namna hii huwa machache hata hivyo sababu kuu inayopelekea kuwapo kwake ni ukosefu wa fonimu /v/ katika lugha ya Kimeru. Badala ya kikwamizwa hiki cha mdomo meno, lahaja ya Kitigania huwa na kikwamizwa cha midomoni /β/ ambacho huwakilishwa kama /b/ kimaandishi. Ni muhimu kuongezea kuwa wanafunzi hawa hawatatiziki kuandika maneno yaliyo na sauti /b/ kama vile, *baba, bangi na bendera* kwa kuwa wanayo sauti inayowakilishwa hivyo kiothografia. Ni muhali kuona wanafunzi wakichanganya matumizi ya fonimu /b/ na /p/ kwa kuwa wanayo sauti /p/ na wanaelewa mipaka ya matumizi yake. Hali hii ni tofauti katika lugha ya Kiekusii ambayo haina sauti /p/ na /b/, hivyo wanafunzi hukanganyika katika matumizi yake. Obara (2012:41) anatoa mifano ifuatayo inayoshadidia dai hili: *ipia* badala ya *ibia* na *pastola* badala ya *bastola*

### 3.2.5 Udondoshaji wa nazali /n/ na /m/

#### 3.2.5.1 Udondoshaji wa nazali /n/

| Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi | Uwakilisho wa kifonetiki | Kategoria | Kiswahili Sanifu | Uwakilisho wa kifonetiki |
|---|---|---|---|---|
| Dugu | /dugu/ | nomino | **n**dugu | **/n**dugu/ |
| Walikujwa | /walikuɟwa/ | kitenzi | walikunjwa | /walikuɲɟwa/ |

**3.2.5.2 Udondoshaji wa nazali /m/**

| **Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi** | **Uwakilisho wa kifonetiki** | **Kategoria** | **Kiswahili Sanifu** | **Uwakilisho wa kifonetiki** |
|---|---|---|---|---|
| Kumraba | /kumraba/ | kitenzi | kumra**m**ba | /kumra**m**ba/ |
| Balamwezi | /balamwezi/ | nomino | mbalamwezi | /mbalamwez/i |
| Matebezi | /matebezi/ | nomino | mate**m**bezi | /mate**m**bezi/ |
| Nikakubuka | /nikakubuka/ | kitenzi | nikaku**m**buka | /nikaku**m**buka/ |


**Sababu**

Kutokana na mifano kutoka kwa majedwali haya mawili inadhihirika kuwa wanafunzi hudondosha ving’ong’o /n/ na /m/ kwa kutegemea sauti inayopakana na nazali husika. Kwa mfano, nazali /n/ hudondoshwa inapotanguliwa na fonimu /d/, na /ɟ/ nayo nazali /m/ ikadondoshwa inapotanguliwa na kipasuo /b/ cha mdomoni. Makosa haya yanatokana na ujumlishaji mno wa kaida za L2 katika lugha-kati. Pia, yanachangiwa na athari ya L1 kwamba, L1 ina fonimu nazalishwa ilhali L2 haina. Ujumlishaji mno unatokea pale ambapo, wanafunzi wanafahamu kuwa lugha ya Kiswahili Sanifu ina fonimu /d/,/ɟ/ na b / na zinaweza kuunda silabi zinapoungana na irabu. Hata hivyo, sifa za kifonetiki zinatiliwa maanani kwani, sauti /m/ ya mdomoni ndiyo inayodondoshwa inapotanguliwa na sauti ya mdomoni /b/. Hivyo hivyo, nazali /n/ ya ufizini ndiyo inayodondoshwa inapotanguliwa na kipasuo ghuna cha ufizini /d/ pamoja na kipasuo-kwamizwa ghuna cha kaakaa gumu /ɟ/ ambacho huweza kukaakaaisha /n/ na kuwa /ɲ/.

## 3.3 Makosa ya Kimofolojia

Mofolojia ni tawi la isimu ambalo huhusika na maumbo na miundo ya maneno na matumizi yake. Tawi hili hujishughulisha na jinsi maneno yanavyoundwa, vipashio vinavyounda maneno hayo na jinsi vipashio hivyo vinavyoainishwa. Kipashio muhimu cha uchanganuzi wa mofolojia ni mofu. Mofu ni kipashio kidogo kabisa ambacho kina uwezo wa kusitiri maana ya neno (mofimu) ambalo kwalo limeundwa.

Kuna uhusiano mkubwa baina ya mofolojia na fonolojia, sintaksia na semantiki. Kwa mfano, mifanyiko ya kifonolojia kama vile, uyeyushaji huhusisha irabu ya mzizi amacho ni kipashio cha mofolojia na fonimu za irabu ambavyo ni vipashio vya fonolojia. Kwa mfano, /muεtu/→ [{mu}+{εtu}]/→/mwεtu/




Aidha, mofu mbalimbali (eneo la mofolojia) huwakilisha maana (eneo la semantiki). Kwa mfano, kitenzi [jia] kina mofu tatu: {j-} mzizi wa kitenzi (cha silabi moja), {-i-) kauli ya kutendea na {-a} kiishio. Aidha, viambishi mbalimbali katika neno huweza kutoa taarifa za sintaksia kama vile yambwa, njeo na hali. Kwa mfano, kitenzi *ame**m**pik**i**a* kina faridi zifuatazo za sintaksia. {-m-} inawakilisha yambwa tendewa (indirect object), mofu {-i-} ya unyambuaji (kauli ya kutendea) inalazimisha kuwepo na yambwa tendwa *(direct object)* kwa kuwa inakifanya kitenzi husika kuwa na uelekezi maradufu (*ditransitivity).* Hivyo, matawi haya huweza kuingiliana, kutegemeana na kukamilishana.

Makosa mengi yanayofanywa na wanafunzi hutokana na uambishaji kwa kuwa lugha hizi mbili huwa na ruwaza sawa ya uambishaji na unyambuaji. Aidha, baadhi ya wanafunzi hutumia maneno ya lugha yao ya kwanza wakidhani kuwa mfanano wa kimaumbo huwa sawa na mfanano wa kimaana jambo ambalo husababisha utata wa kimaana au upotoshi wa maana. Katika jedwali hili, maneno yenye maumbo yanayofanana yamekolezewa wino.

| | **Mifano yenye makosa kutoka kwa wanafunzi** | **Maana sahihi katika Kimeru** | **Kiswahili Sanifu** (Umbo sawa) | **Aina ya neno** |
|---|---|---|---|---|
| **1** | **ng'orota** | toa misono usingizini | **Korota** | kitenzi |
| 2 | (mvua) **iliyomomoa** | Haribu | (mvua) **iliyobomoa** | kitenzi |
| **3** | **murogi** | mchwawi | **Mrogi** | nomino |
| **4** | **masaa** | Saa (katika wingi) | **(*ma)saa** | nomino |
| **5** | **nyumaye** | Baadaye | **nyumaye** (nyuma yake) | kielezi |
| **6** | **kujipanga** (kwa safari) | kujiandaa/kujitayarisha | **kujipanga** (kuweka katika ruwaza/orodha) | kitenzi |
| 7 | (askari) **munene** | mwenye tapo kubwa | **Mnene** | Kivumishi |
| **8** | **Itikia** | Kukubali | **itikia** (itika kwa niaba ya) | Kitenzi |
| **9** | **Tuma** | sababisha | **tuma** (omba mtu aende mahali) | Kitenzi |
| **10** | **Kunyua** (sigara) | Kuvuta | **Kunywa** (kutia kiowevu mdomoni) | Kitenzi |
| **11** | **niliamuka** | Simama | **niliamka**( kutoka usingizini) | Kitenzi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **12** | **ambulansi** | ambulensi | **Ambulensi** | Nomino |
| 13 | (kwa) **sibidi** | Kasi | **Spidi** | Kielezi |
| **14** | **Sikia** (njaa) | ona njaa | **sikia** (kutumia maskio kupata habari fulani) | Kitenzi |
| **15** | **Andika** (kazi) | Ajiri | **andika** (tia maadishi kwa kalamu) | Kitenzi |
| **16** | **na** | Kwa | **na (pamoja na)** | Kihusishi |

Katika jedwali hili inaonekana kwamba wanafunzi wanatumia maneno yenye miundo sawa au inayokaribiana na ile ya Kiswahili sanifu wakidhani kuwa maana yake ni sawa. Kwa mfano, mwanafunzi anapoandika, "Dereva alituma gari lianguke" kitenzi *tuma* kinazua utata na hata maana iliyokusudiwa kupotea kwani tunabaki kujiuliza, tangu lini gari likawa na uwezo wa kuweza kutumwa? Vivyo hivyo mwanafunzi anapoandika, " Niliitikia kuandamana nao hadi hospitalini", kitenzi *itikia* kinaleta dhana tofauti kabisa katika Kiswahili. Baadhi ya maumbo yaliyotumiwa na wanafunzi yalikuwa ya maneno ya kategoria tofauti, hivi kwamba dhana zilizowakilishwa na maumbo hayo zilikuwa tofauti vilevile. Kwa mfano, "Majeruhi walibebwa na *ambulansi kupelekwa hospitalini" Hapa, maana inapotoshwa kwa kuwa mwanafunzi anatumia umbo la kuunganisha badala ya kutumia umbo la kuhusisha (kwa) yaani, "Majeruhi walibebwa kwa *ambulansi kupelekwa hospitalini".

Makosa mengine yanatokana na uundaji wa maneno hasa nomino zalishwa kutokana na vitenzi. Nomino hizi huundwa kwa kuambisha mzizi wa kitenzi kiambishi cha ngeli na pia kudondosha kiishio na kutia {-i} ya unominishaji. Hata hivyo kama nilivyoeleza awali, viambishi ngeli vya nomino ya 1, na 3 lazima viandamanishwe na irabu /u/ jambo ambalo husababisha makosa katika Kiswahili Sanifu. Hali hii huwa vivumishi vinavyofafanua nomino husika. Kwa mfano, [m+u+rog+i]→/murogi/ (mfano 3) na [m+u+nene] →/munene/ (mfano 7). Aidha, kosa jingine

limesababishwa na utaratibu wa kufanyia maneno ya mabadiliko ya kimaksuudi ili yalandane na muundo wa lugha lengwa. K.m, sibidi badala ya spidi (mfano 13, kwa sababu ya uchopekaji wa irabu na pia, kutokuwepo kwa fonimu /b/) au *ambulansi* badala ya *ambulensi* (mfano 12) kutokana na jinsi wazungumzaji hawa wanavyolitamka neno hili.

**Jedwali 13: Frikwenzi ya vyanzo vya makosa**

| **Aina ya kosa/Chanzo cha makosa** | **Lugha ya kwanza** | **Ujumlishaji mno** | **Mkakati wa mawasiliano** | **Mkakati wa kujifunza L2** | **Ufundiswaji potofu** |
|---|---|---|---|---|---|
| Unazalishaji wa vizuiwa na kizuiwa-kwamizwa ghuna | 1 | | | | |
| Uchopekaji na udondoshaji wa fonimu /h/ | 1 | 1 | | 1 | |
| Uchopekaji na udondoshaji wa irabu | 1 | | | 1 | |
| Matumizi ya(/z/badala ya /s/ ), (z/ badala /s/ ama /ʃ/), (/s/ badala /ʃ/ ama /tʃ/) | 1 | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya /g/ badala ya /ɣ/ | 1 | | | | | |
| matumizi ya sauti /ð/ na /ɵ/ | 1 | | | | 1 | |
| Matumizi ya /b/ badala ya /v/ | 1 | | | | | |
| Udondoshaji wa nazali /n/ na /m/ | 1 | 1 | | | | |
| Mfanano wa maumbo ya maneno | 1 | - | 1 | - | - | |
| JUMLA | 9 | 2 | 1 | 2 | 1 | **Jumla 15** |
| **ASILIMIA** | **60%** | **13%** | **6.7%** | **13%** | **6.7%** | |

Kutokana na jedwali hili yafuatayo yanadhirika. Kwanza, kuna uwezekano wa kosa moja kuwa na ama kisababishi kimoja kama lilivyo lile kosa la unazalishaji ama likawa na visababishi zaidi ya kimoja kama lilivyo kosa la kuchopeka au kudondosha fonimu /h/. Pia, inaonekana kuwa visabishi vina idadi ya jumla ya frikwenzi 15. Kati ya idadi hii, lugha ya kwanza, ina frikwenzi 9 ya usababishaji ambayo ni sawa na asilimia 60%, ikafuatiwa na visababishi vya ujumlishaji mno pamoja mkakati wa kujifunza L2 ambavyo vilirekodi frikwenzi sawa ya 2 tu ambayo ni sawa na asilia 13% navyo vile vya Mkakati wa mawasiliano na Ufundiswaji potofu vikarekodi asilimia 6.7% kila kimojawacho.

### 3.4 Hitimisho

Katika sehemu hii, tumechanganua makosa ya kifonolojia na kimofolojia yanayojitokeza kwenye kazi za wanafunzi. Aidha, tumeainisha makosa hayo na hata kueleza baadhi ya sababu zinazochangia makosa hayo. Baadhi ya makosa ya kifonolojia yanayojitokeza ni pamoja na yale ya kunazalisha vizuiwa na vituo-kwamizwa, udondoshaji wa wa sauti, uchopekaji wa irabu na utumiaji wa sauti mbadala. Makosa ya kimofolojia nayo, yameonywa yakitokana na uambishaji na unyambuaji, pamoja na kuwa na maumbo yanayokaribiana.

Chanzo kikuu cha makosa haya kimebainishwa kuwa athari ya lugha ya kwanza kiilichojizolea asilia 60% katika frikwenzi ya usababishaji. Kwa hakika kila kosa limetokana na kisababishi hiki. Chanzo hiki ndicho kikuu kwani wanafunzi wanahawilisha miundo ya lugha yao ya kwanza kama vile miundo ya silabi hadi lugha-kati. Pili,ukosefu wa vitamkwa katika L2, unasababisha wanafunzi kutumia vitamkwa vinavyokaribiana na vile vya L2, kutoka kwa L1 yao na tatu,ukosefu wa faridi fulani katika mojawapo ya lugha ikasababisha wanafunzi kuchanganya vitamkwa kiholela holela kwa kutokuwa na uhakika ni kitamkwa kipi kinafaa kutumika wapi. Vilevile, kama anavyodai Selinker, tumeona kuwa baadhi ya makosa yametokana na hali ya wanafunzi kujumlisha mno kaida za L2 katika lugha-kati yao. Chanzo hiki kilirekodi asilimia 13% na kuchukua nafasi ya pili pamoja na kile chanzo cha mkakati wa kujifunza L2. Hali hii imedhihirika hasa katika lile kosa la kuchanganya sauti. Pia, makosa mengine, ni zao la mkakati wa wanafunzi kuwepesha mawasiliano. Ingawa hali hii hujitokeza zaidi katika mazungumzo, naweza kudai kuwa wanafunzi walihawilisha tabia hii katika maandishi kwani katika Kiswahili, Kitigania na Lugha-Kati inayoshughulikiwa humu, watumiaji lugha aghalabu huandika maneno jinsi yanavyotamkwa. Visababishi vingine vimekuwa ufundishwaji usio sahihi ingawa hali hii ni ngumu kueleza wazi ni nani aliyewafunza wanafunzi hawa visivyofaa. Labda ndio sababu chanzo hiki kimerekodi frikwenzi ya chini 6.7% .

# SURA YA NNE

## UCHANGANUZI WA JINSIA NA KATEGORIA YA MANENO INAYOHUSIKA

### 4.1Utangulizi

Sehemu hii inalenga kubainisha namna jinsia huathiri utokeaji wa makosa ya kifonolojia na kimofolojia yaliyochanganuliwa katika sura ya tatu. Kwa kushughulikia jinsia, tutaweza kujaribisha nadharia ya nne ya utafiti huu inayotabiri kwamba, *zaidi ya asilimia 50% ya makosa itadhihirika katika kazi za wanafunzi wa kiume ikilinganishwa na wenzao wa kike*. Matokeo ya sehemu hii yanaweza kutumika katika kulinganisha matokeo ya tafiti nyingine ambazo zimefanywa. Mathalani, matokeo ya utafiti wa Kang'ahi na wenzake (2016) yalionyesha tofauti kidogo baina ya wanafunzi wa jinsia zote katika mtihani wa kaunti ya Vihiga (2011) katika somo la Kiswahili. Pia, kategoria inayohusika itawekwa wazi. Ili kuwezesha hali hii, majedwali saba yatatumika. Matokeo ya kila shule yatatiwa katika majedwali matatu. Jedwali la kwanza litaonyesha matokeo ya wanafunzi wavulana, la pili lionyeshe yale ya wasichana kisha jedwali la tatu lijumuishe matokeo ya jedwali la kwanza na la pili. Hali itakuwa vivyo hivyo katika shule ya pili (nyingine). Jedwali la saba nalo litadhihirisha matokeo yote ya shule mbili kwa nia ya kufanyia majaribio nadharia tete husika.

### 4.2 Matokeo ya shule ya Kaamu

**Jedwali 4.2.1: Frikwenzi ya makosa yaliyofanywa na wavulana**

| | Nomino | Viwakilishi | Vivumishi | Vitenzi | Vielezi | Viunganishi | Vihusishi | Vihisishi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mvu1 | 2 | 0 | 2 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mvu 2 | 3 | 0 | 0 | 6 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mvu 3 | 3 | 0 | 1 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mvu 4 | 0 | 0 | 1 | 7 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Mvu 5 | 0 | 0 | 3 | 8 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mvu 6 | 2 | 1 | 1 | 5 | 1 | 0 | 1 | 1 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mvu 7 | 1 | 0 | 1 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 8 | 2 | 0 | 3 | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | |
| Mvu 9 | 0 | 0 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 10 | 3 | 0 | 0 | 8 | 3 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 11 | 4 | 0 | 1 | 9 | 0 | 0 | 1 | 0 | |
| Mvu 12 | 5 | 0 | 4 | 6 | 2 | 1 | 2 | 0 | |
| Mvu 13 | 4 | 0 | 2 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 14 | 3 | 0 | 1 | 4 | 1 | 0 | 1 | 0 | |
| Mvu 15 | 0 | 0 | 3 | 8 | 1 | 0 | 0 | 0 | |
| **Jumla ya makosa katika kila kategoria** | 32 | 1 | 24 | 102 | 10 | 1 | 9 | 1 | **Jumla ya makosa 180** |
| **Asilimia %** | 17.78 | 0.56 | 13.33 | 56.67 | 5.56 | 0.56 | 5 | 0.56 | |

Kutokana na jedwali hili, jumla ya makosa 180 yalifanywa na wanafunzi wa kiume. Kategoria ya vitenzi iliibuka kuwa na frikwenzi kubwa zaidi ya 102 ambayo ni sawa na asilimia 56.67%. Kategoria hii ilifuatwa na kategoria ya nomino kwa asilimia 17.78%, nayo ile ya vivumishi ikachua 13.337%. Kategoaria ya vihisishi ilipokea frikwezi ya chini zaidi ya 0.56%. Pia, inaonekana kwamba kosa linalohusu kategoria ya vitenzi lilijitokeza katika insha ya kila mvulana

**Jedwali 4.2.2: Frikwenzi ya makosa yaliyofanywa na wasichana**

| | **Nomino** | **Viwakilishi** | **Vivumishi** | **Vitenzi** | **Vielezi** | **Viunganishi** | **Vihusishi** | **Vihisishi** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Msi1 | 2 | 0 | 1 | 12 | 0 | 0 | 2 | 1 | |
| Msi 2 | 2 | 0 | 0 | 8 | 0 | 1 | 0 | 0 | |
| Msi 3 | 1 | 1 | 1 | 14 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 4 | 2 | 0 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 5 | 1 | 0 | 0 | 8 | 0 | 1 | 0 | 0 | |
| Msi 6 | 0 | 0 | **1** | **6** | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 7 | 1 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 8 | 2 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 9 | 3 | 1 | 1 | 6 | 2 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 10 | 2 | 0 | 1 | 5 | 2 | 0 | 1 | 0 | |
| Msi 11 | 4 | 0 | 2 | 6 | 0 | 0 | 1 | 1 | |
| Msi 12 | 2 | 0 | 1 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 13 | 3 | 0 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 14 | 4 | 0 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 15 | 1 | 0 | 1 | 10 | 2 | 0 | 2 | 1 | |
| **Jumla ya makosa katika kila kategoria** | 30 | 2 | 10 | 110 | 6 | 2 | 6 | 2 | **Jumla ya makosa 168** |
| **Asilimia %** | 17.86 | 1.19 | 5.96 | 65.47 | 4.41 | 3.57 | 4.41 | 1.19 | |

Jedwali hili linaonyesha kwamba, jumla ya makosa 168 yalijitokeza kwenye insha za wanafunzi wa jinsia ya kike. Kati ya makosa haya, kategoria ya vitenzi ilikuwa na frikwezi ya juu zaidi ya asilimia 65.47% ikifuatwa na nomino iliyoonyesha frikwenzi ya 17.86%. Pia ni wazi kwamba

kosa la kategoria ya vitenzi lilijitokeza kwenye insha takrbani zote za wanafunzi wa kike kama ilivyokuwa kwa wenzao wa kiume.

**Jedwali 4.2.3: Jumla ya makosa yaliyofanywa na wavulana na wasichana kutoka shule ya Kaamu**

| **Kategoria** / **Jinsia** | **Nomino** | **Viwakilishi** | **Vivumishi** | **Vitenzi** | **Vielezi** | **Viunganishi** | **Vihusishi** | **Vihisishi** | **Jumla ya makosa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wav | 32 | 1 | 24 | 102 | 10 | 1 | 9 | 1 | 180 | **51.72** |
| Was | 30 | 2 | 10 | 110 | 6 | 2 | 6 | 2 | 168 | **48.28** |
| Jumla | 62 | 3 | 34 | 212 | 16 | 3 | 15 | 3 | **348** | |
| % | 17.82 | 0.86 | 9.77 | **60.92** | 5.60 | 0.86 | 4.31 | 0.86 | | |

Jedwali hili linalinganisha matokea ya wanafunzi wa jinsia zote kwa wazi. Jumla ya makosa 348 yalijitokeza katika insha za wanafunzi. Kati ya makosa haya, jumla ya makosa 180 yalifanywa na wavulana ambayo ni sawa na asilimia 51.72% nao wenzao wa kike wakafanya jumla ya makosa 168 ambayo ni sawa na asilimia 48.28%. Kwa ujumla wanafunzi wa kike waliweza kufanya vizuri kuliko wenzao wa kiume. Aidha, kategoria ya vitenzi iliongoza katika frikwenzi ya utokeaji ikiwa na frikwenzi ya asilia 60.92%, ikifuatwa na nomino kwa 17.82%, vivumishi 9.77% huku asilimia 11.49% iliyosalia ikichukuliwa na aina nyingine za maneno.

## 4.3 Matokeo ya shule ya Kimachia

**Jedwali 4.3.1: Frikwenzi ya makosa yaliyofanywa na wavulana**

| | **Nomino** | **Viwakilishi** | **Vivumishi** | **Vitenzi** | **Vielezi** | **Viunganishi** | **Vihusishi** | **Vihisishi** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mvu1 | 2 | 0 | 3 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 2 | 2 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 2 | 1 | 1 | 0 | |
| Mvu 4 | 0 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 5 | 2 | 0 | 3 | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | |
| Mvu 6 | 4 | 0 | 1 | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | |
| Mvu 7 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 8 | 5 | 1 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 9 | 4 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | |
| Mvu 10 | 9 | 0 | 1 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 11 | 2 | 0 | 2 | 5 | 2 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 12 | 3 | 1 | 1 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | |
| Mvu 13 | 3 | 0 | 3 | 3 | 2 | 0 | 3 | 0 | |
| Mvu 14 | 6 | 0 | 2 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | |
| Mvu 15 | 1 | 0 | 2 | 1 | 4 | 1 | 0 | 0 | |
| **Jumla ya makosa katika kila kategoria** | 48 | 3 | 24 | 52 | 12 | 3 | 7 | 0 | **Jumla ya makosa 149** |
| **Asilimia %** | 32.21 | 2.01 | 16.11 | 34.90 | 8.05 | 2.01 | 4.70 | 0 | |

Wanafunzi wavulana wa shule hii waliandikisha jumla ya makosa 149. Vitenzi vilidhihirisha frikwenzi ya juu ya asilimia 34.90% huku vikifuatwa kwa karibu na kategoria ya nomino kwa asilimia 32.21%. Vivumishi vilipokea 16.11%. Vihisishi havikuandikisha kosa lolote.

**Jedwali 4.3.2: Frikwenzi ya makosa yaliyofanywa na wasichana**

| | **Nomino** | **Viwakilishi** | **Vivumishi** | **Vitenzi** | **Vielezi** | **Viunganishi** | **Vihusishi** | **Vihisishi** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Msi1 | 2 | 0 | 2 | 7 | 1 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 2 | 0 | 0 | 1 | 6 | 2 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 3 | 1 | 0 | 2 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | |
| Msi 4 | 4 | 1 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 5 | 1 | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | |
| Msi 6 | 4 | 0 | 1 | 4 | 1 | 0 | 1 | 0 | |
| Msi 7 | 1 | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | |
| Msi 8 | 1 | 0 | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 0 | |
| Msi 9 | 1 | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 10 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 11 | 6 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 12 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | |
| Msi 13 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | |
| Msi 14 | 3 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | |
| Msi 15 | 2 | 0 | 1 | 5 | 1 | 0 | 1 | 1 | |
| **Jumla ya makosa katika kila kategoria** | 30 | 1 | 17 | 45 | 12 | 3 | 6 | 2 | **Jumla ya makosa 116** |
| **Asilimia %** | 25.86 | 0.86 | 14.66 | 38.79 | 10.34 | 2.59 | 5.17 | 1.72 | |

Jedwali hili linaonyesha kuwa wanafunzi wa kike walifanya jumla ya makosa 116. Kategoria ya vitenzi iliibuka kuwa na idadi ya juu ya makosa 45 ambayo ni asilimia 38.79%. Nomino zilifuata kwa asilimia 25.86%. Kategoria ya viwakilishi ilipokea frikwenzi ya chini ya asilimia chini ya moja. Kama ilivyokuwa katika shule ya Kaamu, kundi hili la wasichana liliandikisha kosa la kitenzi katika kila insha.

**Jedwali 4.3.3: Jumla ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi wa shule ya Kimachia**

| **Kategoria / Jinsia** | **Nomino** | **Viwakilishi** | **Vivumishi** | **Vitenzi** | **Vielezi** | **Viunganishi** | **Vihusishi** | **Vihisishi** | **Jumla ya makosa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wav | 48 | 3 | 24 | 52 | 12 | 3 | 7 | 0 | 149 | **56.23** |
| Was | 30 | 1 | 17 | 45 | 12 | 3 | 6 | 2 | 116 | **43.77** |
| Jumla | 78 | 4 | 41 | 97 | 24 | 6 | 13 | 2 | **265** | |
| % | 29.43 | 1.51 | 15.47 | **36.60** | 9.06 | 2.26 | 4.91 | 0.75 | | |

Jedwali hili linaonyesha jumla ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi wa shule ya Kimachia kwa pamoja. Jumla ya makosa 265 yaliandikishwa. Kati ya makosa haya, idadi 149 ilidhihirishwa na wavulana ambayo ni sawa na asilia 56.23% ya makosa yote nayo idadi ya 116 ikaandikishwa na wasichana ambayo ni asilimia 43.77%. Kategoria ya vitenzi iliendelea kuonyesha athari kubwa kama inavyothibishwa na frikwenzi yake ya asilimia 36.60% huku ikifuatwa na nomino kwa 29.43%. Vihisishi vilikuwa na frikwenzi ya chini zaidi ya 0.75%.

## 4.4 Hitimisho

Data yote ya shule hizi mbili ikijumuishwa pamoja, matokeo yake yanakuwa yafuatayo kama inavyoonyeshwa na jedwali hili.

**Jedwali 4.4: Jumla ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi wa shule mbili**

| Kategoria / Jinsia | Nomino | Viwakilishi | Vivumishi | Vitenzi | Vielezi | Viunganishi | Vihusishi | Vihisishi | Jumla ya makosa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wav | 80 | 4 | 48 | 154 | 22 | 4 | 16 | 1 | 329 | **53.67** |
| Was | 60 | 3 | 27 | 155 | 18 | 5 | 12 | 4 | 284 | **46.33** |
| Jumla | 140 | 7 | 75 | 309 | 40 | 9 | 28 | 5 | **613** | |
| % | 22.84 | 1.14 | 12.23 | **50.41** | 6.53 | 1.47 | 4.57 | 0.82 | | |

Wanafunzi wote 60 waliandikisha jumla ya makosa 613. Kati ya makosa haya, 329 yalifanywa na wanafunzi wavulana ambayo ni sawa na asilimia 53.67% ya makosa yote. Wanafunzi wa kike waliandikisha jumla ya makosa 284 ambayo ni sawa na asilimia 46.33% . Aidha, kategoria ya vitenzi ilijitokeza kuwa na frikwenzi ya juu zaidi ya 309 ambayo ni sawa na asilimia 50.41%. Kategoria ya nomino ilifuata kwa asilimia 22.84%, vivumishi 12.23%, Vielezi 6.53%, vihusishi 4.57%, viunganishi 1.47%, viwakilishi 1.14% navyo vihisishi 0.82%.

Kutokana na data hii ni wazi kuwa, wanafunzi wa kike walifanya vizuri zaidi wakilinganishwa na wenzao wa kiume kwani asilimia ya makosa waliyoandikisha ni ya chini (46.33% ) ikilinganishwa na ya wa kiume (53.67%). Matokeo haya yanathibitisha nadharia ya nne iliyodai kuwa, *zaidi ya asilimia 50% ya makosa itadhihirika katika kazi za wanafunzi wa kiume ikilinganishwa na wenzao wa kike.*Vilevile, imejitokeza kwamba, kategoria ya vitenzi ndiyo iliyo na frikwenzi ya juu zaidi ya utokeaji wa makosa ikilinganishwa na kategoria nyingine. Kategoria hii imedhihirisha asilimia 50.41%. Frikwenzi hii vilevile imethibitisha nadharia ya tatu iliyodai kwamba, *makosa mengi hujitokeza katika kategoria ya vitenzi kuliko kategoria nyingine.*

Jambo ambalo limejitokeza kutoka mwanzo wa uchanganuzi wa data ya sura hii ni kwamba, matokea haya hayabadiliki hata pale ambapo sampuli ni ndogo mathalani shule moja au kundi la wanafunzi 15 wa jinsia moja. Imeonekana kuwa, kategoria ya vitenzi ndiyo inayoongoza huku ikifuatiwa na nomino kisha vivumishi. Sababu kadha zinaweza kutolewa kuonyesha ni kwa nini kategoria ya vitenzi ndiyo inayoathiriwa zaidi. Kwanza, vitenzi vya Kiswahili kama vilivyo vya

Kitigania hubeba viambishi mbalimbali. Viambishi hivi huwa mofimu tegemezi ambazo huwasilisha uamili anuwahi mathalani: nafsi, ngeli, ukanushaji, njeo, urejeshi, yambwa, kauli na viishio. Kutokana na wingi wa viambishi hivi, ambavyo vingi vyavyo, licha ya kuwa na umbo sawa, huwakilisha dhana zaidi ya moja, frikwenzi ya makosa inatarajiwa kuwa kubwa ikilinganishwa na kategoria nyingine. Jambo lili hili linadhihirika kwa kiwango kidogo katika kategoria ya nomino ambayo pia hubeba viambishi lakini sio vingi kama ilivyo katika vitenzi. Kwa upande mwingine, vihisishi, vihusishi na viunganishi vilirekodi frikwenzi ya chini zaidi. Hali hii inaweza kuhusishwa na ushahidi kwamba aghalabu kategoria hizi huwa na mizizi huru. Vilevile, vitenzi ndivyo hubeba uarifu au habari kuu ya kishazi kwa hivyo kitenzi kinatarajiwa kuathirika zaidi kwani kitenzi kisichofaa kikitumiwa, uarifu potovu hutokea. Aidha, kwa mujibu wa Myers-Scotton (2005: 19), vitenzi ndivyo huzipa nomino majukumu ya kisemantiki/kithita. Nomino hizi zinaweza kuwa na majukumu ya mtenda, mfaidi, mwathiriwa, kitumizi, lengo, chanzo miongoni mwa majukumu mengine kama walivyofafanua (Fillmore 1968, Stowell 1981).

Pale ambapo jinsia mbili zinapojumuishwa, jinsia ya kiume ndiyo inayodhihirisha idadi kubwa ya makosa ikilinganishwa na ile ya kike. Hii ina maana kwamba wanafunzi wa kike hufanya vyema kuliko wanafunzi wa kiume. Wanaisimu wengi huamini kwamba, matumizi ya lugha hutegemea masuala ya kijamii na kitamaduni na jinsia haipewi uzito mkubwa. Hata hivyo, suala hili la jinsia limekuwa likiwashughulisha watafiti na walimu kwa muda. Kuna mitazamo na madai kadha ambayo yamezuliwa kueleza hali hii. Merritt, A (Makala katika gazeti la *The Telegraph* Januari 13, 2014) anaeleza mitazamo hii. Kwanza, kuna ule mtazamo unaodai kwamba wanawake na wanaume huzalisha lugha kwa namna tofauti bongoni zao. Sehemu za bongo za wanawake zinazohusika na usimbaji lugha huwa na uwezo mkubwa kuliko zile za wanaume. Sehemu hizi zinaweza kunakili mambo dhahania ya lugha lakini bongo za wanaume zitahitaji vichocheo vya kisensa kama vile, kutazama maandishi au kusikiliza kinachosemwa ili kuzalisha data ya lugha husika (Burman D. D. na wenzake 2008).

Pili, jinsia hizi hutumia mikakati tofauti katika kujifunza lugha. Kulingana na Rúa López (2006), wanawake hutumia mikakati anuwai ikilinganishwa na wanaume. Wanawake hutumia ujuzi zaidi kwa mfano, wanapoandika au wanapozungumza na vilevile kutumia vyema elementi za lugha kama vile msamiati na matamshi kuliko wanaume ambao hujikita tu na mikakati michache ya

kujifunza lugha. Mikakati hii ndiyo chanzo cha ufanisi unaoshuhudiwa katika jinsia ya kike kuwapiku wenzao wa kiume.

Tatu, jinsia ya kike huzungumza *(converse)* zaidi kuliko yenzao ya kiume. *Busuu (*eneo linalohusika na kujifunza lugha ana kwa ana mtandaoni), liliripoti kwamba wanawake wangewasiliana na wazungumzaji wazawa wa lugha lengwa mara nne zaidi kuliko wanaume. Huku kuwasiliana na wazawa lugha kunamwesha mtumiaji lugha kujenga ujuzi wake wa kusikiliza na kuzungumza, kuboresha matamshi, sarufi na msamiati miongoni mwa stadi nyingine za lugha.

Aidha, kwa mujibu wa jarida la Cananda la Isimu Tumikizi, wasichana huwa na motisha ya kujifunza lugha kuliko wavulana. Tafiti zilizofanywa Cananda, Uingereza na Hungari zote zilionyesha kwamba, wanafunzi wa kike wangeendelea na masomo yao kuhusu lugha ya pili/kigeni hata pale ambapo madarasa hayo hayakuwa ya lazima. Dai hili linalohusiana na motisha ni la mjadala. Baadhi ya madai kuhusiana na motisha ya jinsia ya kike ni kwamba: eneo la kujifunza lugha huchukuliwa kama eneo la jinsia ya kike. Pia, kwa kuwa walimu wengi wa lugha ni wanawake basi wanafunzi wa kike hupata ilhamu ya kujifunza lugha kwa kujinasibisha na walimu hawa kama vielelezo bora.

# SURA YA TANO

# MIKAKATI YA KUKABILI MAKOSA

## 5.1 Utangulizi

Sehemu hii inalenga kupendekeza baadhi ya mikakati ambayo inaweza kutumiwa kupunguza makosa ambayo tayari yameshaainishwa katika sura ya tatu na nne ambapo tumeshaona kwamba wanafunzi hufanya makosa ya kifonolojia na kimofolojia. Katika sura ya nne, imedhihirika kwamba wanafunzi wa kiume huathirika zaidi ikilinganishwa na wenzao wa kike. Nayo kategoria ya vitenzi ikaandikisha frikwenzi kubwa ya makosa ikilinganishwa na kategoria zenzake. Aghalabu mikakati hii itahusu ile ambayo tayari imependekezwa na wataalam mbalimbali pamoja na ile ambayo tunahisi kwamba inafaa kwa mujibu wa eneo ulimokitwa utafiti huu. Baadhi ya mikakati inawalenga walimu moja kwa moja kwa kuwa wao ndio huchukuliwa kuwa kiungo muhimu katika ujifunzaji wa L2 Hedge (2000, 288). Aidha mikakati mingine inalenga wanafunzi pamoja na watayarishaji mitaala.

## 5.2 Jinsia na ufundishwaji lugha

Katika sura ya nne, ilibainika kwamba utokeaji wa makosa huathiriwa na jinsia maadam wanafunzi wa kiume walifanya makosa mengi wakilinganishwa na wenzao wa kike. Hali hii imekuwa ikiibua mijadala ambayo sio lengo letu kuizamia walakini tutataja machache tu ili yawe msingi wa pendekezo la mbinu za kushughulikia jinsia hizi. Baadhi ya maoni yanayotolewa ni kuwa, wanabayolojia wamethibitisha, watoto wa kike huzaliwa na uwezo mkubwa wa kujifunza na kutumia lugha ikilinganishwa na wenzao. Inadaiwa, sehemu ya ubongo ya watoto wa kike inayodhibiti lugha hukomaa mapema ikilinganishwa na ile ya watoto wa kiume. Halpern (2006). Hata hivyo, tafiti zilizofanya na Tella, Indoshi na Othuon (2010) katika somo la Kiingereza nchini Kenya, zilionyesha wanafunzi wa jinsia zote wakikaribiana mno kimatokeo. Katika uchunguzi wa matokeo ya Kiswahili, Kang'ahi M. na Wenzake, waligundua kuwa wanafunzi wote wa kidato cha nne walifanya sawa katika Kiswahili, wasichana wakiwa na jumna ya alama ya wastani ya 4.12 nao wa kiume wakipata 4.10. Matokeo ya jinsi hii yanaonyesha kwamba licha ya tofauti za kimaumbile, kuna haja ya kuwapa wanafunzi wote nafasi sawa wakati wa masomo na vilevile kuwamotisha wote huku walio na matatizo zaidi wakitengewa muda zaidi kuweza kuwapa msaada wa kielimu. Aidha, kulingana na Burman D. D. na wenzake (2008) ubongo wa

jinsia ya kiume huhitaji vichocheo vya kisensa ili kusimba masuala dhahania ya lugha, hivyo basi walimu na watayarisha wanafaa kutumia vifaa anuwai vya kufundisha ili kuwafaa wanafunzi wavulana.

### 5.3 Baadhi ya mbinu za kupunguza makosa

Kumekuwapo na mjadala kuhusiana na mkakati ambao ndio bora zaidi kukabiliana na makosa yanayojitokeza katika ujifunzaji wa L2. Kila mkakati unaopendekezwa unaibuka kuwa na udhaifu kiasi kwamba wataalamu wanapendekeza matumizi ya mikakati mseto au mkakati zaidi ya mmoja. Hali hii ya udhaifu, ndiyo iliyopelekea kuwepo kwa nadharia mbalimbali za kujifunza lugha kwani nadharia za awali zilikemewa kwa kutojitosheleza. Aidha, kuna suala la ikiwa mkakati mmoja unaweza kutumika kuyakabili makosa yote yawe ni yale ya kiusemi au ya kuandikwa. Vilevile, suala jingine linatokana na nafasi ya mwalimu katika kumwelekeza mwanafunzi au ni mwanafunzi anafaa kujisahihisha mwenyewe baada ya kupata vichocheo fulani kutoka kwa mwalimu. Masuala mengine ni pamoja na muda mwafaka wa kumkosoa mwanafunzi, mahali pa kumkosolea, aina ya kosa linalofaa kukosolewa na jinsi ya kulikosoa.

Kuhusiana na ukosoaji wa makosa andishi au kiusemi, Sheen (2007) anapendekeza ukosoaji au usahihishaji wa kilengo (*focused corrective feedback*) ambapo mwalimu hulenga aina moja ya kosa badala ya kushughulikia aina zote za makosa katika mkumbo mmoja. Mbinu hii ina manufaa yake kwani huwafanya wanafunzi kumakinika zaidi, kutambua kosa husika na hata kuweza kufanya ulinganishaji kwa sababu dhana huwawia wazi zaidi inapokuwa mahususi. Makosa ya aina nyingi yanaposhughulikiwa kwa pamoja, huzua utata na wakati mwingine wanafunzi kukosa kuunganisha na kuhusisha kwa pamoja anachofanya mwalimu. Kwa mfano, mwalimu anaweza kufunza kuhusiana na aina ya kosa la udondoshaji wa fonimu /h/ kama lilivyobainishwa katika sura ya tatu badala ya kushughulikia aina zote. Mbinu hii pia itafaa zaidi katika nyakati ambapo walimu hujikuta wakiwa na idadi kubwa sana ya wanafunzi. Pawlak (2014, 106-107) ) anapendekeza kwamba mwalimu achague makosa yale tu anaona ndiyo yanayojitokeza zaidi miongoni mwa wanafunzi pamoja na yale ambayo yanatishia kukwamiza mawasiliano kisha ayashughulikie.

Ilibainishwa kuwa L1ndicho chanzo kikuu cha makosa katika Lugha-Kati. Wanafunzi walihamisha mifumo ya L1 hadi Lugha-Kati. Wardhaugh (1970) anapendekeza walimu watilie

maanani faridi ambazo ni tofauti katika L2 na L1. Maoni haya yanashabihiana sana ya yale ya wananadharia Uchanganuzi Linganuzi mathalani, (Stockwell na wenzake 1968, Stockwell na Bowen 1965) ambao wanaona kuwa miundo ya L1 na L2 inafaa kulinganishwa kwa lengo la kutambua vipengele ambavyo vitamwia mwanafunzi ugumu. Wanaona kwamba, lugha ikiwa na miundo sawa itakuwa rahisi kujifunza ilhali mwanafunzi atatatizika katika zile sehemu ambazo zinahusu miundo tofauti. Kwa hivyo miundo hii tofauti inafaa kutiliwa maanani zaidi katika ufunzaji wa lugha. Wataalamu hawa hata wanapendekeza ujifunzaji wa L2 kwa kutumia "ngazi za ugumu wa makosa "*hierarchies of difficulty.* Ingawa nadharia hii ilipingwa sana, (König na Gast 2009) wanadai kuwa ulinganishaji huu wa miundo unaweza kuwafaa sana wanafunzi wenye kiwango kikubwa cha ufahamu wa L2. Corder (1967) naye anaona kwamba makosa ambayo yanafaa kukosolewa na mwalimu ni yale tu makosa ambayo mwanafunzi hawezi kujikosoa mwenyewe *(errors)* wala sio makosa ambayo anaweza kujikosoa *(mistakes).* Maoni ya Corder yana udhaifu mkubwa kwani ni vigumu kutambua makosa ambayo mwanafunzi anaweza kujisahihisha au kutojisahihisha mwenyewe hususan ikizingatiwa kwamba wanafunzi wanakuwa na uwezo tofauti tofauti na hata vigezo ambavyo vinaweza kutumiwa kutathimini aina hizi mbili za makosa. Kimsingi, tunachopendekeza ni kwamba itakuwa bora ikiwa walimu watafundisha kwa kina mfumo wa sauti wa Kiswahili huku wakitilia mkazo zaidi zile sauti ambazo hazipatikani katika L1 na hata kuwasaidia wanafunzi kutambua ukweli huu ili kuzuia tabia ya kuhamisha vipengele vya L1 katika L2 kivoloya.

Kuhusiana na muda wa kutoa majibu ya ukosoaji, tunapendekeza mikakati mitatu kama ilivyofafanuliwa na Allwright na Bailey (1991, uk.103). Mbinu hizi tatu zitategemea masiala mbalimbali mathalani: aina ya kosa, hali ya wanafunzi na mwalimu. Hii ina maana kwamba, baadhi ya mikakati itafaa wakati wa mazungumzo na mingine itafaa kwenye mazungumzo na kazi andishi. Kwanza, majibu yanaweza kuwa ya papo kwa papo (*immediate*), yakacheleshwa (*delayed*) au yakaahirishwa (*postponed*). Ukosoaji wa papo kwa papo husaidia mwanafunzi kufahamu kosa lake na kulirekebisha. Hata hivyo mbinu hii inapingwa na wanaelimu kama vile (Edge 1989, Ur 1996 na Harmer 2007). Seedhouse (2004), anaona kuwa mbinu hii haifai darasani kutokana na athari ya kumwondoa mwanafunzi katika kiini cha mada yake na pia kusababisha fedheha. Pili, mwalimu anaweza kusubiri hadi mwanafunzi kuwasilisha kazi yake au nafasi ya ukosoaji inapojitokeza bila kumtatiza mwanafunzi. Tatu, mwalimu anaweza kuwa

kama mtazamaji tu ambapo ataandika makosa yanayofanywa na wanafunzi kisha ayajadili baaada ya somo au hadi somo lifuatalo. Mbinu hii ndiyo inayopendelewa na wataalam wengi kama vile (Edge 1989; Bartram na Walton 1991, Basturkmen na Wenzake 2004). Hata hivyo iwapo kosa litaahirishwa hadi siku nyingine kuna hatari ya wanafunzi kutokumbuka kama walilifanya ikiwa lilitokea katika mazungumzo.

Walimu wanaposahihisha insha za wanafunzi, tunapendekeza watumie mbinu mojawapo ya hizi mbili kutegemea viwango vya ufahamu na uwezo wa wanafunzi wao. Kwanza, kuna mbinu ya kutoa majibu moja kwa moja na ya pili ni ile ya kutumia alama au ishara mbalimbali kuashiria kwamba kosa limetelelezwa. Katika mbinu ya kutoa majibu moja kwa moja (*direct correction feedback*) kwa mujibu wa Sheen na Ellis (2011, uk. 593), mwalimu hupigia mstari neno lenye kosa au sauti kisha huandika umbo au sauti sahihi karibu na neno hilo. Kwa mfano, mwanafunzi aliyeandika **siba*, mwalimu akalikata na kuandika *shiba* badala yake. Mbinu hii humfaa mwanafunzi kwani anaweza kutambua papo hapo kosa lake na kuweza kulirekebisha. Pia, humpunguzia muda wa kwenda kusaka umbo sahihi. Katika mbinu ya pili *(indirect correction feedback*), mwalimu hutumia hutumia alama/ishara mbalimbali kuonyesha kuwa kosa limefanywa bila kuandika umbo sahihi. Ishara hizi zinaweza kuwa zile zimependekezwa na taasisi husika au zikawa za kubuni. Kwa mfano, pale ambapo mwanafunzi amedondoa fonimu ishara ya kutoa (-) inaweza kutumiwa, ikiwa ni kosa na kuchopeka, ishara ya kujumlisha (+) inaweza kutumiwa na kadhalika. Mbinu hii ya kutumia alama humpa mwanafunzi changamoto ya kufikiria kosa na kuweza kulirekebisha mwenyewe Harmer (2004, uk. 111). Hata hivyo, wanafunzi wanafaa kufundishwa kuhusiana na maana ya matumizi ya ishara husika. Udhaifu wa mbinu hii ni kwamba, huenda ikasababisha utata pale ambapo mwanafunzi hushindwa kumaizi lengo la mwalimu. Wanafunzi wengine hata huenda wasifanye juhudi za kufikiria au kusaka umbo sahihi kwa mfano katika kamusi.

Mkakati mwingine ni ule unaojulikana kama vikao vya uandishi (*writing conferences)* (Goldstein na Conrad 1990, Ferris 2002, Williams 2004). Katika vikao hivi wanafunzi hupata fursa ya kuonana ana kwa ana na mwalimu wao. Nafasi hii, huwawezesha kuuliza maswali kuhusiana na makosa waliyoyafanya pamoja na maoni yaliyoandikwa na mwalimu katika insha zao. Mwalimu anaweza kuwa aliashiria kosa kwa kutumia alama fulani au awe aliandika umbo

ambalo wanafunzi wangetaka ufafanuzi zaidi. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kuwa aliandika *waling'orota* badala ya *walikorota* na akawa bado haoni tofauti. Katika hali kama hii ataweza kusaidiwa kwa upesi. Hali kadhalika, mwalimu anaweza kutoa visawe na miktadha mingine kadha wa kadha ya matumizi ya maneno husika. Mbinu hii inachukuliwa kuwa mojawapo ya zile zilizo bora Bitchener na Wenzake (2005, uk. 194). Tatizo la mbimu hii ni kwamba inahitaji muda mwingi na pia idadi chache ya wanafunzi. Kwa hivyo, wizara ya elimu inafaa kuhakikisha kuwa walimu wa lugha ya Kiswahili wanatosha ili kuwapa wanafunzi wote nafasi ya kupata msaada kutoka kwa mwalimu ikiwa wizara inatarajia mbinu hii kutumika.

Makosa mengine ya wanafunzi hutokana na urithishwaji wake kutoka kwa walimu. Hali hii hutokana na ukweli kwamba wengi wao sio wazungumzaji wazawa wa lugha lengwa. Madai haya yanathibitishwa na Allwright na Bailey (1991) wanaposema:

> Walimu ambao sio wazungumzaji wazawa wa lugha lengwa inatarajiwa wawe na tatizo la kipekee katika uwezo wao wa kutambua makosa ya wanafunzi. Wanaweza hata kushuku nafasi zao katika mwendelezo wa Lugha-Kati. Walimu wasio wazawa wa lugha hawawezi kutarajiwa kusahihisha makosa ambayo hawawezi kutambua uk. 100–101 (Tafsiri yetu)

Kwa mantiki hii basi, tatizo hili linaweza kupunguzwa ikiwa walimu wataendelea kupata mafunzo ya mara kwa mara. Hata inapowezekana, wanaweza kutangamana na wazungumzaji wazawa kwa lengo la kuimarisha umilisi wao.

Iwapo mwalimu amekuwa akifundisha sheria au kipengele fulani kwa muda au hadi katika kiwango fulani, wataalam wanapendekeza mkakati wa kumfanya mwanafunzi afahamu kuwa kosa limetendeka badala ya kutoa jibu la kosa husika (Komorowska 2003 na Harmer 2007). Mantiki iliyomo katika mbinu hii ni kwamba, mwanafunzi anakuwa na uwezo wa kurekebisha kosa lile mwenyewe na hivyo kurahisisha ujifunzaji wa L2. Ili kufikia shabaha hii, mikakati ifuatayo inapendekezwa:

i) Kumwuliza mwanafunzi arudie kauli yake. Kwa mfano, mwanafunzi akitamka, "*Mbasi ilianguka." Mwalimu anaweza kurai, "Samahani? Rudia tena?". Hapa, swali huulizwa kwa kusisitiza kiimbo.

ii) Kuuliza swali kwa namna ambayo jibu litakalotolewa litagusia faridi y(z)enye makosa. Kwa mfano,

Mwanafunzi: *Tulichoma vitabu kwa bidii.

Mwalimu: Ati mlifanya nini kwa bidii?

iii) Kujitia kutoelewa kauli yenye kosa.

Mwanafunzi: * Wazazi walienda msituni.

Mwalimu: Ajabu! Kwani wazazi wanaishi msituni?

iv) Kurudia kauli ya mwanafunzi walakini kwa kutilia mkazo zaidi sehemu yenye makosa kwa kiimbo chenye kuibua shaka. Kwa mfano,

Mwanafunzi: * Baba ni tajiri, hana mali nyingi sana.

Mwalimu: Baba ni tajiri, HANA mali nyingi sana.

v) Kurudia kauli hadi sehemu au neno la mwisho ambalo ni sahihi kwa namna ya kusita na kuinua kiimbo. Kwa mfano:

Mwanafunzi: * Hamisi aliaga dunia kwa kunywa sigara kupindukia.

Mwalimu: Hamisi aliaga dunia kwa…

Mbinu hii humfanya mwalimu kuonyesha mahali lilipo kosa kwa njia isiyo ya kukera.

vi) Kauli na swali ambapo mwalimu huamua kutoa kauli inayoonyesha kwamba kosa la kiisimu limetokea mathalani, "Umejaribu sana, lakini kuna kosa dogo umefanya." Anaweza pia kutumia mbinu ya swali. Kwa mfano, "Una uhakika kwamba hivyo ndivyo hilo neno hutamkwa?"

Kwa kutamatisha sehemu hii, Krashen (1982) anapendekeza mkakati wa ruwaza radidi (*pattern drills).* Mbinu hii huhusu urudiaji au ufanyiaji mazoezi muundo wa kiisimu ambapo mwanafunzi huiga mwalimu. Katika hali hii, mwanafunzi hurudia kwa mfano matamshi ya neno fulani kama anavyolitamka mwalimu huku akijaribu kufikia au kukaribia matamshi yake (mwalimu). Kwa hivyo matamshi ya mwalimu huwa kichocheo *(stimulus)* nayo matamshi ya mwanafunzi huwa majibu *(response).*

Mwalimu: sababisha

Mwanafunzi: sababisa

Mwalimu: sababisha

Mwanafunzi: sababisha

## SURA YA SITA

## HITIMISHO

### 6.1 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kuchanganua na kubainisha makosa ya kifonolojia na kimofolojia yanayojitokeza katika kazi andishi za wanafunzi wa shule za upili za Tigania jimboni Meru. Nadharia ya Lugha-Kati ilitumika kuongoza utafiti huu nayo data ikakusanywa kupitia uandishi wa insha.Shule za Kaamu na Kimachia zilitumika ambapo wanafunzi thelathini kutoka kila shule walitumika kama sampuli ya utafiti. Kazi hii tumeigawa katika sura sita. Sura ya kwanza ni muhtasari wa jinsi utafiti ulivyofanywa, katika sura ya pili, tumeainisha na kueleza fonimu na silabi za Kiswahili Sanifu na za Kitigania.Sura ya tatu imehusu uchanganuzi wa makosa ya kifonolojia na kimofolojia. Sura ya nne imemulika jinsia inayoathiriwa zaidi na makosa na vilevile tukadhihirisha kategoria ya maneno inayoonyesha frikwenzi kubwa ya makosa. Katika sura ya tano, tumependekeza mikakati inayoweza kutumiwa kukabiliana na makosa yaliyodhihirishwa. Katika sura ya sita, tumetoa muhtasari na matokeo ya utafiti huu pamoja na kupendekeza sehemu zinazoweza kutafitiwa baadaye.

### 6.2 Matokeo ya utafiti

Matokeo ya uchunguzi huu yamedhihirisha kwamba aina mbalimbali za makosa hujitokeza kwenye insha za wanafunzi. Baadhi ya makosa haya ni pamoja na yale ya unazalishaji wa fonimu, udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa irabu na utumiaji wa sauti mbadala. Pia kuna makosa yaliyotokana na uambishaji na unyambuaji pamoja na mlandano wa kiumbo. Chanzo kikuu cha makosa cha makosa haya kilibainishwa kuwa athari ya lugha ya kwanza kwa kujizolea frikwezi ya asilia 60%. Vyanzo vingine yaani: ujumlishaji mno, mikakati ya mawasiliano, mikakati ya kujifunza L2 na uhawilishaji wa ufundishwaji viliandikisha asilimia 40% iliyosalia. Matokeo haya yalithibitisha nadharia tete za kwanza mbili.

Aidha, kategoria ya vitenzi imejitokeza kama kategoria inayoathiriwa zaidi na makosa ya kifonolojia na kimofolojia  kwa kuandikisha frikwenzi ya juu zaidi ya 309 kwa 613 ya jumla ya makosa ambayo ni sawa na asilimia 50.41%. Kategoria ya nomino ilifuata kwa asilimia 22.84%,

vivumishi 12.23%, Vielezi 6.53%, vihusishi 4.57%, viunganishi 1.47%, viwakilishi 1.14% navyo vihisishi 0.82%. Matokeo ya data hii vilevile yalithibitisha nadharia tete ya tatu kuwa ya kweli.

Kuhusiana na jinsia, uchunguzi huu umeonyesha kwamba jinsia ya kike hudhihirisha idadi chache ya makosa kuliko ile ya kiume. Wanafunzi wa kiume wameandikisha asilimia 53.67% ya makosa yote nayo ile ya kike ikifuata kwa asilimia 46.33%. Nadharia tete ya nne iliyodai kuwa, *zaidi ya asilimia 50% ya makosa itadhihirika katika kazi za wanafunzi wa kiume ikilinganishwa na wenzao wa kike* imethibitishwa maadam jinsia ya kiume imeandikisha asilimia zaidi ya 50% (53.67% ) ya makosa.

Isitoshe, utafiti huu umependekeza mikakati na mbinu anuai ambazo zinaweza kutumiwa na wanaohusika kuweza kukabili makosa haya. Tumedhihirisha namna kila mbinu inavyoweza kutumika kukabiliana na baadhi ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi. Hata hivyo, ni muhali kudai kwamba kuna mbinu bora kuliko nyingine kwa sababu kila mojawapo ina manufaa na udhaifu wake. Tunapendekeza washika dau kutathimini mkakati unaofaa katika muktadha husika. Mbinu hizi pia hazifai kutumika katika upeke wake bali walimu wanaweza kuhusisha mikakati kadha.

Uchunguzi huu uliongozwa na nadharia ya Lugha-Kati ya Selinker (1972). Bila ya shaka nadharia hii imeweza kuwa dira kwa kutolea utafiti huu mwanga. Imejitokeza kuwa nadharia inayofaa kuchunguza makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha lengwa huku L1 ikiwa lugha yao ya kwanza/ asilia (mama). Ufaafu huu unatokana hususan na mtazamo wake usioegemea upande mmoja kama ile nadharia ya awali ya Uchanganuzi Linganuzi. Tumeona kuwa kuna visababishi vingi vinavyochangia kuwepo kwa makosa wala sio tu lugha ya kwanza. Isitoshe, aina mbalimbali za makosa yaliyobainishwa katika sura ya tatu yanaweza kuelezwa kama juhudi za wanafunzi za kujifundisha lugha lengwa kwa hivyo wanaishia kuunda na Lugha-Kati yao yenye mfumo wake; mfumo ambao si wa Gitigania wala Kiswahili Sanifu. Vilevile, makosa haya ni idhibati ya kutosha kwamba wanafunzi hawa hawajafikia umilisi wa lugha ya Kiswahili Sanifu. Hii ina maana kwamba wamekwama mahali au wako katika hatua fulani katika kile ambacho Shameen T. (1992) alichokiita Mwendeleo wa Lugha-Kati (*Interlanguage Continuum*). Mikakati iliyotolewa ni ya kuwasaidia wanafunzi kufikia umilisi wa lugha lengwa ambayo ni Kiswahili Sanifu.

Kando na ufaafu wa nadharia hii pamoja na sifa chanya ambazo wataalam wameimiminia, kuna udhaifu na changamoto ambazo tumeona zinahusishwa na nadharia hii na itakuwa kuitendea haki taaluma hii tukizitaja. Kwanza, mifanyiko ya kiisimunafsia inayopendekezwa kuwa chanzo cha uyabisi ni ya kidhahania mno hivi kwamba inakuwa muhali kuiashiria moja kwa moja. Kwa mfano, mojawapo ya visababishi vya makosa inachukuliwa kuwa ufundishwaji usiofaa. Inakuwa vigumu kuweka mipaka wazi baina ya chanzo kimoja na kingine. Ugumu huu unatokana na ukweli kuwa masuala ya ujifunzaji lugha hutokea ubongoni na ni vigumu kwa binadamu kuingia ubongoni kwenda kuchunguza michakato inayohusiana na lugha. Kutokana na hili tunasalia tu kutegemea tabia za wajifunza lugha yaani data ya nje ikiwa ni pamoja na tunachokisia na kukiona kutoka kwao. Hata suala ya kukadiria hatua mbalimbali za kujifunza lugha lengwa linazua ugumu wake. Ugumu huu unatokana na ukweli kuwa itabidi tumfuate mjifunzaji lugha tangu pale anapoanza kujifunza lugha huku tukirekodi hatua mbalimbali anazofanya katika hatua mbalimbali za ujifundishaji. Suala jingine la kidhahania ni lile la kupima umilisi hususan ikizingatiwa kuwa umilisi hauna dosari. Kwa hivyo inakuwa vigumu kuweza kubaini ni lini ambapo mwanafunzi amefikia umilisi kamili wa lugha lengwa na vipimo vipi vinafaa kutumika. Hata hivyo, manufaa na umuhimu wa nadharia hii unazidi udhaifu wake kwa hivyo tunatoa changamoto kwa wataalamu kuzua mbinu zaidi za kuboresha nadharia hii au hata kujaribu kubuni nadharia itakayokuwa na nguvu zaidi kuzidi hii ya Selinker.

### 6.3 Mapendekezo

Kwa kuwa utafiti huu haukushughulikia matatizo yote yanayokumba wanafunzi wa Tigania wanaojifunza lugha ya Kiswahili, tunapendekeza sehemu zifuatazo kushughulikiwa na tafiti zingine. Kwanza, makosa ya vipengele vingine vya kiisimu kando na fonolojia na mofolojia yaachunguzwe. Pili, mbinu zaidi ya moja za kukusanya data zihuzishwe katika tafiti za usoni; matokeo yatakayotokana na mbinu hizo yanaweza kutumiwa kulinganisha matokeo ya utafiti huu uliotumia mbinu moja. Tatu, sampuli za wanafunzi kutoka viwango tofauti tofauti zitumike kwa nia ya kulinganisha hatua za kujifunza lugha zao lengwa. Hali kadhalika, tafiti za jinsi hii zifanywe katika majimbo mbalimbali yenye L1 tofauti kwa minajili ya kulinganisha matokeo haya na hata kubaini ikiwa matokeo ya jinsi hii yana ubia wowote kwa kila anayejifunza lugha ya pili.

## MAREJELEO


Baljit, B. (1999). "Native Language Interference in Learning a Second Language: Exploratory Case Studies of Native Language Interference with Target Language Usage."*International Education Journal*, Vol. 1(1): 22-31.

Myers-Scotton, C. (2005) Uniform Structure: Looking Beyond the Surface in Explaining Codeswitching. *International Journal of Bilingualism.*

Chepkwony J. G. (1993). *Makosa Yanayofanywa na Baadhi ya Wanandi Katika Matumizi ya Kiswahili.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Corder, S.P. (1967). *Error Analysis and Interlanguage*, Oxford: Oxford University Press.

_________(1981). *Error Analysis*, London: Longman.

Gacunku, L. (2005). *A Phonological Investigation on Irregularity and Variation in the Kimeru Nominal Concordial System.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Gass & L. Selinker (Eds.), *Language transfer in language learning* (pp. 197-216). Amsterdam: John Benjamins.

Gesare, (1992) *Mofolojia ya Lugha ya Ekegusii*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Guthrie, M. (1948) *Classification of Bantu Languages.* Oxford. Oxford University press.

Habwe, J. H. na P. Karanja (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers

Iribemwangi, P. (2010) *The Structure of Kiswahili Sounds, Sound changes and Words*. Saarbruken: Verlag

Kang'ahi na wenzake (2012) Gender and Students' Academic Achievement in Kiswahili

Language. *Journal of Emerging Trends in Educational Research and Policy Studies* (JETERAPS) 3(5): 716-720.

Katamba, F. (1992) *An Introduction to Phonology*. Longman: London

Kimaro, H. (2013 March 21) *Why Kiswahili Performance is Sliding*. Daily Nation. Retrieved from http://www.nation.co.ke

Kisakwah B. A. (2014) Uchanganuzi *Makosa na Muundo Sentensi: Ulinganisho wa Sentensi Sahili za Kiswahili Sanifu na za Kisuba*. Tasnifu ya Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Lado, R. (1957): *Linguistics Across Cultures*. Ann Arbor: University of Michigan Press

Macharia, M. (2013). "The Phonological Basis of Misspellings in the Written english of Kikuyu Speakers"**.** *Journal of Language, Technology & Entrepreneurship in Africa,* Vol. 4(2)

Mangwa, D.O (2005), *Athari za Ekegusi Katika Kiswahili na Zinazochangia Matokeo Mabaya ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili kwa Wanafunzi wa Kisii Wilayani Kisii Kusini*. Tasnifu ya uzamili (haijachapishwa) Chuo kikuu cha Egerton.

Marete, G. (1981) The Grammatical Agreement in Kimeru Syntax. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Merritt, A. (2014, January 13) *Are Women Really Better at Learning Languages?* The Telegraph. Retrieved from http://www.telegraph.co.uk

Mgullu, R.S (2001) *Mtalaa Wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*.

Musa (2008*).Athari za Lugha ya Kigweno Katika Kikiswahili na Jinsi Zinavyoathiri MatokeoMabaya ya Mtihani wa Kitaifa*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Islamic Mbale, Uganda.

Mudhune (1994). *Matatizo ya Kimofosintaksia Yalinayowakumba Wanafunzi Katika Jamii ya Waluo Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili*.*Tasnifu ya Uzamili* (isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Islamic, Uganda.

Ng'ang'a (2002). *Makosa ya Kisarufi Katika Insha za Wanafunzi na Jinsi Yanavyoshughulikiwa na Walimu Katika Tarafa ya Ndaragwa*.Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.

Obara J. M. (2014) *Uchanganuzi wa Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii*. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.

Orengo P., & Opiyo P. (2011 December 29) Sheng Affecting English, Kiswahili Performance. Standard Digital. Retrieved from http://www.standardmedia.co.ke

Otiende, M. A. *(*2013) *Athari za Mofofonolojia ya Kibasuba katika Matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya Pili.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Polome, E. (1967) Swahili *Language Handbook*. Washington: Centre for Applied Linguistics.

Rapando, M. M. (2005) *Makosa ya Kimofosintaksia Yanayojitokeza katika Kazi za Kiswahili ilizoandikwa na Wanafunzi wa Shule za Upili Jijini Nairobi*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Richards, J. (1974). Analysis: Perspective on second language acquisition. In J. C. Richards (Eds.), *A Non-contrastive Approach to Error Analysis* (pp. 172-188). London: Longman.

Richards, J. C., Plott, J., & Platt, H. (1996). *Dictionary of Language Teaching and Applied Linguistics*. London: Longman.

Rúa López (2006) The Sex Variable in Foreign Language Learning: An integrative Approach. *Porta Linguarum (*6): 99-114

Selinker, L. (1969). *Language Transfer, General Linguistics*. New York: Rawlence Eribaum Associates, inc. (RAL).

___________ (1972) *Interlanguage*. New York: Rawlence Eribaum Associates, inc. (RAL).

Selinker, L. (1972). Interlanguage. *International Review of Applied Linguistics in Language Teaching, 10*(3), 219-231.

Selinker, L. (1974). Error analysis: Source, cause, and significance. In J. C. Richards (Eds.), *Error analysis: Perspective on second language acquisition.* London: Longman.

Tarone, E. (1988). *Variation in Interlanguage*. London: Edward Arnold.

Tarone, E. (1990). On variation in interlanguage: A response to Gregg. *Applied Linguistics, 11*(4), 392-400.

Tarone, E. (2001). Interlanguage. In R. Mesthrie (Eds.), *Concise encyclopedia of sociolinguistics* (pp. 475- 81). Oxford: Elsevier.


Wa Mberia, K. (1981) *The Consonants of Kitharaka*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

https://www.aclacaal.org/Revue/vol-9-no1-art-kissau.pdf/

https://www.blog.busuu.com/are-women-better-language-learners/

https://www.researchgate.net/publication/229021477/

**KIAMBATISHO I**


AJALI YA AJABU NILIYOSHUHUDIA

**KIAMBATISHO II**

AJALI YA AJABU NILIYOSHUHUDIA

Ilikuwa ni siku ya Ijumaa ambapo niliamka nikiwa nimechangamka na kukaramkia shabiki kibogoyo aliye ota magego na shagego angalau yakutafunia ubwabwa apo ndipo majira ya asubuhi yalibisha hodi nalo jua likatapanya miale ya macho ya upea nilikoga kwa maji fufutende na kuvaa mavazi haliahalia na kuenda shabuleni. Nilitoka nyumba kwa mwendo wa aste aste huku moyo ukinindunda ndwindu ndu na wasiwasi zi haba

Wakati niliwadia kufika njiani pikipiki ilitokea papo hapo nilimwaaisha kunipeleka mpini iii kuchukua gari ya kunipeleka Nairobi pale nilipokuwa nikienda hapo ndipo niliamini kuwa mkikanga na nyakanguzi hawakutubisha joho linalotubwagabwaga kwa kiburuyo cha kuguaya walipo neno kuwa siku moaya huanza asubuhi kwa yule niliyo stuwia kwa takribani muda wa dakika kumi gari nililiitokea kwa mwendo wa haraka ambalo lilikuwa na dereva aliyekuwa mlevi yule niliyo yaona nilikoza kuamini macho yangu kwani nilistuka na kubaki kinywa wazi ajali iiitokea baina ya ile gari na ingine kutoka upande wa kulia. yaligongana papo hapo machoni umwangu mayirani kutoka pande zote walizuhudia iya hayali kwani hawakuwa na lingine la kufanya ila kuwahudumia waliomo kwa lako magari. bila shaka wawili waliweza kukufia hapo hapo na wengine kuwa na majeraha mengi mwilini wengi wao hawangeweza hata kutembea wala kuchungumza.

Gari la kuwahudumia wagonjwa lilifika kwa haraka lakini maji yakimwagika

## KIAMBATISHO III

AJALI YA AJABU NILIYOSHUHUDIA.

Ilikuwa ni Jumamosi moja tarehe 20/02/2016 ambapo
nilikuwa pilapila zangu kuelekea shuleni asubuhi
na mapema kama kawaida. Nilipofika karibu na kilango
kikuu cha shule (gate) Niliona gari mbili zikiwa
zinakulana moja ikigonga ingine zote zikaanguka
hapo papo ambapo palikuwa na miima zilibingirika
bingiringi kuelekea upande wa chini.
Watu walioga dunia na wengine kupelekwa
hospitalini kwa matibabu ya daktari na waliokufa
kupelekwa katika chumba cha maitimaiti walilaa
hapo kuja kuona ni nini kinaendelea. Ilikuwa inaone
kana kama miujiza kwa sababu akna mtu aliua
hiyo ajali ikikuwa imesababishwa na nini kwa
sababu waliona magari yakiwa yana ki[illegible]
kugongana.
Walipofuatiliwa na wana sayansi na asker[illegible]
nini ilikuwa na shida kulionekana kil[illegible]
ilikuwa kwa upande wake lakini akna [illegible]
shida imetokea wapi! Ndipo waligundua ni mauni
yako hapo kwa sababu aja siku nyingine pikipiki
zilikutania hapo papo na kuja kuanguka zote
zikaanza kutaliam na akna mtu aliyeumia ala
mmoja au pikipiki [illegible] ikiharibika. Wote walam
ka wakajipanguza na kuendelea safari yao.
Siku moja wanakijiji wote waliungana na kuenda
a kwa Polisi na kuripoti hayo mambo lakini polisi
walikosa la kufanya. Waliambiwa waende wakamwo
te Padri au kasisi ambaye wanajua ni muombaji
hodari ili akuje atatue hayo mambo.
Walikamatana wote mpaka kwa Padri ambaye
alikuwa wa kijiji ambaye alikuwa amebandika namba
ri yake ya simu kwa kila barabara walipofika

scan 3.jpg
Type: JPG File
Size: 738 KB
Dimension: 1700
pixels

## KIAMBATISHO IV

AJALI YA AJABU NILIYOISHUHUDIA.

Kwa kweli ajali haina kinga. nakumbuka ilivyompokonya rafiki yangu machozi yananidondoka hivi hivi. rafiki wangu Juma alikuwa ametumwa dukani kununua unga na mandazi. Alichukua muda mrefu sana kwani nyumbani nami nikaenda kumwona.

Nilipofika nilimwona kwa umbali akija. Alikuwa akitembea kando ya barabara kuu. Ghafla basi moja, gari lilikuwa likienda kwa kasi, yeye hakuliona gari lile. Lilimpiga na kumrusha juu na kisha akaanguka chini kwa kishindo kama gunia la viazi. Hata gari likapinduka na kugongana na basi la abiria.

Sikuamini nilichokiona. nilidhani kwamba nilikuwa ndoto. Lakini ilikuwa wapi? ulikuwa ukweli mtupu. nilianza kukimbia huku nikipiga mayowe. Kabla nijue hapo umati wa watu ulikuwa umefurika, huku kila mtu akieleza [illegible]. Lakini hakuna aliyekuwa akimsaidia mwenzake, ila kila mtu alikuwa akishangaa kuwaona watu hao.

Nilimwendea rafiki wangu huku nikilia na [illegible] mwili wake ulikuwa umelala mbali na ajali ilipo. Mkono bando [illegible] kamba. mdomo wake ulikuwa umejawa na damu. Wala kabla hatujaona na mimi alipiga damu tena. Msamaria mwema aliyekuwa na simu aliwaita polisi na ambulensi..

Daktari alipofika baadaye walifika na kuanza kuwasaidia abiria ambao majeruhi kwa waliokuwa wengi, si majeruhi si hayupo. Wale waliojeruhiwa vibaya sana walipelekwa hospitali na wengine walipona baada ya kwanza. Nilipatwa na majonzi kila nilipomkumbuka rafiki wangu Juma.

**KIAMBATISHO V**

Ajali ya Ajabu Niliyoshuhudia

Siku moja nilipokuwa nimetembea kwa njia nikaona gari mbili zikiwa zina kimbia kwa haraka. Wakati huo huo gari hizo zilipigana sana mpaka watu kumi wakakufa wengine walipelekwa hospitalini walikuwa mauhututi kwa muda mfupi wakawa wamekufa.

Wakati huo polisi walifika hapo kuangalia na hata umati wa watu ulikuwa hapo. Polisi walichukua yale gari na kumpeleka kwa kituo cha polisi. Polisi wakati walifika walikuta wale abiria walipelekwa hospitalini na watu wengine.

Magari hayo madereva walikuwa walevi kwa sababu hii ajali ilitokea ya ajabu. Sasa wanapolisi walisema yule atapatikana akiwa mlevi nitamsema apewe faini ya au kifungo miaka mitano hii kwa sababu ya pombe.

Abiria nao wanaona madereva walikuwa walevi wanaingia kwa hiyo gari bana wanaona vile gari inaenda kwa mbio wanafurahia kubebwa ili wafike mahali wanapoenda hata hiyo inasababisha ajali.

Hiyo ajali ilisangazasha watu wengi sana kwa sababu hii ajali ilitangazwa kwa redio zetu. Sasa watu ili wakiwa kutumia barabara zetu kwa sababu ajali afao kuisha.

Punde si punde ajali ingine ilitokea kubwa kushinda hiyo kwa barabara Nairobi gari ikiwa imeanguka ikaangukia watu kumi wakakufa na wale waliko ndani ya hiyo gari walikufa wote ikawasangazasha watu wote.